# BUNGE LA TANZANIA

______________

# MAJADILIANO YA BUNGE

______________

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 23 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 704

### Ukarabati wa zahanati katika Jimbo la Kwela

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati zahanati 18 katika Tarafa za Laela, Mpui, Mtowisa na Kipeta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Mheshimiwa David Silinde, kwa niaba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inaendelea kufanya tathmini ya majengo yote chakavu yanayohitaji ukarabati ili yaweze kukarabatiwa na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa zahanati kongwe kote nchini zikiwemo zahanati 18 katika Tarafa za Laela, Mpui, Mtowisa na Kipeta katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na mkakati wa jumla wa Serikali wa kukarabati zahanati 18 ndani ya Jimbo la Kwela lakini katika Kijiji cha Kavifuti, Kata ya Miangalua na Kijiji cha Kiandaigonda zahanati zake ni kama magofu kabisa zimechakaa. Je, Serikali wana mpango gani wa dharura kunusuru walau wananchi wapate huduma sehemu iliyo salama?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wa Kijiji cha Kapewa, Mtetezi, Mumba pamoja na Mtapenda wametumia nguvu kubwa kujenga zahanati ambayo imebaki fedha kidogo kumalizia. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka fedha ili wananchi wapate huduma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa anafanya kazi nzuri sana kuwasaidia

wananchi wa Jimbo lake la Kwela hususan katika kufatilia haya masuala ya zahanati. Bahati nzuri maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge, anayataja hata mimi binafsi nimewahi kufika na nimeona hiyo changamoto na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishaahidi kuyafanyia kazi. Katika sehemu ya mpango wa dharura hususan katika maeneo ya Miangalua, maeneo ya Mpui hayo yapo katika mpango wa Serikali. Kwa hiyo kikubwa sasa ni kuendelea kuyafuatilia ili yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Mtapewa ambapo kuna nguvu kubwa ya wananchi moja ya mpango wa Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ambayo wananchi wameweka nguvu yao, itapeleka fedha kwa ajili ya kumalizia maboma hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa afya za wananchi ni muhimu na ni uwekezaji wa Serikali kwa ajili ya nguvu kazi, kumekuwa na jitihada za wananchi kujenga zahanati katika maeneo mbalimbali kwa nguvu zao na kumekuwa na bajeti ndogo kwenye halmashauri baadhi ambazo hazina uwezo. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuweza kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia zahanati zilizojengwa na wananchi katika maeneo yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kama nilivyojibu kwenye swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, kwamba moja ya mkakati wa Serikali hususan katika maeneo ambayo kuna nguvu za wananchi ni kupeleka fedha na kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kutafuta fedha kwa ajili ya kumalizia maeneo ambayo wananchi wameweka nguvu zao. Kwa hiyo katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameyaainisha yapo katika mpango ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini sasa aulize swali lake. Mbunge yeyote wa Tabora aliyeko humu ndani? Haya, simwoni Mbunge yeyote wa Tabora.

Tunaendelea, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 706

**Kupandisha hadhi barabara ya Kalenga kuelekea Madibila**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara kutoka Kijiji cha Kalenga kupitia Kata za Ulanda, Maboga, Wasa - Madibila zitapandishwa kuwa za Mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007, kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya Mwaka 2009, Kifungu cha 43(1) na (2) na kifungu cha 44(1) kupitia Tangazo la Serikali Namba 21 la tarehe 23 Januari, 2009, limeainisha vigezo vya utaratibu wa kupandisha au kuteremsha hadhi barabara toka daraja moja kwenda daraja lingine.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya upandishaji hadhi wa barabara hii ulifanyika mwaka 2019 na Wizara Ujenzi na Uchukuzi, yalibaini barabara hiyo kukosa sifa kama barabara ya mkoa

*(regional road)* na hivyo kupewa hadhi ya barabara za Wilaya katika kundi la mkusanyo *(collector roads)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Barabara ya Kalenga – Wasa - Mafinga ni barabara muhimu sana kwa uchumi katika Mkoa wetu wa Iringa. Je, katika kilometa 100 za Mradi wa *RISE* kwa nini wasipatiwe japo kilometa 10 tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Barabara ya Itimbo – Kitelewasi inapita katika milima na miteremko mikali, hivyo inahitaji kujengewa makalavati. Je, Serikali ipo tayari sasa kujenga makalavati ili wananchi wa Kitelewasi na Itimbo waweze kupita kwa uraisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA MIFUGO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Sika, ahsante sana. Kwanza natambua kwamba kuna mahitaji makubwa ya ujenzi wa barabara hususani katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha. Barabara ya Kalenga mpaka Mafinga ambayo ina urefu wa kilometa 100 hususani hizi za *RISE* na amekuwa akiomba kilometa kumi, niseme tu kwamba zile barabara zimeshawekwa katika mpango wake. Kwa hiyo kikubwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI itazingatia katika mipango ijayo ili kuona sasa tunatafuta hizo kilometa 10 waweze kujenga katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Itimbo – Kitelewasi ambayo ina mteremko mkali, mahitaji ya Kalavati, nafikiri kwa kutumia fedha za Mfuko wa Dharura, Ofisi ya *TARURA* Mkoa wa Iringa tuwaelekeze tu kwamba kulingana na mahitaji ya maeneo hayo, waipe kipaumbele barabara hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu nikuombe Mawaziri na Naibu Mawaziri wanapokuwa hawapo wa Wizara inayohusika, Ofisi yetu ijulishwe ili maswali yao yasipangwe. Kwa sababu yakipangwa tunapunguza maswali ya Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu anayejibu ni wa Wizara nyingine, wakiwa ni wawili wa Wizara moja ni afadhali, akiwa anatoka nje ya Wizara kabisa inakuwa ngumu sana Wabunge waliosimama kuwapa nafasi, kwa sababu Mbunge anaweza akauliza mkakati wa Serikali.

Sasa mkakati wa Serikali Naibu Waziri mwingine anaweza asiujue kwenye hilo eneo pamoja na kwamba Serikali ni moja. Kwenye hoja ya maswali nadhani tukiwasiliana vizuri, tutaondoa hii changamoto ya Waheshimiwa Wabunge, kunyimwa maswali ya nyongeza Naibu Waziri wa Wizara nyingine anapojibu. *(Makofi)*

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Idd Kassim Idd, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa haya, Msalala si ni Shinyanga Mheshimiwa? au Singida?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Hapana, ila naomba niulize kwa niaba yake.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Miraji Mtaturu kwa niaba ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. *(Kicheko)*

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala ambaye kwa sasa amekwenda Hija, naomba swali lake sasa lijibiwe kwa niaba ya wananchi wa Msalala.

Na. 707

**Hitaji la mtaro Kata za Bulyanhulu, Segese, Ngaya na Bulige**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga mitaro ya kuchepushia maji katika Kata za Bulyanhulu, Segese, Ngaya na Bulige?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Idd Kassim Idd, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Bulyanhulu na Segese zinapitiwa na Barabara ya Kahama hadi Kakola ambayo ipo kwenye mpango wa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2023/2024. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea na ujenzi wa mitaro utafanyika wakati wa utekelezaji wa mradi huo. Aidha, Mji Mdogo wa Bulige unapitiwa na Barabara ya Kahama – Solwa ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea na utahusisha ujenzi wa mitaro. Vilevile, mitaro iliyopo katika Kata ya Ngaya inakidhi mahitaji ya barabara hiyo na itaendelea kufanyiwa matengenezo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa sababu suala la ujenzi wa barabara tunatumia fedha nyingi na maeneo mengine mvua zimekuwa zikiharibu miundombinu hii, hii ni kwa sababu labda hatukufanya *design* au hatukufanya utafiti wa kutosha kwenye athari ya kimazingira. Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba kabla ya ujenzi wa miundombinu hii ambayo inatumia gharama kubwa kuangalia athari za kimazingira zisilete matatizo katika miundombinu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Mtaturu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara na hasa hizi za udongo na za changalawe mara nyingi zinaharibika hasa kipindi cha mvua na Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa ajili ya kufanya ukarabati na hasa kutengeneza mitaro na mifereji ili kutoa hayo maji, kwa sababu moja ya chanzo kikubwa cha kuharibu barabara ni maji. Pia Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kutotumia barabara kwenye hifadhi za barabara na kupitisha mifugo kwenye barabara. Kwa sababu hicho pia ndiyo chanzo kikubwa cha kufanya uharibifu wa barabara, kwa sababu ukishalima karibu na barabara unatuamisha maji na hivyo barabara zinaharibika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Barabara ya Kagoma – Biharamulo katika Mji wa Muleba pale, walielekeza maji kwenye makazi yatu ambapo wamechimba mtaro mkubwa ambao unajulikana kama Buhimba, lakini Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wakati wa Kampeni 2020 - 2025 alitoa maelekezo mahususi kwamba Mamlaka zinazohusika wakae…

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** ...tumalize hilo tatizo. Je ni lini Mamlaka ya *TANROADS* itakuja kumaliza tatizo la maji katika eneo la Buhimba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sababu yalikuwa ni maelekezo mahususi na kuhusu eneo mahususi, naomba pia kutumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Kagera aende kwenye eneo lililokuwa limetolewa maelekezo na Mheshimiwa Rais, kutoa ama kuyatoa maji yaliyokuwa yameelekezwa kwenye makazi ya watu na kuyapitisha kwenye njia sahihi. Nimwombe atakapokuwa anafanya hivyo aweze kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ambaye ametoa hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 708

**Ujenzi wa barabara ya Mpanda – Uvinza**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Mpanda hadi Uvinza yenye kilometa 159 utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mpanda hadi Uvinza yenye urefu wa kilometa 194 kwa awamu. Ujenzi wa Barabara ya Mpanda hadi Vikonge kilometa 37.6 umekamilika na ujenzi wa sehemu ya Vikonge hadi Luhafwe kilometa 25 unaendelea. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Luhafwe hadi Mishamo unatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Kwa sehemu iliyobaki ya Mishamo – Uvinza kilometa 94, Serikali iko kwenye mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuruhusu bakaa

ya fedha za Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Koga hadi Mpanda zitumike katika ujenzi wa sehemu hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Restuta Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inatuongezea pesa na wakandarasi zaidi ya mmoja, wawe watatu ili Barabara ya Mpanda – Kigoma ikamilike ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kufunguka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, mazungumzo hayo na Benki ya Afrika yatakamilika lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika taratibu za kandarasi inategemea na mlivyopanga *lots* ama vipande na vipande tunavyovijenga hakuna ambacho kwa sasa kinazidi kilometa 50.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika hivyo vipande vitatu vinavyojengwa kila kipande kina mkandarasi lakini tunategemea katika swali lake la pili kama *African Development Bank* tutakuwa tumekubaliana nao kutumia bakaa iliyobaki kukamilisha hiyo barabara kwa urefu wa kilometa 94 ni wazi kwamba hatutakuwa na mkandarasi mmoja tutakuwa na zaidi ya mkandarasi mmoja ili kukamilisha kazi kwa haraka kati ya Mpanda na Uvinza kwa kilometa 94 ambazo zimebaki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 709

**Ujenzi wa barabara ya Mbuguni Tengeru Sokoni – Arumeru hadi Mererani**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Mbuguni kuanzia Tengeru Sokoni, Arumeru hadi Mererani utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Tengeru Sokoni – Arumeru hadi Mererani yenye urefu wa kilometa 28 ambapo *TANROADS* wanaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itakamilika Agosti, 2023. Baada ya usanifu kukamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha Mikoa miwili, Arusha na Manyara pia ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa. Sasa barabara hii kwa unyeti wake iko *busy* na imekuwa ni changamoto kubwa sana ya afya kwa wanachi walioko katika barabara hii kwa sababu ya vumbi. Naomba *commitment* ya

Serikali kwamba; Je, ni lini ujenzi utaanza kwa sababu kuna fedha nyingi, kuna mpango wa *RISE,* kuna *Agri - connect*. Je, Serikali haiwezi ikafanya utaratibu barabara hiyo ianze kujengwa mara moja baada ya usanifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili...

**SPIKA:** Nimezisikia je mbili hapo au je zote zilikuwa zinahusu swali moja?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ni swali moja tu.

**SPIKA:** Maana nimesikia je mara mbili. Sasa usije ukamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali matatu.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ni moja tu linahusu barabara hiyo hiyo.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna ahadi nyingi sana za Serikali, Viongozi Wakuu za ujenzi wa barabara kwa viwango vya lami, na mojawapo ni barabara ya King'ori kutoka Malula hadi Ngarenanyuki. Barabara hii ilikuwa ahadi ya…

**SPIKA:** Uliza tu swali Mheshimiwa.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize barabara ya King'ori kutoka Malula hadi Ngarenanyuki lini itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ni ahadi ya Viongozi Wakuu wa Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *commitment* ya Serikali imeshaonekana na ndiyo maana tayari tumeshaanza taratibu za kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami tukitambua kwamba inaenda kwenye sehemu muhimu sana ya kiuchumi eneo la mgodi wa Mererani lakini pia inaunganisha kama alivyosema Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara. Isingekuwa rahisi kufanya chochote kabla ya kukamilisha usanifu. Kwa hiyo, kama fedha inaweza ikatokea yoyote katika kipindi hicho tutafanya, vinginevyo ni kwamba baada ya kukamilisha usanifu basi tutaipangia bajeti kwa mwaka ujao wa bajeti kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu hii barabara aliyoitaja. Ni kweli barabara ya King'ori – Ngarenanyuki ilikuwa inatengenezwa na wenzetu wa *TARURA* tumekasimiwa, kwa hiyo tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu inapita kwenye maeneo makubwa sana ya uzalishaji wa wenzetu ambao ndiyo wanalisha Mji wa Arusha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mpango wa Serikali ni kuunganisha kwa kiwango cha lami kutoka Wilaya kwenda Mkoa. Waziri ni lini Serikali itaanza kujenga barabara Halmashauri ya Wilaya Mbogwe kwenda Geita Makao Makuu ya Mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maganga Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli huo ndiyo mpango na bahati nzuri barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge zitafadhiliwa na wenzetu wa *World Bank* kupitia mradi wa *RISE* ambao sasa hivi wanakamilisha kufanya *review* ya usanifu wa barabara za kuiunganisha Wilaya ya Mbogwe na Wilaya ya Geita kwa kiwango cha lami. Tunategemea kuanzia mwaka ujao wa fedha kwa sababu taratibu zinaendelea na ni fedha za *World Bank,* mara baada ya kukamilisha hizo taaratibu ujenzi utaanza kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa kusaini mkataba wa Barabara ya Sengerema kwenda Nyehunge klilomita 54 lakini awali barabara ile ilisomeka Sengerema - Nyehunge na kipande cha Kahunda kilometa 32. Kilometa 32 za Nyehunge - Kahunda zimeondolewa.

Je, Serikali inaweza kutoa *commitment* ya kwamba kilometa 32 za Nyehunge - Kahunda pamoja na kipande cha Bukokwa – Nyakalilo zitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la, Mheshimiwa Mbunge Shigongo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii katika *design,* ili - *design* – wa kilometa zote mpaka hizo kilometa 32 kwenda Kahunda. Lakini tumeanza kuzijenga kulingana na upatikanaji wa bajeti na ndiyo maana *commitment* ya Serikali tayari tumeshasaini kipande hicho cha kilometa kuanzia Sengerema hadi Nyehunge kwa kuanzia na tukitegemea kwamba pengine katika mwaka wa fedha ujao, basi tutakamilisha hizo kilometa zote zilizobaki kwa sababu ndiyo mapango wa Serikali kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sengerema - Buchosa inaunganisha na Mkoa wa Geita kipande kidogo tu cha kilometa 14 kutoka Nyehunge kwenda Nzela, Serikali imeishia Nyehunge.

Je, Serikali ina mapango gani kuunganisha kutoka Nyehunge kwenda Nzela ambako Mheshimiwa Waziri unapita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba tuna kila sababu ya kuunganisha Mkoa na Mkoa. Bahati nzuri hiyo barabara mimi nimeipita, kama nilivyosema kwamba mpango wa Serikali ni kuziunganisha Mkoa na Mkoa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kadri fedha itakavyopatikana barabara hii ya kutoka Nyehunge hadi Nzela kipande kilichobaki pia kitajengwa kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na Nzela hadi Kome ambayo iko kwenye hatua za manunuzi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 710

**Kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza afua kuu zifuatazo katika kutokomeza ugonjwa wa Malaria: -

(i) Udhibiti wa mbu waenezao Malaria kupitia njia kuu zifuatazo:-

   (a) Kusambaza vyandarua vyenye dawa kwa jamii kupitia kampeni za kugawa vyandarua kwa kila kaya; kliniki za mama wajawazito, watoto na vituo vya kutolea huduma kwa makundi maalum kama wazee.

   (b) Upuliziaji wa dawa ukoko kwenye kuta ndani ya nyumba katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria.

   (c) Unyunyiziaji wa viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ili kuuwa viluilui wa mbu.

(ii) Kuhakikisha vipimo na dawa za malaria zinapatikana wakati wote katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vipimo na dawa za Malaria zinapatikana bila malipo kwenye vituo vyote vya kutolea huduma vya Serikali.

(iii) Kuhamasisha jamii kutumia njia mbalimbali za kujikinga na ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha kufikiwa kwa azma ya kutokomeza ugonjwa wa malaria hapa nchini, Serikali imeanzisha

Baraza la Kutokomeza Malaria *(End Malaria Council)* lililozinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 25 Aprili, 2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kagera una maambukizi makubwa ya Malaria, ni namba tatu kwa maambukizi makubwa Kitaifa na kwa kuwa Wilaya ya Ngara ndiyo inayoongoza katika maambukizi ya Malaria Mkoani Kagera. Je, ni lini sasa Serikali itatusaidia kufanya unyunyiziaji wa viuatilifu *(Indoor Residual Spraying)* katika Wilaya ya Ngara ili kupunguza maambukizi ya Malaria?

Swali la pili, kwa kuwa zipo nchi duniani ambazo tayari zimeshatokomeza kabisa Malaria. Je, ni lini Tanzania tumelenga ni mwaka gani tutakuwa tumefikia *zero* Malaria, kwa maana ya kutokomeza kabisa Malaria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kuhusu Mkoa wa Kagera. Ni kweli kwamba Mkoa wa Kagera ni Mkoa wa tatu una asilimia 18 ukiongozwa na Tabora wenye asilimia 23 ukifuata Mtwara. Ni kweli Ngara inaongoza na tulikwenda na tunao ushirikiano na wenzetu wa Rwanda katika kutokomeza na tumeshajenga vituo upande wa Tanzania na upande wa Ngara kwa ajili ya kuweka utaratibu.

Mheshimiwa Spika, moja ni huu ambao amesema kunyunyuzia hiyo dawa, lakini tunafikiria kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anazindua Malaria *Council* alielekeza

kwamba tuandike Wizara ya Fedha tuoneshe tunahitaji shilingi ngapi kwa ajili ya kununua zile dawa za kuua viluilui na tayari tumeshafanya na tumewasilisha Wizara ya Fedha bilioni 22 kwa ajili ya nchi nzima na mojawapo Ngara kwa maana ya Mkoa wa Kagera ikiwepo ni sehemu ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu ni lini tutaweza kutokomeza Malaria. Kwanza nikuhakikishie kabisa kuna Mikoa zaidi ya tisa sasa ni chini ya asilimia moja Malaria kwenye nchi yetu, na Mikoa mingi sana imeshuka. Kwa hiyo, tunadhani mpaka 202030 nchi yetu nayo itafikia kwenye kiwango cha hizo nchi nyingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hapo uliposema 202030 hiyo ni miaka mingi sana au ulimaanisha 2030? Mheshimiwa Naibu Waziri hujawasha kisemeo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni mwaka 2030.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 711

**Kusimamia na kufuatilia mipango na bajeti zinazopitishwa**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, Serikali inatumia utaratibu gani kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango na Bajeti zinazopitishwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali husimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango na bajeti zinazopitishwa na Bunge kwa utaratibu ufuatao: -

(a) Wizara ya Fedha na Mipango kila mwaka huandaa na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali;

(b) Kutoa Waraka Na.1 wa Mwaka wa Fedha wa utekelezaji wa bajeti unaoelekeza na kusisitiza utekelezaji wa vipaumbele;

(c) Kuandaa mwongozo wa maombi na utoaji fedha kwa lengo la kuhakikisha fedha inatolewa wakati wa uhitaji na inatumika kwa wakati;

(d) Kusimamia uwasilishwaji wa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti na ambazo huchambuliwa ili kutathmini utekelezaji wa mipango kwa kuoanisha na malengo tarajiwa na bajeti zilizotengwa; na

(e) Kubainisha viashiria hatarishi vya utekelezaji wa bajeti na kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kujiridhisha na uhalisia na kuchukua hatua stahiki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kusuasua kwa utekelezaji wa bajeti kadri tunavyotenga kwenye Bunge hili kipindi cha bajeti, wakati mwingine kuchelewa kufika au kufika kwa asilimia ndogo. Sasa naomba kufahamu mkakati wa Serikali kutatua

changamoto hii, kwa sababu tukitenga bajeti tunatarajia ifike kama tunavyotenga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Natamani kufahamu mpaka sasa hivi Serikali imechukua hatua gani kwa Watendaji ambao wamekuwa siyo waaminifu na wabadhilifu wa mali za umma hususan bajeti kadri tunavyotenga badala ya kusubiri taarifa ya *CAG* pamoja na Mwenge? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa fedha kama zilivyotengwa katika bajeti kadri ya fedha zinavyopatikana. Kwa kuwa, mfumo wetu wa bajeti ni *cash budget,* pesa zitakusanywa ili ziweze kutumika katika bajeti, hivyo Serikali itaendele kukusanya na kuongeza uwezo wa ukusanyaji wa mapato ili tuweze kutekeleza bajeti kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili. Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa wale watumishi ambao siyo waadilifu. Hatua hizo ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani, wako wale ambao wamefungwa sasa, wako ambao wamesimamishwa kazi na wako ambao wamefukuzwa kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali sasa haioni kuwa ni wakati muafaka wa kukitumia kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuweza kufatilia bajeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inakitumia ipasavyo kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani na tumekiongezea uwezo mwaka huu uliopita na mwaka ujao tumetenga kuongeza uwezo wa kufanya ukaguzi unaostahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Moja ya eneo ambalo Serikali inatekeleza chini ya asilimia 50 kwenye bajeti na mpango ni ahadi za Viongozi wa Kitaifa.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kumaliza ahadi zote za Viongozi wa Kitaifa za miaka ya nyuma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, samahani sijamuelewa.

**SPIKA:** Amesema hivi Viongozi Wakuu wa nchi wanatoa ahadi nyingi. Katika zile ahadi kwa tathmini yake utekelezaji uko chini ya asilimia 50. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha ahadi za hao Viongozi zote zinatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha mawasiliano lakini inaendelea kuimarisha makusanyo ya fedha, na hivi nimuombe Mheshimiwa Mbunge naye awe ni Balozi wa kushawishi na kuwashauri wafanyabiashara pamoja na yeye na mimi kuendelea kukusanya kodi ili tuweze kutekeleza ahadi za viongozi wetu kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu. Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 712

**Kuondoa mianya kwenye ukadiriaji wa kodi**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, ni lini mianya ya majadiliano yanayopelekea rushwa kwenye mfumo wa ukadiriaji wa kodi kwa Wafanyabiashara itaondolewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ukaguzi na makadirio ya kodi huongozwa na Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 na Kanuni zake, pamoja na miongozo inayotolewa na Serikali kupitia *TRA*. Hivyo, mawasiliano yote yanayofanyika baina ya *TRA* na Mlipakodi kabla ya makadirio ya kodi kutolewa yanaongozwa na misingi iliyotajwa hapo juu. Aidha, *TRA* inachukua hatua mbalimbali ili kuondoa mianya ya rushwa kama ifuatavyo: -

(i) Kutoa elimu kwa walipa kodi kujua haki na wajibu wao;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa sera ya maadili kwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(iii) Kurahisisha utoaji wa taarifa za watumishi wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kupitia tovuti na kupiga simu kupitia namba za simu zisizo na gharama; na

(iv) Kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali katika kuelimisha, kuzuia na kushughulikia vitendo vya ukiukwaji wa maadili ndani ya mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuunda, kutumia na kuimarisha utendaji kazi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kupunguza vitendo vya ubadhilifu na rushwa vinavyosababishwa na utaratibu wa kuonana ana kwa ana kwa Afisa wa Kodi na Mlipa Kodi wakati wa ukadiriaji wa mapato. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika taasisi ambazo zinalalamikiwa sana kwa uonevu na kukithiri kwa rushwa ni pamoja na *TRA,* hili linasababishwa na kujadili kodi ana kwa ana kupitia utaratibu wa sasa. Sasa kwa kuwa taratibu hizi zimekuwepo kwa miaka 22 iliyopita, *TRA* haioni kwamba inahitaji mabadiliko ya haraka ya kuondoa mawasiliano ya ana kwa ana ili kudhibiti jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; dunia sasa inafanya biashara zaidi kupitia mitandao na imethibitika kwamba *TRA* bado wanaendesha makadirio yao kianalogia. Ni hatua zipi za haraka ambazo inachukua ili kuweza kukusanya kodi ambayo inapotea kwenye mitandao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kanyasu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa ipo changamoto ya mifumo na ipo changamoto hiyo ya kukutana ana kwa ana kati ya Mlipa Kodi na Afisa Kodi. Serikali hatua ambayo imechukua ni kuimarisha mifumo kuhakikisha kwamba

Mlipa Kodi na Afisa Kodi hawatokutana ana kwa ana ili kuepusha hiyo mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili. Serikali kupitia Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya sheria pamoja na kuanzisha Kitengo Maalum kwa ajili ya kusimamia kodi za biashara, mtandao na kuhakikisha kwamba utambuzi wa mfanyabishara ya kimtandao amesajiliwa na kulipa kodi inayostahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 713

**Hitaji la Kituo cha Polisi – Ngaramtoni**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Ngaramtoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Polisi haina eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi na nyumba za

makazi ya Askari. Tunazo taarifa kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni inaendelea na mchakato kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kupata eneo na kutenga kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za taasisi za umma ikiwemo Kituo cha Polisi na nyumba za makazi ya Askari. Pindi eneo hilo litakapopatikana Wizara itatenga fedha za ujenzi wa kituo na nyumba za makazi ya Askari kupitia Jeshi la Polisi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, eneo linalotumiwa na Kituo Kidogo cha Polisi cha Ngaramtoni linatumiwa tangu mwaka 1984 ambalo liko chini ya Wizara ya Kilimo; je, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haioni ni vizuri sasa wakaomba eneo hilo ili waweze kurasimishiwa moja kwa moja badala ya kusema hawana eneo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Jeshi la Polisi ndiyo limepewa mamlaka ya kuangalia raia na mali zao: Je, Serikali inaona ni vizuri Askari kukaa kwenye makuti bila nyumba wala Kituo cha Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mambo ya Ndani kuzungumzia suala ambalo limetengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na sasa limekosa kibali cha watu wa Polisi kujenga, mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara hizi mbili ili kupata kibali cha kuhalalisha hilo eneo ili liweze kujengwa Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili eneo la usalama wa mali za wananchi, Polisi wanatambua umuhimu mkubwa kabisa wa

usalama wa wananchi na mali zao, na hivyo basi ndiyo maana msukumo wa mazungumzo unaendelea kati ya hizi taasisi mbili ili kuweza kuhalalisha hiyo eneo na badae kujenga kwa ajili ya usalama wa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Naona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo umesimama.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nimshauri Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru wakakae na Halmashauri yao watafute eneo. Eneo la Wizara ya Kilimo linatumika kwa ajili ya wafanyakazi wa utafiti na pale tuliwapa hifadhi ya muda, watafute eneo lingine. Wizara haitatoa kipande cha ardhi cha uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 714

**Kulinda ardhi ya kilimo kisheria**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria wa kulinda ardhi ya Kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kulinda ardhi ya kilimo kama ilivyobainishwa katika Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013. Kwa msingi huo, Wizara inapitia na kuchambua

Sheria Mbalimbali zinazohusiana na usimamizi na matumizi ya ardhi ya kilimo ikiwemo Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi, Sura ya 116 na Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Sura ya 118.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo utabainisha upungufu uliopo katika sheria hizo na kuainisha maeneo ambayo yatajumuishwa kwenye Sheria ya Maendeleo ya Kilimo inayopendekezwa kutugwa ambayo itakuwa na sehemu ya masuala ya usimamizi wa ardhi ya kilimo. Baada ya uchambuzi huo wa kitaalam, itawasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kuhusu mapendekezo ya sheria hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nataka kumkumbusha tu kwamba, pamoja na kwamba nchi yetu kuwa na ukubwa wa eneo lenye *square kilometer* 947,300 eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta milioni 44 tu.

Je, Serikali haioni wakati umefika kuharakisha kutunga sheria itakayolinda eneo hili la kilimo ili lisije likavamiwa kwa shughuli nyingine? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuilinda ardhi kwa ajili ya kilimo. Kama nilivyosema hapa, tumeamua kupitia baadhi ya sheria ili mwisho wa siku tuje na sheria ambayo imekamilika. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaharakisha mchakato huu ili mwisho wa siku tupate sheria yetu ya kilimo, tutunze ardhi ya kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza namshukuru Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu yake mazuri aliyoyajibu kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, lakini nilichotaka kusema tu ni kwamba, Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Kilimo tumeshaanza mchakato wa kuyatambua yale maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo. Kwa hatua ya kwanza itakayofanyika ni kuya-*gazette* ili yasiweze kuingiliwa na watu wengine. Kwa hiyo, *stage* nyingine itakayofuata ndiyo hiyo ya kutunga sheria ili kuyalinda kwa ajili ya uhifadhi wa kilimo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rugwe, sasa aulize swali lake.

Na. 715

**Kupeleka umeme wa *REA* – Rungwe**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Umeme wa *REA* katika vijiji na vitongoji ambavyo vimeshawekewa nguzo Jimbo la Rungwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rungwe, mkandarasi *M/S State Grid Ltd.* anakamilisha maandalizi ya vifaa vya ujenzi wa maeneo yaliyobaki na kazi zinatarajiwa kuanza tarehe 1 Julai, 2023 na kukamilika mwezi Oktoba, 2023. Pamoja na miradi mingine katika bajeti ya mwaka 2023/2024, kila Jimbo limetengewa bajeti ya kupelekewa umeme katika vitongoji 15 vya kuanzia wakati maandalizi ya mradi wa *Hamlet Electrification Project (HEP)* unaotarajiwa kuanza mwaka 2024/2025 yanakamilika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipate ufafanuzi zaidi kwenye jibu la msingi. Mkandarasi anayetekeleza mradi sasa hivi kule Rungwe ni *ETDCO* siyo *State Grid Limited.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi zaidi kwamba, huyu *State Grid Limited* ameingiaje hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwenye *REA II* kuna vijiji 25 viliachwa, vilitelekezwa, yaani kama viporo; napenda nijue kwamba ni lini huu Mradi wa *REA II* vijiji 25 utaanza kutekelezwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkandarasi *ETDCO* ndio yuko *site* na Mkandarasi *ETDCO* anatekeleza Mradi wa *REA III Round II.* Ndiyo mradi unaoendelea ambao ni mkubwa ambao *ETDCO* anautekeleza na tunatarajia itakapofika Desemba atakuwa amemaliza kwa sababu, ni katika ile azma ya kuhakikisha vijiji vyote vinapata umeme ifikapo Desemba.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili sasa lililosema la vijiji 25 ambavyo vilikuwa vimeachwa na *REA* Awamu ya Pili tulikuwa tuna mabishano na mkandarasi kuhusu wigo wa utekelezaji na namna ya utekelezaji. Kuna maeneo alisimamisha nguzo, kuna maeneo aliweka waya halafu akaondoka, baada ya mvutano wa muda mrefu, ndiyo sasa tumemrudisha yeye mwenyewe, huyu

huyu *State Grid,* ili aje kukamilisha vile vijiji vyake 25 ambavyo alikuwa ameviacha. Ndiyo maana tunasema ataanza Julai na atamaliza mwezi wa Kumi wakati *ETDCO* alianza tangu mwaka juzi, atamaliza Desemba mwaka huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji vya Kata ya Shizuvi ambavyo ni sehemu ya *REA* Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo viko kwenye Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, vitakamilika ifikapo Desemba mwaka huu wa 2023. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Oran Manase Njeza kwamba vijiji hivyo pia katika kata hizo vitakuwa vimefikiwa na umeme kabla ya Desemba mwaka huu 2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika vijiji 15 alivyovitaja vya vitongoji kumekuwa na changamoto kidogo kwa sababu, tulishapeleka vijiji 15 wakasema kwamba vijiji hivyo havitambuliki na TAMISEMI, lakini pia wakatoa *condition* nyingine kwamba vijiji hivyo lazima vipitiwe na mkondo mkuu wa waya.

Je, Serikali inatoa maelezo gani ya msingi kwa sababu inaonekana kule wale watendaji hawana uhakika wa kitu gani cha kutekeleza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa najaribu kusikiliza kama swali lako linahusiana na swali la msingi au Hapana? Maana umetoa maelezo ya ziada hapo mwanzo yanayokuondoa kwenye swali la msingi. Swali lako ni nini? Uliza swali bila maelezo, itakusaidia kuwa kwenye swali la msingi

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, vitongoji 15 alivyovitaja kwamba ndiyo vinatakiwa vipitiwe kwa *level* hii ya umeme aliyoisema sasa hivi kunakuwa na mkanganyiko, wale watekelezaji hawajui kwamba watekeleze vipi? Kwa sababu, ukiwapelekea vitongoji wanasema ah, ah, vitongoji hivi havistahili kwa sababu, hakuna umeme. Sasa je, kuna *condition* ya vitongoji au hakuna *condition* kwamba, vitongoji vyovyote vinaweza kuwekewa au kuna *condition* fulani lazima ndiyo vipelekewe huo umeme?

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, katika vitongoji 15 ambavyo tumepata fedha ya kuvipelekea umeme katika mradi huu utakaotekelezwa mwaka 2023/2024 nieleze wazi kwamba ni vitongiji ambavyo tunaviita *underline*. Ni vitongoji ambavyo tayari miundombinu ya umeme mkubwa ilishapita katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwenye kijiji kimoja chenye vitongoji labda vitano, vitongoji viwili vimefikiwa na miundombinu kwa maana ya kuwashwa, kitongoji kimoja miundombinu imepita kwa juu haijashuka kwenye kile kitongoji na labda vitongoji vingine viwili havijafikiwa kabisa na umeme mkubwa na havijafikiwa na umeme mdogo.

Mheshimiwa Spika, fedha hii ndogo tuliyoipata Shilingi bilioni 379 inatosha kwa kupeleka miundombinu ya umeme mdogo tu katika yale maeneo ambayo tayari miundombinu ya umeme mkubwa ilishapita. Kwa hiyo, wale watendaji wenzetu kule chini wanayo maelekezo haya na wanajua namna ya kuwasilisha maelezo haya. Wataleta vile vitongoji ambavyo vilishapitiwa na *line* kubwa, sasa tunashusha umeme kwa ajili ya kujazia katika maeneo hayo. Pia mwaka 2024/2025 kwenye mradi wetu mkubwa wa *HEP* wa shilingi trilioni sita hapo tutakwenda kumaliza vitongoji vyote ambavyo vilishafikiwa na ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu mliwapa uhuru Waheshimiwa Wabunge kwamba vile vitongoji 15 wao ndio wachague ni wapi? Sasa upo uwezekano Mbunge akachagua kule ambako umeme hakuna kabisa ili ndiyo uende sasa kule. Kwa hiyo, huu ufafanuzi unaoutoa sasa nafikiri ni muhimu pengine kutafuta maelezo ya kitaalamu kabisa ili uwape Waheshimiwa Wabunge pengine kwa maandishi ili na wao ule uchaguzi mliowapa na ule uhuru wajue ile mipaka yake. La sivyo, hili swali litajirudia sana ndani ya mwaka wote huu, kwa sababu mtu atasema vitongoji nilivyoleta siko mlikopeleka umeme. Kwa hiyo, mkitoa maelezo ya jumla kwa Waheshimiwa Wabunge, walielewe hilo ili wanapoleta vitongoji vifuate hayo maelekezo unayotoa, itaondoa huu mkanganyiko ambao anausema Mheshimiwa Mchungahela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Katika Kata ya Tarada, Kijiji cha Ngunga upo mradi wa nguvu za jua ambao ni wa gharama ya shilingi bilioni 275. Zoezi la kulipa fidia kwa waathirika bado limeanza kusuasua kutokana na changamoto ya migogoro ya maeneo.

Je, Waziri yuko tayari kufika katika eneo hilo ilimradi kutatua kwa haraka tatizo hilo na mradi huu uanze kutekelezwa kwa haraka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ameuliza kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufika katika eneo hilo, ninayo hakika kwamba dhati ya moyo wake, lakini na sisi wasaidizi wake Wizarani tutafika na kuweza kuona tatizo ni nini kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi ili tuweze kulitatua. Kwa kuonesha nia ya dhati, tayari na mkataba wa utekelezaji wa mradi ule umeshasainiwa. Hivyo, hizi changamoto nyingine ambazo zitazuia utekelezaji hatuwezi kukubaliana nazo. Tutafika ili tutatue tatizo na mradi uanze mara moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona mliosimama, lakini muda wetu siyo rafiki sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 716

**Kuwezesha vijana kunufaika na Ziwa Victoria**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa kuongeza nguvu kwenye uvuvi ili vijana wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa wanufaike na Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi boti za kisasa kwa mkopo usio na riba kupitia Benki ya Kilimo Tanzania *(TADB)*. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na *TADB* inakamilisha taratibu za kutoa maboti 158 kwa mkopo kwa Vyama vya Ushirika 45, Vikundi vya Wavuvi 71 na watu binafsi 43 ambao wengi wao ni vijana. Aidha, katika Ukanda wa Ziwa Victoria, jumla ya Vyama vya Ushirika 20 kwa maana ya Mkoa wa Mwanza 14, Vikundi 17 kwa maana ya Mkoa wa Mwanza 10, na watu binafsi 17 kwa Mwanza wanne, wanatarajiwa kunufaika na mkopo wa maboti hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imetenga fedha kwa ajili ya miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria

kwa kuwawezesha vijana kupata pembejeo za ufugaji samaki kwa mikopo isiyo na riba. Aidha, jumla ya wanufaika 3,154 ambao wengi wao ni vijana wameainishwa kunufaika na mkopo huo ikijumuisha vikundi 67, kwa maana ya Mwanza 42, vyama vya ushirika 24, Mwanza 14; kampuni 10, kwa Mkoa wa Mwanza vitano; na watu binafsi 32, kwa Mkoa wa Mwanza 16 kutoka ukanda wa Ziwa Victoria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona *potential* iliyoko kwenye Ziwa Viktoria na haja ya kulitumia ziwa hili kuweza kutatua changamoto za kiuchumi na ajira kwa vijana walioko katika Kanda ya Ziwa na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza fedha hizi zimetengwa takribani Shilingi bilioni 20 kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na tunavyozungumza sasa utaratibu ulianza tangu mwaka 2022 na sasa tumebakiwa na kama siku saba tu kumaliza mwaka huu wa fedha 2022/2023; naomba *commitment* ya Serikali: Ni lini hasa utekelezaji wa mradi huu utaanza kwa sababu, taratibu zote za awali zimeshatimia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa vile tayari kuna sintofahamu na changamoto fulani kwa vijana wa Mwanza na Mikoa yote ambayo inahusika na mradi huu ambazo baadhi yake nilizungumza jana: Je, Serikali au Waziri na wasaidizi wake wako tayari kuambatana nami baada ya Bunge hili la Bajeti kwenda kuwasikiliza vijana wanaonufaika na mradi huu juu ya changamoto na sintofahamu zao kuweza kuzitatua? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia jambo hili kwa ukaribu kabisa. Nimhakikishie tu kwamba tuko katika hatua za mwisho za maandalizi za ugawaji wa hivi

vifaa, hususan maboti kwa wavuvi wa Kanda ya Ziwa Victoria. Uzinduzi huu tutafanyia huko huko ukanda wa Ziwa Viktoria. Kwa hiyo, tuko katika hatua za mwisho na ninaamini ndani ya muda mfupi Wizara ya Mifugo na Uvuvi itataja hiyo tarehe rasmi ya lini sasa tunatoa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuambatana na Mheshimiwa Mbunge, mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri tuko tayari muda wowote mara baada ya Bunge lako kuahirishwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 717

**Mkakati wa Serikali kuimarisha sekta ya mifugo nchini**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, Mwaka 2021 – Januari, 2022 Sekta ya Mifugo imeuza nyama nje ya nchi kwa asilimia ngapi na upi mkakati wa kuimarisha Sekta hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya tani 10,415 za nyama zimeuzwa nje ya nchi zenye thamani ya dola za Kimarekani 42,500,994.90 ikilinganishwa na tani 1,774.29 za nyama zenye thamani ya dola za Kimarekani 4,290,000 zilizouzwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 492.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuimarisha tasnia ya nyama ikiwemo; kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa machinjio za kisasa zinazokidhi viwango vya kimataifa ambapo hadi sasa, zipo machinjio sita tu zenye ithibati ya kuuza nyama nje ya nchi; kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara katika tasnia ya nyama kwa kupunguza tozo na kodi za usafirishaji wa nyama nje ya nchi; kuwajengea uwezo vijana waliohitimu vyuo vya mifugo kupitia vituo atamizi ili waweze kufuga kisasa na kuzalisha malighafi ya kutosha kwa ajili ya viwanda vya kuchakata nyama na kuboresha mbari za mifugo kupitia uhimilishaji, ugawaji wa madume bora na usambazaji wa mitamba ya ng'ombe wa nyama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na eneo hili, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mkakati wa Serikali umejikita kwenye wafugaji wapya wanatoka vyuoni. Ni nini mpango wa kuwawezesha wafugaji hawa wa sasa ambao wengi wanafuga kienyeji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; upande wa nyama ya kuku kumekuwa na tatizo la vifaranga mara nyingi. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha vifaranga vinapatikana ndani vyenye ubora ambao nyama yake inaweza pia kuuzwa nje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia tasnia hii ya nyama nchini kwa umakini mkubwa. Nimwondoe shaka tu kabisa kwamba mipango ya Serikali siyo

kwa vijana wanaotoka vyuoni, ama vijana wa kisasa pekee, ni pamoja na wale ambao wamezoea kufuga kwa mifumo ya kiasili. Kwa hiyo, mipango yetu inajumuisha makundi yote mawili na tunaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunaboresha mbari za mifugo kwa wafugaji wote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa vifaranga, ndiyo moja ya mikakati ambayo sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunayo sasa hivi kuhakikisha tunaongeza uzalishaji ili vifaranga vipatikane kwa wingi na tuwasaidie wafugaji wetu, hususan wa kuku, na mifugo mingine, ili tuweze kuuza nje ya nchi kwa wingi mkubwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Tarime, Jimbo la Tarime Vijijini lina kata 26 na vijiji 88, vijiji vyote…

**SPIKA:** Muda wetu umekwenda sana, nenda moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niulize Wizara, kwa nini katika jimbo zima hakuna josho la kuogeshea wanyama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mikakati ambayo tunayo katika mwaka wa fedha unaokuja, 2023/2024, Halmashauri ya Tarime ni miongoni mwa halmashauri ambazo zitapata majosho katika yale majosho ambayo tuliyatangaza katika fedha ambazo tuliziweka katika mpango, shilingi bilioni 5.7.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake. Mbunge kutoka Dodoma.

Haya, basi tunaishia hapo, ndiyo lilikuwa swali letu la mwisho hilo.

Mheshimiwa Kanyasu, nimeshataja Dodoma, sasa wewe unatoka Geita.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo ukimaliza.

**SPIKA:** Wewe unaomba Mwongozo?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete matangazo niliyo nayo hapa mbele halafu tutaendelea na utaratibu wetu.

Mheshimiwa Mtaturu, naona na wewe unataka kusimama tena, tumalize matangazo kwanza. Tutaanza na tangazo la wageni; kwanza ni wageni wangu ambao wako Jukwaa la Spika, halafu tutaendelea na wageni wangu wengine.

Tunaye Profesa P.L.O. Lumumba kutoka Kenya; karibu sana. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu yeye anaweza asijue maana ya hayo makofi; maana ya hayo makofi ni kwamba wamekupa heshima Profesa. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Lloyd Ward kutoka Marekani. Hapa wamesema Mwafrika mweusi kutoka Marekani wa kwanza, lakini

nafikiri nia ilikuwa ni njema. Huyu anatoka Marekani, ni Mmarekani mweusi wa kwanza kuwa Kiongozi wa *Fortune 500 Companies,* pia amekuwa mshauri wa viongozi wengi duniani, karibu sana Ndugu Llyod Ward na ahsante sana. *Thank you so much, you may be seated. (Makofi)*

Yupo pia *Dr. Rev.* Paul Enenche ambaye ni Daktari Bingwa wa Binadamu, Mwandishi wa Vitabu na kiongozi mashuhuri wa kiroho duniani mwenye jengo la kanisa kubwa kuliko yote duniani la watu laki moja kwa ibada kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Sasa huyu sijui ndiyo yupi pale? *Dr. Rev.* Paul Enenche, ama hajafika. Haya, anakaribishwa sana. *(Makofi)*

Yupo pia *Rev. Dr.* Canon Moses Matonya ambaye ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania *(CCT),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia *Rev.* Peter Konki, Mwenyekiti aliyepita wa *CPCT* Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia *Bishop* Dunstan Maboya ambaye ni *General Overseer, Calvary Assemblies of God (CAG)*. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine kutoka *Kingdom Leadership Network Tanzania (KLNT)* na hawa ni Ndugu Isaac Mpatwa ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji. *(Makofi)*

Jamani, hawa wageni wako sehemu gani, ama hawajaingia humu ndani? Maana sasa nitajikuta nasoma majina mara nyingi.

Basi kundi zima nadhani hawapo hawa, niende kwenye kundi lingine.

Wapo wasanii 20 na wajasiriamali kutoka Mbeya Mjini; karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika wageni hawa wapo kikundi kimoja kinaitwa *Waarabu Dancers,* karibuni sana. *(Makofi)*

Kipo kikundi kingine cha *dancers,* naona jina lao hawajawekwa hapa, lakini wote tutaweza kuwaona vizuri siku ya kesho vizuri, msiwe na wasiwasi, karibuni sana mnaweza kuketi.

Tunao pia walimu 55 ambao ni wanashirikisho kutoka Mkoa wa Mbeya; karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wangu wengine, nao wanatoka Marekani na mtafsiri wao, na hawa ni *Rev.* Sherry Lynin Welch, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Rhonda Cheryl Amer, karibu sana; yupo pia Cynthia Jeanne Washam, karibu sana; yupo pia Melodie Sue Joyce; karibu sana; na yupo pia Dkt. Elieshi Kisinza; karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine ambao ni Wakurugenzi wa Majimbo kutoka Idara ya Wanawake (WWK) ya Kanisa la *TAG;* Ndugu Lucy Enelia Masembo, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Elizabeth John Ngoda, karibu sana; yupo Ndugu Esther Stanley Mwanza, karibu sana; yupo Ndugu Sevelina William Luvanda, karibu sana; yupo Ndugu Mary Maula Kabora, karibu sana; yupo Ndugu Rose Gambo Tango, karibu sana; yupo pia Ndugu Rehema Jonas Ayo, karibu sana; yupo pia Ndugu Flora Justo Bisaya, karibu sana; yupo pia Ndugu Martha Seth Mnzava, karibu sana; yupo pia Ndugu Joyce Songelael Kayanda, karibu sana; na yupo pia Ndugu Jane Benjamin Makweta, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa nimewaona wageni wengine wamekaa pale lakini kwa sababu sijajua ni wapi katika hii orodha ya majina, nadhani msaidizi aende nikajue ni kina nani wale waliokaa Jukwaa la Spika ambao bado hawajatangazwa ili tumalize tangazo hilo la wageni walioko humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo tutaendelea kuwatangaza wageni wengine, lakini nadhani hawa viongozi ambao ni Wakurugenzi wa Majimbo kutoka Idara ya Wanawake,

Kanisa la *TAG*, naona kuna waliovaa sare ambao hawajakaa Jukwaa la Spika, nao wasiame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wetu Waheshimiwa Wabunge wote, na nianze kuwatangaza hao; yupo mgeni wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo, na huyu ni Mwenyekiti wa wadau wa zao la pareto Tanzania, Ndugu Anangisye Mwankina, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kutoka Mufindi, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo na hawa ni Chawa wa Mama kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Daniel Sillo kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni watoto wake kutoka Busega Mkoa wa Simiyu, wakiongozwa na mke wake, Ndugu Tupondilwe Chaula, karibuni sana. *(Makofi)*

Mke wa Mheshimiwa Simon Songe ndiyo yupi? Haya, ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Hapa nimeona makofi mengi yakiwa yanatokea Njombe, mengine yanatoka Ruvuma, mengine Iringa. Kila mtu anamwona Mheshimiwa Songe ni shemeji yake. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Ussi Pondeza ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni watoto wake kutoka Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka kutoka Kibiti, Mkoa wa Pwani, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Sylvia Sigula kutoka Jijini Dar es Salaam ambao wamesoma naye *Mount Carmel Girls Secondary School,* Mkoa wa Kigoma, wakiongozwa na Ndugu Agness Kahamba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo kutoka Chuo cha Ushirika, Moshi Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambao ni Kwaya ya Katumba Kutoka Rungwe, Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambacho ni kikundi cha maendeleo kutoka Ikungi, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wakulima na wadau wa zao la kahawa kutoka Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe, wakiongozwa na Diwani wa Nyimbili, Mheshimiwa Tinson Nzunda, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Issa Mtemvu na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambao ni viongozi wa vyama rafiki kutoka Wilaya ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Isack Kamwelwe kutoka Mpanda, Mkoa wa Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga ambao ni wakulima wa miwa kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana, nilikuwa sijui kuna kilimo cha miwa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambao ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Lushoto, Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Joseph Tadayo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari Juhudi kutoka Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitakapoletewa orodha ya wageni wengine tutaendelea kuwatangaza.

Lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba vifaa vya michezo ya *Bunge Bonanza* ambalo litafanyika kesho tarehe 24 Juni, 2023 vitagawiwa leo kupitia kwenye Kamati zenu.

Aidha, kutakuwa na kikao kifupi kuhusu utaratibu mzima wa *Bunge Bonanza* ambacho kitafanyika leo jioni katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnaomba kuhudhuria kikao hicho ambacho hakitakuwa kirefu sana, lakini ni muhimu tukutane sote pamoja hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka 12 Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Geita ilikuwa inatumika kama hospitali ya mkoa, na hivi karibuni Mkoa kwa maana ya Wizara imekamilisha ujenzi wa hospitali yake ya mkoa na ikaelekeza ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa umekuwepo utaratibu usio rasmi ambao niliwahi kuufikisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa Waziri pia ambapo waliohamia kwenye hospitali ya sasa ya Mkoa wanahama na vifaa ambavyo vilinunuliwa kuhudumia hospitali ya halmashauri ya mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, baadhi ya huduma zimesimama kutolewa, na watu wanakuwa *stranded* kwa sababu hawawezi kwenda hospitali ya mkoa, na wakienda hospitali ya halmashauri ya mji wanakuta vifaa hakuna kama *hematology machine,* mashine ya *full blood picture* pamoja na mashine ya *DM detector,* ikiwa ni pamoja na baadhi ya wataalam kuondoka kabla ya tarehe 01 ya hospitali ile kupata bajeti na kuanza kujihudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili tumelizungumza na Waziri wa Afya na Naibu Waziri wa Afya, na bado linaendelea kufanyika na kusumbua wananchi. Naomba Mwongozo wako namna bora ya *transition* ili wananchi wa Geita wasiendelee kupata matatizo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ajili ya kuomba Mwongozo wako kwa ajili ya suala ambalo lilitokea jana hapa kuhusiana na masuala ya ununuzi wa mahindi. Bado tuna taarifa zilizo sahihi kabisa kwamba bado zoezi la ununuzi wa mahindi kwenye maeneo yetu haliendelei kama ambavyo tulikuwa tumepata taarifa jana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mwongozo wako ili tupate nafasi ya kulijadili suala hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unayewatoa wageni huko juu subiri kidogo, nimeshasimama.

Amesimama Mheshimiwa Kanyasu hapa akiomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea huko, jimboni kwake, lakini Kanuni yetu ya mwongozo ya 76 inataka jambo liwe limetokea Bungeni mapema. Pamoja na umuhimu wa Jambo lenyewe lakini halihitaji kutolewa mwongozo na Spika, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri yupo hapa atakuwa amesikia hiyo hoja yako Mheshimiwa Mbunge na aende akaifanyie kazi.

Waheshimiwa, kwa sababu kama hospitali hiyo ya mji inao uwezo wa kutoa hizo huduma na vifaa vilipelekwa hapo sina hakika kwa nini vifaa vinahamishwa kupelekwa hospitali mpya ya mkoa, na kama wataalam wapo na wanaweza kutumia hapo sioni ni namna gani mnatumia hiyo busara ya kuhamisha hivyo vifaa. Kwa hiyo nadhani uonane na Mheshimiwa Mbunge hapo mlimalize hilo jambo ili hospitali hiyo iendelee kutoa huduma maadam watu wanaweza kupata huduma kutokea hapo.

Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani umemsikia Mheshimiwa Mbunge, na Mheshimiwa Mbunge umesikia, siwezi kulitolea mimi mwongozo lakini ninyi wawili muonane mlimalize hilo jambo.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, na yeye ameomba mwongozo kwa jambo ambalo lilitokea jana hapa, lakini nafikiri ni kwa sababu jana nilitoa maelezo kwamba jambo hilo Waheshimiwa Wabunge, ambao walikuwa wakizungumzia jambo la bei ya mahindi

kushuka na Wizara ikawa imeshatoa hapa mwelekeo ama majibu. Kwamba *NFRA* wameshapewa fedha kwa ajili ya kununua mahindi. Na kwa bei ambayo ilikuwa inalalamikiwa na Wabunge, maana yake kama wakulima wangeenda kuuza hayo mahindi huko *NFRA* kusingekuwa na hayo malalamiko ambayo Wabunge waliyaleta hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu niliwaambia wakawasiliane na wananchi wao na yeye amesema hapa kwa kifupi nimpe fursa ya kumsikia ni jambo gani limetokea huko halafu nifanye maamuzi, Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nishukuru kwa hatua ambazo Serikali inachukua kuhakikisha kwamba inataka kutanua *tax base* hasa kwenye mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimepiga simu Iringa na nikaulizia kwa wale watu ambao wanafanya kazi ya kuuza mahindi. Pale sisi tuna migogoro miwili, kwanza tuna *NFRA* ambao huwa wananunua mahindi pale Iringa lakini kwa sasa kuna watu wa *CPB* ambao nao wana zoezi la kununua mahindi pale kwenye Kihenge chetu. Kinachoendelea pale, hawa wakulima wanachoniambia ni kwamba *NFRA* hawajaanza kununua hayo mazao, hawa *CPB* wakulima waliwalipa fedha tangu tarehe tano Mei kwa sababu walitaka kuuziwa mahindi ambayo tayari yalishanunuliwa na hawa *CPB* ambao nafikiri ni bodi ya mazao mchanganyiko. Kwa hiyo walilipa fedha tayari ili wapewe mahindi likatoka zuio kwa Serikali kwamba hawawezi kutoa mahindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Nadhani hapo utakuwa unanichanganya mimi lakini pia unalichanganya Bunge. Hii hoja yako ya pili ina uhusiano na hoja ya kwanza?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ndiyo.

**SPIKA**: Ngoja tuelewane vizuri, ina uhusiano na *NFRA* kupewa fedha kwenda kununua halafu fedha zikawa hakuna? Maana hiyo ni taasisi nyingine uliyoitaja hapo. Unasema yenyewe imepokea fedha kutoka kwa wakulima na sio mahindi vinahusianaje?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika,ndio nataka nikupe muunganiko pale mbele nikuunganishie kwamba *NFRA* hawana fedha kwa sababu…

**SPIKA:** Ngoja, *NFRA* hawana fedha wakati huo huo hao uliowataja sijui *CPB*, umesema *CPB*?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Hao *CPB* wamepewa fedha na wakulima, unaziunganishaje hizo hoja mbili?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naziunganisha kama Serikali ingekuwa na ela kwa nini *CPB* wanang'ang'ania fedha za wakulima kununulia mazo ili wawalipe mahindi wakulima wenyewe wakati *NFRA* wananunua? Kwa hiyo *NFRA* hawapo pale kununua, na ndiyo maana hata hawa wakulima waliopo pale wanauza mahindi bado wanaidai Serikali kwa sababu *CPB* nayo ni ya Serikali na *NFRA* ni ya Serikali, kwa hiyo wakulima wanaidai Serikali fedha zao ambazo walitakiwa wapewe mahindi wakaomba warudishiwe fedha wameshindwa kurudishiwa kwa hiyo hakuna kinachoendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, subiri kidogo. Tutenganishe hoja, kwa sababu hii hoja yako ya pili sijui imepita wapi kuingia hapa ndani kikanuni. Usipoitenganisha unanipa wakati mgumu kufanya uamuzi kwa sababu hoja ya hawa *CPB* kuchukua ela kwa wakulima ili wawape mahindi ni hoja tofauti na bei ya mahindi ya wakulima. Hoja ambayo nimekupa nafasi ya kutoa ufafanuzi ni hoja ya kwanza, hoja inayohusu bei ya mahindi ya wakulima wanaouza mahindi yao na si ambao wameenda kununua mahindi *stick* hapo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba niko-*conclude* hivi, sehemu ambayo huwa wananunulia *NFRA* mahindi Iringa kwenye kihenge wako hawa *CPB* ndio wenye *issue* hiyo kwa hiyo *NFRA* hawapo na mahindi hayanunuliwi, hiyo ndio hoja yangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, ngoja tuelewane vizuri tu hakuna shida. Wakati ukieleza umesema *CPB* wamechukua fedha za wakulima na hawajawapa mahindi, nimekuelewa vizuri?

**JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa, sasa hii hoja yako unaichanganyaje? Hebu jisikilize wewe mwenyewe unavyosema, unaichanganyaje yaani?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Hebu mwenye hoja ya jana yuko wapi? Mwenye hoja yake ya jana yuko wapi?

**MHE.JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba ni-*conclude*.

**SPIKA:** Mheshimiwa, usi-*conclude* kabla sijaelewa, utakuwa una-*conclude* nini?

**MHE.JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Sawa, basi naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Hebu mwenye hoja yake ya jana yuko wapi? Mheshimiwa George Mwenisongole yuko wapi? Maana naona hii hoja ikipelekwa Iringa inakuwa na mambo mawili ambayo hayatuelekezi kwenye hoja ya jana. Hoja ya jana inahusu bei ya mahindi; sasa hapa inakuja kesi nyingine sio bei ya mahindi ni ya *CPB* wamechukua fedha za wakulima hawajawapa mahindi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba unipe muda basi nimalizie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, nimekupa nafasi umeleta hoja mbili, elezea hoja iliyokuwepo jana ukiniongezea hoja nyingine sikuelewi ni kanuni gani unaingiza hilo jambo hapa ndani.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nikuelezee hiyo hoja ya jana.

**SPIKA:** Mheshimiwa, eleza hoja ya jana kwa maelezo niliyotoa mimi. Nilisema hivi; ninyi Wabunge mnaotoka maeneo ambayo wakulima wa mahindi bei yao imeshuka, na Serikali ilitoa ufafanuzi hapa ndani kwamba *NFRA* imepewa fedha ili inunue kwa bei ambayo Mheshimiwa Waziri aliitaja hapa na Waziri aliitoa wazi, mimi nikasema mkafuatilie kwa sababu kelele ziliendelea, kwamba hizo fedha zipo huko na kama *NFRA* wananunua mahindi.

Mheshimiwa sasa wewe umenikorogea hoja hap ahata sielewi nikuelekeze kwa namna gani. Kama umenielewa jielekeze kwenye hoja hiyo.

**MHE.JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, najielekeza kwenye hoja. *NFRA* kwa Mkoa wa Iringa huwa wananunua mahindi kwenye Kihenge pale, wana kituo kingine wananunua Makambako. Kwa Mkoa wa Iringa, kwa nini niliingiza na ile ni kwa sababu pale kwenye kile kituo wapo hawa *CPB*, sasa naachana na hawa *CPB* ni kwamba sasa *NFRA* hawapo pale kununua haya mahindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, sawa, nimekuelewa. Waheshimiwa Wabunge hoja hii ingekaa vizuri sana kama mwenye hoja angekuwepo; kwa sababu maelekezo niliyoyatoa jana yalikuwa ya moja kwa moja yaani Wabunge wanao husika wakafuatilie, wakishafatilia waniletee hiyo taarifa ndiyo nifanye maamuzi hapa. Sasa mpaka sasa hivi siyapati hayo maelezo na kwa kuwa siyapati nashindwa kuitoa hoja kwenu kwamba tuendelee na mjadala. Naona mmesimama wengi hebu mtafuteni mwenye hoja aje hapa Bungeni mimi nitampa nafasi maana yeye ndiye alielewa vizuri maelezo niliyoyatoa wengine

wote mnanichanganya, ama wa Jimbo jirani umeelewa? Haya Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, kulingana na hoja ambayo mtoa hoja aliitoa jana ni kwamba Serikali haijatoa katazo lakini imetoa maelekezo ambayo yanawafanya wakulima au wafanyabiashara wapate changamoto ya kutoa mazao nje ya nchi. Changamoto hiyo ikasababisha bei za mahindi kushuka. Ukatuagiza kwamba twende kwenye vituo vyetu tukaulize kama *NFRA* wameshaanza kununua mahindi.

Mheshimiwa Spika, hali iliyopo sasa hivi ni kwamba *NFRA* mpaka sasa hivi bado hawajaanza kununua mahindi kwenye vituo. Hoja yetu iko hapa; wazo la Serikali ni jema lakini masharti waliyoyaweka yanafanya wafanyabiashara wasiweze ku-*export* mazao hayo kwa wakati, hata *NFRA* kwenye hivyo vituo vilivyopo si rafiki kumfanya mkulima aweze kuuza mazao. Hivyo basi mazingira yanakuwa magumu kwa wakulima wetu, kwa hiyo sisi tulikuwa tunaomba tutoe hoja ili Wabunge tunaotoka kwenye maeneo hayo tujadili ili tuweze kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ngoja kwanza. Mheshimiwa Condester Sichalwe, hoja ya kutolewa mahindi nje ya nchi ama kuuza nje ya nchi imekuja kama sehemu ya kupungua kwa bei ya mahindi, maana yake kama yananunuliwa humu ndani kwa bei inayofaa hiyo hoja haipo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo ya jana, na ndiyo maana nasema mwenye hoja; wewe kwa maelezo uliyotoa sasa hivi hapa nataka niulize jambo moja halafu ndio nijue cha kufanya. Kama mahindi yatanunuliwa kwa bei iliyopo na *NFRA* ile bei si ni sawa? Maana ndiyo majibu yalikyokuwepo hapa jana. Hoja ilikuwa ni kwamba *NFRA* ilikuwa haijaanza kununua mahindi kwa bei hiyo kwa sababu bei aliyotoa mtoa hoja ilikuwa shilingi mia nane sijui mia ngapi ndiyo ikaonekana bei inakuwa chini kuliko ile aliyotaja Waziri?

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kukujibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama bei hiyo ambayo Serikali wametoa bado mahindi yataendelea kushuka kwa sababu mbili zifuatazo: -

i. *NFRA* ukipeleka mahindi, wanavyo vigezo vyao vingi unaweza kupeleka tani mia tano wakachukua tani kumi. Hivyo kufanya wakulima hawa wasipate mahali pa kuuza mahindi lakini wachuuzi wa kawaida wenyewe wanachukua mahindi maadam ni mahindi na wananchi wanapata nafasi ya kununua.

**SPIKA:** Haya, nani anataka kutoa taarifa? Mheshimiwa Yahaya ngoja. Mheshimiwa Condester Sichalwe toa hoja.

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nomba kutoa hoja Wabunge wote waunge mkono. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamliwe)*
*(Hoja Iliamliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, sasa tuketi ili wasimamae wale Wabunge ambao watachangia hoja na kwa sababu muda wetu umekwenda sana nitawapa Wabunge wachache sana na kwa uwakilishi, kwa sababu nafahamu Mikoa mingi inalima mahindi. Kwa kuwa mtoa hoja anatokea Songwe, basi mmeshawakilishwa. Mchangiaji kutoka Manyara atakuwa Ole-Lekeita, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Watawawakilisha jamani kwa kuwa hoja ni hizo hizo? Haya, Mheshimiwa ole kaita, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Yahya Massare, Mheshimiwa Joseph Musukuma…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Ngoja ngoja jamani, mimi si ndiye nachagua wa kuzungumza? Si ndiyo? Haya, Mheshimiwa Selemani Kakoso na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Waheshimiwa, upande wa Wabunge tuketi halafu upande wa …

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, bado Rukwa.

**SPIKA:** Rukwa jamani si ni ukanda, Katavi akichaguliwa si atawakilisha, mnataka kila mkoa haiwezekani.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, bado Rukwa, Rukwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge teketi, tafadhari wabaki upande wa Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mara, Mara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Kanda ya Kati mmewakilishwa huku. Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, bado Rukwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mara, Mara.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Rukwa kakae karibu na Mheshimiwa wa Katavi yule pale.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Katavi na Rukwa ni tofauti.

**SPIKA:** Ukakae na Mheshimiwa wa Katavi karibu ili mshauriane vizuri.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana…

**SPIKA: N**ilifikiri unaomba kuchangia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, Hapana, kwa upande wa Serikali tunaomba kama itakupendeza na muda wa Bunge lako unaruhusu Naibu Waziri wa Viwand ana biashara pia angechangia hoja hii.

**SPIKA:** Sawa aingie kwenye wachangiaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa, sasa hapa uwiano kidogo utakuwa mgumu kwa sababu Serikali tayari nimeshaweka wawili. Kwa hiyo Wabunge wanakuwa wamepungua.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ongeza Mara.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Rukwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi, haya Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Rukwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Dodoma.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Rukwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Dodoma ndio inawalisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mbunge wa Vijana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Kanda maalum, Mara.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa. Tutaanza na Mheshimiwa Ole-Lekaita …

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Ruvuma pia…

**SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane, Mheshimiwa Ole-Lekaita atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuzungumzia habari ya suala la mahindi.

**SPIKA:** Muda wa kuchangia ni dakika tatu.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, okay, ahsante sana, Kiteto ni *hub* na ndio *bred basket* ya ukanda huu. Tangazo la Serikali la kufunga kupeleka mahindi nje tunaamini ilikuwa ni nia njema sana. Lakini kwa mfano Kiteto, mahindi kwa gunia ilishafika elfu tisini lakini baada ya zuio hilo, na nimetoka jana Kiteto imekuwa shilingi 55,000.

Mheshimiwa Spika, tunachosema, wazo la Serikali kununua mahindi hapa limepokelewa vizuri sana na wakulima. Tunachoomba Serikali inunue kwa bei ambayo wakulima walikuwa wauze huko. Tukitoa tangazo na likashusha bei itaumiza wakulima. Kwa hiyo tunachoomba ni rahisi sana, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mahindi yalishafika bei elfu tisini kama mnatoa na kwingine naambiwa imefika laki na ishrini.

Mheshimiwa Spika, kama mnataka kununua mahindi yote na fedha zipo, tengenezeni vituo na tuwe na navyo Kiteto na kila Kanda ya nchi hii na tukubaliane bei hapa na Mheshimiwa Waziri, tangaza bei hiyo, tena chukua ile ambayo ni *the highest* kama ni laki na ishirini ndio imekuwa *the highest* Serikali inunue kwa hiyo laki na ishirini. Mkifanya hivyo wakulima mtakuwa mmewatendea haki sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mvua ilikuwa kidogo, upatikanaji wa mahindi umekuwa ni mgumu sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii. Wazo la Serikali la kuwa na vituo hivi ni la muhimu na ni la msingi kwa ajili ya faida ya mkulima wa chini kabisa. Lakini vituo hivi vya *NFRA* viko vichache, na mwendo wa mkulima kutoka kata moja kwenda sehemu ambayo wameweka kituo ni mbali sana na hivyo kuongeza gharama katika ununuzi wa mazao hayo. Kwa mfano, mkulima anabeba mahindi anapeleka zaidi ya kilometa 100 kwenda kuuza; *obvious* ile bei ya shilingi mia nane itamkata mkulima. Kwa hiyo tunaomba vituo viongezeke viwasogelee sehemu ambapo wakulima wapo.

Mheshimiwa Spika, lakini mbili wale wauzaji ambao Mheshimiwa Bashe ni watendaji wako kule chini wengi sio waaminifu wanaenda kusema mahindi haya hayafai ni *reject* lakini wakati huo huo wanaenda kuuziwa wao pembeni nakuja kuuza ndani. *Of course* hili suala linahitaji utafiti wa kiintelijensia ili uweze kuhakikisha hilo suala, kwa sababu leo mkulima kabeba mahindi kilometa zake tano, sita amepeleka kwenye kituo mnunuzi anasema mahindi haya hayafai.

Hilo nililisema hata kwenye parachichi haya, lakini usiku watu wachache, wajanja, madalali wananunua na tena wanayapeleka kwenda kuyauza kesho yake. Tunaomba uangalizi wa karibu uwepo na kuhakikisha maadili yanakuwepo kwa wale wanunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, hili ni soko huria, tunaomba wananchi wapewe uhuru wa kuuza. Nimelima mahindi yangu, nahitaji kumpeleka mtoto shule, nikauze ninapotaka mimi, baadaye itatusaidia sisi kuweza kujua bei itakuwa juu na mkulima atajisikia vizuri akiuza anapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele imegonga. Mheshimiwa Yahaya Masare atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma na Mheshimiwa Selemani Kakoso, ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naunga mkono hoja hii. Uwazi na ukweli ni kwamba hadi tunavyoongea ni kwamba hadi tunavyoongea sasa *NFRA* hawajaanza kununua mazao mahali popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wilaya ya Manyoni tunalo ghala ambalo *NFRA* wananunua mahindi, hakuna hata mtu mmoja wa *NFRA* pale, lakini wakulima wa Itigi, wakulima wa Mkoa wa Dodoma, wakulima ambao wanauza katika Soko la Kimataifa la Kibaigwa, mahindi yalikuwa yamefika katika bei nzuri sana. Leo kilo moja imeshuka zaidi ya nusu ya bei iliyokuwepo kutokana na zuio.

Mheshimiwa Spika, dhamira yetu ni nini? Tuna nia ya kuwasaidia wakulima wetu, nia ya kuwasaidia pembejeo lakini bado hazijafika. Sasa wanapofanya jitihada zao wanalima na wanunuzi wanakuja kununua mazao, leo tunapoweka zuio tunawadhulumu wakulima wetu. Naomba sana Serikali ione ni namna gani ya kutengeneza matajiri kutoka kwa wakulima wa nchi hii. Tusiwafanye wakulima ni watu dhalili, wakati wakulima wanatumia nguvu zao, wakati wa kuuza Serikali inaingilia kati. Kwa nini isifanye uwezeshaji mkubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kule mipakani kwa nini visitolewe vibali hivyo? Kama ni leseni nchi hii ni moja kwa nini zisitolewe leseni mahali popote, wananchi wakaomba leseni ilimradi awe na vielelezo vile kama *TIN, Clearance* na vile ambavyo ni vigezo vya biashara? Tunaomba Serikali irahisishe ufanyaji wa biashara katika maeneo mengi hususani katika kilimo. Wakati Serikali hainunui mazao, basi wale wangeweza kununua. Sasa hivi wananchi baada ya kulima, uhitaji ndio unakuwa mkubwa, wanataka kupeleka watoto wao shule, wanataka... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana, kengele imeshagonga.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja kwa mara nyingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Msukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba sisi Wabunge tumwogope Mungu. Nakumbuka mwezi wa Februari na Machi tulipokuwa tunapiga kelele humu kulalamikia mfumuko wa bei, tulipotuma lawama ni Serikalini. Sasa, kama Serikali imeamua kuweka utaratibu ili tukipiga kelele iwe na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilinde, mimi ni mfanyabiashara na mimi na–*export* mahindi. Humu kuna wengine hawafanyi biashara hiyo. Mimi najitoa kusema, nafanya hiyo biashara. Hakuna mahali Serikali imezuia kutoa mahindi nje, mpaka leo mimi natoa, lakini nataka niwaulize Wabunge wenzangu, ni nchi gani ambayo inafanya biashara kiholela? Juzi Watanzania zaidi ya 50 waliandamana Zambia. Walikwenda kununua mahindi Zambia, yakakamatwa kwa sababu hawakufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, masharti yaliyowekwa ni kukata leseni na kufungua Kampuni. Waheshimiwa Wabunge tumwogope Mungu.

Mimi nafanya hiyo biashara na Jimbo langu linaongoza Kanda ya Ziwa kwa kulima, Wabunge wanafahamu. Watu wanatoka Uganda na mitumbwi wanakuja kukaa Ziwani wananunua, wanapakia na hela za Uganda na mataka taka bila kufuata utaratibu. Ninyi ni wasomi wa *design* gani? Tutawezaje ku–*control* hata hizo dola tunazohangaika? Serikali iweke utaratibu, watu wafuate utaratibu na hela ziwe kwenye *system* ya Serikali, ndio tutapata hata dola kutoka nje. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, tutakaribisha magaidi, wafanyabiashara watakatishaji. Nikuombe masharti ya kufungua kampuni ukianza leo sasa hivi saa ni nne, saa kumi una leseni, wanaogopa nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa kengele imegonga. Waheshimiwa Wabunge muda wa kuchangia ni dakika tatu, sasa ikiingia tena taarifa, hapo kidogo itakuwa ni mtihani.

Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi. Maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Bashe jana kwenye Bunge hili ni vitu viwili tofauti na uhalisia uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Rukwa na mikoa yote ambayo inazalisha zao la mahindi, bei ilikuwa nzuri sana katika kipindi ambacho soko lilikuwa huria. Mkoa wangu gunia la kilo 100 lilikuwa likiuzwa shilingi 90,000 mpaka shilingi 95000. Hali halisi baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, leo hii

Mkoa wa Katavi mahindi ni shilingi 50,000, shilingi 60,000. Kwa hiyo, ni anguko kubwa sana kwa wwakulima.

Mheshimiwa Spika, maelezo ambayo yanazungumzwa na wenzangu na maelezo ya Mheshimiwa Musukuma ambaye amesimama hapa, asilimia kubwa ya maelezo hayo ni wale ambao ni madalali, walanguzi ndio wanaokwenda watachangia hoja hii, lakini uhalisia kwa mwananchi mkulima ambaye anazalisha ana masikitiko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *NFRA* hawana uwezo wa kununua mahindi kwa sasa na masharti yao ni magumu mno. Hata hivyo, namba mbili, mfumo uliozungumzwa na Mheshimiwa Waziri haujafunguka mpaka sasa, ni vitu viwili tofauti vinavyozungumzwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri asisahau, alisimama kwenye Bunge hili akauthibitishia umma kwamba hakuna mkulima yeyote atakayezuiliwa kuuza mahindi mahali popote pale. Alishasahau? Ni jambo ambalo linafanywa tofauti kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazo kwa mikoa ambayo tunazalisha zao la biashara ambalo sasa hivi tumeambiwa na Serikali na wao wenyewe wakatuhamasisha, zao la mahindi ni zao la biashara na ni zao la chakula…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kazi ya Serikali ni kununua mazao. Kama hawana uwezo wa kununua, waaachie wakulima wauze mahali popote pale wanapotaka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Aeshi Hilaly ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niunge mkono hoja iliyotolewa. Hakuna mtu anayepinga mambo ya Wizara. Wizara ilitoa maelekezo kwamba wafanyabiashara watafute leseni, watafute *TIN number* ili waweze kufanya biashara zao vizuri. Elimu hiyo haijawafikia watu wengi. Kwa hiyo watu wanahangaika, wanatupigia simu kila mara, utaratibu upi ufanyike?

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa tangu Mheshimiwa Bashe akiwa *back bencher* alikuwa ni mtetezi wa wakulima. Tunamwomba ajipambanue ili wakulima waweze kuuza mazao yao maeneo mbalimbali wanakotaka. Kwa sababu mpaka sasa hivi wakulima walikuwa tayari wamepata wateja kutoka maeneo mbalimbali katika mikoa mbalimbali. Kwa mfano, sisi Kigoma tuko mpakani walikuwa wanapata wateja kutoka Tabora, Musoma, Kagera na wengine kutoka Uganda. Tunaiomba Serikali iweze kutoa tamko, wakulima waendelee kuuza mazao katika sehemu mbalimbali. Hivyo basi, tunafahamu Mheshimiwa Bashe ni mkulima na anawapenda wakulima…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba atoe mchanganuo ili wakulima waweze kunufaika kwa kuuza mazao yao nje. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Hilaly na Mheshimiwa Exaud Kigahe, ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza, naomba ni–*admit* jambo moja ambalo linaleta masikitiko. Wakulima wa mahindi wamekuwa wakipitia misukosuko mikubwa sana. Mwezi Mei na Juni huu ambao upo, mwanzoni bei ilikuwa imefika shilingi 80,000 shilingi 90,000 hadi shilingi 100,000. Ghafla tu ni kama Serikali hawakuwepo na hawakujua kama kutakuwa na jambo hili. Ghafla bei zilipokuwa

hapo ndio wana–*impose* mambo mengi yanayojitokeza, *documentation* na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa ni *tendency* kwa wakulima wa zao la mahindi yaani kila mwaka kuna jambo. Vile vile, kuna mtu mmoja anajaribu ku–*admit* kwamba ule mchakato ni rahisi na nini. Ungekuwa rahisi ungesababisha wanunuzi waje kirahisi. Hii inatokana kwa sababu hakuna *competition*. Mheshimiwa Waziri, jana amesema kwamba bei elekezi ni shilingi 800. Mahindi sio kama mafuta anayopanga bei elekezi. Bei ya mahindi inakuwa *determined* na *competition* kwa maana ya *demand* na *supply*. Kwa nini imeshuka? Ni kwa sababu *supply* ya mahindi ni kubwa na *demand* imepungua kwa sababu wanunuzi hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuache soko huru. *NFRA* najua watanunua lakini hata baadaye hawawezi wakanunua mahindi, najua sasa hivi hawanunui. Hata wakija hawana uwezo wa kununua mahindi yote. Turuhusu *competition,* wafanyabiashara wanunue. Hizi *restriction* tunakubaliana na jambo Serikali ililokuja nalo. Waahirishe mpaka mwakani ndiyo wajipange, lakini kwa mwaka huu tuache amani kwa wakulima wauze, nao wanataka wainue uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe tu, Mheshimiwa Bashe, aahirishe jambo hilo. Kwa sasa, hizo *restrictions* kama tutaendelea kwa namna tunavyoenda hivi, tunakwenda kumuumiza mkulima wa mahindi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Aeshi Hilaly, atafuatiwa na Mheshimiwa Exaud Kigahe na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, naomba ku–*declare interest* kwamba na mimi ni mkulima, lakini ni mfanyabiashara.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mariam naomba basi tuheshimiane.

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Spika, naungana na hoja za Wabunge waliokuwa wanaomba Serikali kwamba, hili jambo sasa hivi liahirishwe na haya masharti mengine yawekwe wakati wa msimu ujao. Nasema hivyo kwa sababu moja tu, haya masharti ambayo yamewekwa sasa hivi, yangewekwa kabla, nafikiri wakulima na wafanyabiashara wangejiandaa, lakini yamekuja katikati ya msimu, wafanyabiashara wameshaanza kununua mazao na wengine wamesafirisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Waziri, ni rafiki yangu lakini tulikaa naye hapa, ni muumini wa kutofunga mipaka. Juzi Mheshimiwa Waziri aliruhusu magari yaliyozuiliwa mipakani yaende Kenya na mengine yaende Rwanda. Pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Waziri ya kuruhusu, lakini imetokea wale wote waliokuwa na magari wamepigwa faini ya shilingi milioni moja moja kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, sasa inawezekana Mheshimiwa Waziri aliruhusu bila kuwapa maelekezo. Hata hivyo, Wakuu wa Mikoa wameamrisha magari yote walipe faini ya shilingi milioni moja moja bila kosa, laiti wangelijua wangelijiandaa mapema.

Mheshimiwa Spika, sio kazi ya mkulima kuhakikisha kwamba mwananchi wa Tanzania hafi na njaa. Ni kazi ya Serikali kuhakikisha kwamba mwananchi anapata chakula, lakini vile vile anapata huduma nyingine. Hatujawahi kuona Serikali ikimsaidia mkulima kwa asilimia 100. Hata hivyo, mkulima huyu anajitahidi mwenyewe anafanya kazi mwenyewe, analima mwenyewe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aeshi, kengele imeshagonga, ahsante sana.

Mheshimiwa Exaud Kigahe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Mohammed Bashe, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza, tuweke wazi kwamba Serikali hatujazuia na hatujafunga wafanyabiashara kuuza mazao nje hasa zao hili la mahindi.

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ambayo Serikali tunakuja nayo ni kuona namna gani tunarasimisha biashara zote kwenye sekta zote ikiwemo hii ambayo imekuwa na changamoto kubwa sana, sekta ya kilimo, kwa maana ya zao hili la mahindi.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, mwaka jana kama ambavyo wachangiaji wamesema kulikuwa na changamoto kubwa sana ya bei ya mazao mbalimbali ikiwemo mazao ya chakula kupanda bei na kukithiri vile ambavyo tumezoea. Sababu mojawapo ilikuwa ni hii ya kutokuratibu vizuri biashara ya mazao ya kilimo na hasa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tunataka tuhakikishe kwamba tunarasimisha biashara zote ikiwemo ya kuuza mazao ya chakula ili wafanyabiashara waweze kuwa na bei nzuri ya kununua kwa wakulima. Kwa sababu kumekuwa na taratibu za walanguzi na hasa wengine kutoka nje ya nchi kwenda kununua kwa wakulima kule chini kwa bei ya chini ambayo haina maslahi wala tija kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, pili, tunataka tuone kwa uratibu huu maana yake na yule mkulima wa chini anakwenda kuuza kwa vipimo na si kwa zile njia ambazo tulizoea za lumbesa, ndonya, ndoo na kadhalika. Hii imeenda kumuumiza mkulima kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, la tatu, tunataka tu–*formalize* kwamba, sasa hawa wanaofanya biashara wawe na leseni na sasa hivi tumerahisisha kupitia kituo cha pamoja kutoa leseni ambazo

zinawasaidia wafanyabiashara kufuata taratibu zote ili pia waweze kuchangia pato la Taifa katika kulipa kodi, lakini pia kumwezesha mkulima aweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, nne, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tunadhani sasa ili kusaidia wakati huu kabla ya taratibu kukamilika, *NFRA* nao waendelee kununua kwa bei ambayo tunadhani itakuwa haimuumizi mkulima, lakini pia ni faida kwa mfanyabiashara ambaye atakuwa amefuata taratibu zote ili aweze kuuza kokote atakakoweza kuuza. Vile vile, hata mkulima mwenyewe, kuna wakulima ambao wana mazao ya kutosha wanaweza kuuza hata nje kama watafuata utaratibu huu ambao tumesema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe na Mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii ili niweze kuchangia. Nitanukuu maneno ya Waziri wa Sekta. Ukifuatilia mjadala niliona kuna maeneo hivi ambayo yalikuwa yanaleta *confusion* kidogo. Kwa hiyo, naomba nisisitize ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kisekta alisema, Serikali haijafunga mipaka.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukiongelea kufunga mipaka, tukiongelea *NFRA* tunaleta mkanganyiko. Serikali haijafunga mipaka na hili Waziri wa kisekta alilisisitiza sana. Serikali imetoa utaratibu wa namna ya kuvuka hiyo mipaka. Vile vile, Waziri wa Viwanda hapa amesisitiza na ameonesha jinsi ambavyo masharti yale yamepunguzwa. Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo na jana Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo, nadhani tungejikita sana kwenye kuhamasisha hawa wenzetu ambao wanauza hayo mahindi, wawahi wachukue hizo leseni na wapeleke hayo mahindi nje. Wanunue, kila mtu aende anunue, wala hatujafunga soko, wala hatujapunguza hiyo *competition*.

Mheshimiwa Spika, kila mtu aende achukue leseni, anunue na apeleke anakotaka kupeleka. Pia, tukishafanya hivyo ingekuwa ni vema sana tungekuwa tunajadili kama upatikanaji wa leseni ni mgumu, hilo ndilo lingetakiwa liwe jambo la mjadala na sio kuhusu mipaka kwa sababu mipaka iko wazi, lakini kuhusu leseni watu wachukue leseni.

Mheshimiwa Spika, niombe Waheshimiwa Wabunge tuelewane vizuri kwenye hilo. Serikali imekwenda kuwekeza na kuona kwamba *potential* ya nchi yetu iko kwenye kilimo. Nikiongea kilimo naongea kwa dhana pana ambapo kuna kilimo, mifugo na uvuvi. Kama huo ndio mwelekeo, ni vizuri sana tuendelee kuweka misingi ya kufanya urasimishaji kwenye eneo hili, vinginevyo tutawafanya watu wetu waumie, halafu hiyo nguvu yote, watu watakuwa wanajiingilia tu kama matunda ya mti wa barabarani, kila mtu anachuma na kuondoka ambacho sio kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *NFRA* hiyo tumeongezea ushindani tu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde thelathini, malizia Mheshimiwa Waziri kengele imeshagonga.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, tuimeongezea fedha *NFRA* ili na yeye aweze kununua. Ndio maana mwaka 2022 ilikuwa Sh.100,000 tu sasa hivi tumeenda Sh.400,000 na fedha hiyo imekwishapatikana. Kwa maana hiyo itakwenda kuongeza bei kwa mkulima na kuweka uhakika.

Mheshimiwa Spika, nadhani tuwaelimishe watu wetu, wawahi wakate hivyo vibali na waweze kuuza mazao wanakotaka kuuza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe na Mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu, nataka tu niwahakikishie, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiwezi ku-*institute* sera wala utaratibu unaokwenda kummaliza mkulima. Hili ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, je, Serikali imezuia kuuza mazao nje? Jibu, Serikali haijazuia kuuza mazao nje. Pili, kuna hoja imesemwa na hata dakika tatu zikiisha naomba uniongezee nataka niongee pole pole kwa heshima, kwa unyenyekevu ili wanielewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kutoa *export permit* unafanya kazi ama haufanyi kazi? Jibu, mfumo unafanya kazi. Jana peke yake tumetoa *export permit* zenye jumla ya tani 3,640 kwa siku moja. Toka tarehe Mosi mpaka siku ya tarehe 22 tumetoa *export permit* zenye jumla ya tani 32,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mnielewe, kwa nini tumeweka utaratibu? Wiki iliyopita Wizara ya Kilimo tumepokea *notice* kutoka Mamlaka ya Afya na Chakula ya nchi ya jirani ikitu-*notify* kwamba mahindi yetu yaliyoingia kwao *moisture content* ni *18 percent.* Mnataka tuue soko hili? Yaani nataka nijiulize hili swali, ni lini tunataka kuruhusu tuanze kufungua *border* tupeleke nje ikitokea *condemnation* moja tu inaua biashara yetu yote, na ni akina nani wanaopeleka? Siyo wafanyabiashara wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aeshi yuko pale huwa ananunua mahindi Zambia, muulizeni lini kaenda kununua mahindi kama yeye? Lazima apitie kampuni ya Wazambia. *Why do you want foreigners to come and go to our farms*? Mnataka kuua *small business?* Yaani mtu atoke nje aingie kwenye mashamba ya nchi hii, aondoke na lori lake nimpe phyto*sanitary*? sitampa phyto*sanitary*, *foreigner* yeyote anayetaka kununua mazao ya Watanzania aingie asajili kampuni, aingie mikataba na makampuni ya Watanzania, hilo la tatu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho. Ni hivi siwezi kuwa Waziri wa Kilimo ambae anataka mkulima akose soko la mazao ya chakula, tutayauza mazao ya chakula kwa utaratibu maalum. *NFRA* imefungua vituo, leo Magazeti yametangaza vituo 44 katika Mikoa minane na tumetangaza bei ya kununulia kati ya shilingi 600 mpaka 1,000 kutokana na kituo. Kuna hoja kwamba masharti ya *NFRA* siyo marafiki. Ni hivi, huko nyuma Serikali haikuwa na miundombinu ya kukaushia mazao. Tumeshafungua maghala manane na Mbunge wa Sumbawanga Mjini yule pale shahidi, katika kituo cha kwanza tulichoanza kununu mahindi nchi hii ni Sumbawanga Mjini. Tumenunua mahindi mpaka yana *moisture* ya 15 tunayaingiza kwenye mashine tunayakausha, ile asilimia tatu inayopotea tunaiongeza kwenye *cost of our production,* hatuendi kuchambua.

Mheshimiwa Spika, tumewaagiza *NFRA* mkulima akifikisha mahindi kwa kuwa tunajua wakulima wetu wanapovuna huwa wanapiga kwa fimbo yanakuwa yana uchafu, *ten to 15 percent* ya hayo mahindi yanakuwa yana uchafu. Tumewaagiza *NFRA* chukueni mahindi kwa wakulima, kwa kuwa Sumbawanga Mjini, kwa kuwa Manyara, kwa kuwa Katavi, haya maghala na vihenge vimekamilika, tutayapeleka hayo maeneo hayo, tutayakausha yatakuwa na *moisture* inayotakiwa, tutayasafisha *ten percent wastage* tunayoipata tunaiingiza kwenye gharama yetu ya ununuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na ninataka nitumie nafasi hii kuwatangazia wakulima, usiuze mahindi yako kama uko Mkoa wa Katavi chini ya shilingi 800, usiuze mahindi yako kama uko Kiteto chini ya shilingi 800, usiuze mahindi yako kama uko Sumbawanga chini ya shilingi 800 na Serikali inachukua hatua hii ya kutoa bei elekezi ili *competitors* wote wanapotaka kuyanunua mahindi wayanunue juu ya bei ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya *CPB.*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa malizia dakika moja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama kuna changamoto tutazirekebisha, kama kuna changamoto lakini tukubaliane asisafiri mtu yeyote kutoka Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine kama hana leseni ya biashara. Hii dhana ya kuwafanya wafanyabiashara na Watanzania walioko kwenye sekta ya kilimo kulitumia neno "wanyonge" neno wanyonge lisitumike kuhalalisha mambo ya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, tutarekebisha kama kuna changamoto kama kuna *difficulties* za mfumo tuliouweka tutaupitia lakini hatujafunga mipaka, hatutafunga mipaka, lakini hatutaruhusu mtu yoyote kutoka nje kuingia shambani anunue kupitia Watanzania, asajili kampuni na yoyote anayetaka ku-*trade* a-*trade* kwa mujibu wa sheria za nchi hii na walioingia mikataba na *CPB* Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini…

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, waliolipa fedha kwa *CPB* wana mikataba, na mikataba imeonesha kwamba wametoa benki, wale wamekuwa wajanja, walisaini mikataba ya bei ya juu walivyoona mavuno yameanza wanataka kurudi ku-*renegotiate,* wameshasaini mkataba fedha hazitarudishwa, watayachukua mahindi kwa bei ya shilingi 900 waliyosainia mikataba na tumeshawapa *CPB export permit* wawape hivyo vibali vya kupeleka nje, lakini watapeleka nje kwa bei ya mikataba tofauti na hapo hatutaruhusu. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu nimekuona naomba uketi.

Mheshimiwa Waziri hii hoja yako ya pili kwa sababu sikumpa fursa Mheshimiwa Mbunge ya kujieleza hoja yake ikaeleweka kwa sababu hii nyingine ilikuwa ya jana, sasa wewe umetoa maelezo unayoyajua kuhusu hiyo *CPB* wakati yeye hapa ndani kwenye rekodi yake haitaonekana alikuwa amesema nini, kwa sababu

nilikuwa namuuliza maswali maana hoja yake ilikuwa haihusiani na hoja ya jana.

Sasa Mheshimiwa Jesca kwa kuwa hapo ulisimama nadhani ulitaka kutoa maelezo ya ziada. Hoja yako kwa sababu haijakaa vizuri kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge na Mheshimiwa Waziri hapa yeye amepata muda wa kuelezea hiyo hoja, ambayo wewe hukupata muda, kwa sasa hivi hizo sehemu ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri na ile sehemu ambayo umetoa wewe sawa, tunaziacha tumalize kwanza hoja iliyoko mezani. Nadhani nimeeleweka Waheshimiwa Wabunge. Maana sasa itaonekana anatoa ufafanuzi huo kwenye hoja ipi, maana Mheshimiwa Mbunge hakupata nafasi ya kufafanua hoja yake mpaka mwisho.

Mtoa hoja hitimisha hoja yako.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa nafasi, nimesikiliza maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa na kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tuseme tuko hapa siyo kwa lengo la kupinga maoni ambayo Serikali imetoa na mpango wote ambao wameutoa. Waraka ambao Mheshimiwa Waziri aliutoa tarehe 23 Mei, 2023 kuelezea namna na mchakato ambavyo tunapaswa kutoa mazao nje ya nchi, mimi niseme unaonekana una tija kwa Serikali, una tija kwa wananchi wetu, lakini changamoto iko hapa tu, ametoa jambo hili ghafla sana, jambo hili amelitoa siyo rafiki kwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Waraka wake ukisoma kwenye *para* ya kwanza *roman number three* amesema hivi “wafanyabiashara na wanunuzi hao wanatakiwa kuwa na nyaraka zote muhimu ikiwemo na utambulisho wa mlipa kodi - *TIN, certificate of clearance,* leseni ya biashara ambayo ni *export license,* namba za *NIDA* na wamiliki wa makampuni.

Mheshimiwa Spika, kwenye *TASAF* peke yake tukiwa hapa ndani watu wanakosa *TASAF* kwa ajili ya kukosa namba za *NIDA*.

lwe leo, yaani leo ndani ya mwezi mmoja mtu ataweza kupata namba za *NIDA* ili aweze kufanya hilo jambo, siyo uhalisia. Jambo ambalo Mheshimiwa Waziri amelileta ni rafiki lakini haliendani na mazingira.

Mheshimiwa Spika, biashara ya mazao ni biashara ya msimu, sasa hivi tunavyoongea Zambia imefunga mipaka yake kupeleka mazao ya chakula nchini DRC. Tafsiri yake sisi huku kwetu ni *opportunity.* Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri ame-*raise* haya mambo mapema hivi safari hii hatuwezi ku-*meet* hiyo *demand* ya soko la Congo.

Mheshimiwa Spika, ombi letu kwa Serikali tunaomba mambo haya yaanzishwe mwakani mwezi wa kwanza au kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari jambo hili liendelee awe rafiki yeye kupitia Wizara yake aseme mambo yote haya kila kinachotakiwa mwananchi huyu au Mtanzania huyu anaweza akayapata ndani ya wiki moja ili aweze kuendana na hiyo *demand* ya wakati huo, yaani yeye Mheshimiwa Waziri awe kiungo kwenye hizo Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba Mheshimiwa Waziri apelekewe hii *document* kwenye *para* la pili *roman six* ambapo anaongelea lazima upate *export permit* pamoja na *phytosanitary certificates*. Wameweka *link* hapa ya Wizara ya Kilimo ambayo unapaswa ku-*apply* kupitia mfumo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimesoma *IT degree* yangu ya kwanza, ona vile *system* inavyoonyesha inaonyesha *system* iko *under maintenance,* sasa huyu mwananchi ata-*apply* kitu gani? Naomba mhudumu aje achukue ampelekee Mheshimiwa Waziri hili jambo labda yeye atufafanulie *system* yake inavyosema hivi inamaanisha nini? Inasemaje yaani huyu mwananchi wa kutoka Momba, kutoka kule Kalambo anapata nini hapa, hizo ndiyo *permit* ambazo tunaziongelea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya sekunde 30 maliazia kengele imeshagonga.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni njema lakini ndani ya muda mfupi wameweka masharti lukuki ambayo hata hao wafanyabiashara wetu au Watanzania wetu ambao tunawazuia wafanyabiashara kutoka nje bado hayawa-*favor*. Kwa hiyo, tukuombe Bunge litoe Azimio ili Mheshimiwa Waziri alegeze masharti kwa lengo la kuwasaidia wakulima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mtoa hoja amehitimisha hoja yake na kwa kanuni zetu zilivyo, Maazimio ya Bunge yalipaswa kutoka kwa mtoa hoja na yeye amehitimisha hoja yake kwa maombi kadhaa kwa Serikali. Kwa hiyo, basi Serikali imeyapokea kwa hiyo, hakuna cha kuwahoji Wabunge kuhusu Azimio lolote ambalo limeletwa hapa kwa sababu maazimio yanatoka kwa mtoa hoja.

Sawa, sasa pamoja na hayo Waheshimiwa Wabunge ametoa maelezo marefu sana Mheshimiwa Waziri, nadhani sote tumemsikia na sisi pia tukumbuke huko nyuma changamoto ambazo tumeshazipitia mara kadhaa na ambapo Serikali inakuja kuna mengine ambayo tuliiagiza Serikali ikabidi ichukue hatua na kuna mengine ambayo tuliishauri Serikali ikabidi ichukue hatua kwa ajili ya wakulima hawa ambao leo tunasema mipaka ifunguliwe na Serikali imesema haijawahi kufunga hapo.

Waheshimiwa Wabunge, nilitaka niwakumbushe mambo machache; Kwanza, mwaka 2021 Bunge hili lilijadili hoja ambayo haifanani na sasa lakini ni hoja ya mahindi. Serikali ikalazimika kutoa bilioni 50 kwenda kununua mahindi ya wakulima, maana yake ni nini? Hili jambo lina sura mbili, upande wa kwanza lazima Wabunge Serikali inapoweka haya mambo ama inapoweka utaratibu ni jambo jema kabisa kwa sababu hata sisi tukiishauri kuhusu mambo fulani huwa inafanya. Kama Serikali inaweza kutoa bilioni 50 kwenda kununua mahindi kwa sababu wakulima wanayo mahindi na hawana cha kufanya nayo, Serikali inakuwa imefanya vizuri kwenye eneo hilo.

Kwa hiyo, si kwamba Serikali inaamka tu asubuhi halafu wanasema leo haiwezekaniki Hapana! Nasi tutakuwa hatuna

uhalisia lazima tukumbushane mambo haya. Kwa upande mwingine wa hizi hizi natumia mfano huu wa bilioni 50 zilizotolewa, Mheshimiwa Waziri lazima kufikia sasa, sitaki kuamini kwamba Serikali haifahamu uzalishaji wa mahindi kwa mwaka huu nchini uko kiasi gani? Yale mahindi ambayo *NFRA* pamoja na pesa kiasi ulichotaja jana kwamba mmeipa, kama haina uwezo wa kununua mahindi yote kipindi hiki ambacho bei ni nzuri ya mahindi, *NFRA* inunue hayo mahindi kiasi wanachohitaji, halafu hayo mengine waachwe hao wakulima siyo kwamba wamezuiwa lakini waachwe kwa maana ya kwamba warahisishe zoezi la wakulima kuuza mahindi yao ili tusirudi kule kwenye kutoa tena, tusirudi kule kwenye hoja kurudi hapa ndani halafu tukaanza kuiomba tena Serikali kwamba Serikali mlitoa hizo bilioni 350 hamjaweza kununua mahindi yote wakulima wamebaki na mahindi na msimu mwingine unaingia. Nafikiri Serikali kwenye hilo eneo taarifa hizo ninyi mnazo, *NFRA* vituo vilivyofunguliwa muhimu vipewe kipaumbele.

Waheshimiwa Wabunge na mimi nadhani humu ndani mnakumbuka ninyi wote hakuna aliyesahau, humu ndani mko Wabunge ambao mlipata changamoto kwenye maeneo yenu ya bei za mahindi, bei za nafaka na Serikali ikatoa chakula kupeleka kwenye hayo maeneo ili chakula kiuzwe bei rahisi. Kama hivyo ndivyo, lazima tuipe fursa pia Serikali kuwa na chakula ambacho kitawapelekea hao wananchi kwenye Majimbo wakati wanapohitaji bei zishuke. Tusipoweka huo utaratibu tutakapokuwa tunasema Serikali bei kwenye Jimbo langu imepanda sijui tutakuwa tunataka Serikali itoe wapi hicho chakula.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo na sisi tuwe na pande zote mbili siyo upande mmoja, tunaposema Serikali ipeleke chakula lazima Serikali iwe na chakula mahali ili ipeleke wananchi bei iweze kuwa inaweza kununulika. Kwa hiyo, hayo yote ni ya muhimu lakini la msingi kwamba wakulima wasaidiwe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, bei ulizozitaja mahindi yakauzwe kwa wale ambao wanataka kuuza sasa, lakini mkishajiridhisha kwamba *NFRA* pesa yake inaweza kununua hayo mahindi na imeshanunua basi hilo zoezi lisichukue muda mrefu sana ili kutoa

fursa kwa wakulima kutokubaki na yale mahindi halafu tukarudi tena hapa ndani kuitaka Serikali itoe pesa kwenda kuongeza mahindi.

Mheshimiwa Waziri umeeleza hapo jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge lazima tukumbushane, ni kwamba pia Serikali imetoa mbolea ya ruzuku mwaka jana. Pamoja na changamoto lakini Serikali imetoa mbolea ya ruzuku. Kwa hiyo, si kwamba kwa kutoa mbolea ya ruzuku ndiyo maana inaweka haya masharti Hapana! Tuwe tunaenda mbele na kurudi nyuma. Zile pesa ambazo wamelipa kwenye ruzuku lazima ni kodi imekusanywa, kwa hivyo lazima na sisi tuwe tukitazama mambo haya kwa mapana hayo tusitazame tu upande mmoja hapana. Kwa sababu zoezi hili linaendelea, Serikali lazima ikusanye pesa kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata mbolea ya bei ile ambayo wanaimudu kwenye kilimo, kwa hivyo lazima na sisi tuwe sehemu ya hilo jambo.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo amelisema hapa Mheshimiwa Waziri na naomba nilisisitize ni kwamba kwa sasa Wabunge wamesema kuna mahindi ambayo huwa yanakataliwa na *NFRA,* wakati huohuo wale wanunuzi wengine huwa hawana hayo masharti. Nadhani ni kujaribu kuangalia upande wenu Serikali ni mahindi gani yanakataliwa kama wale wengine wanaweza kuyanunua ni dhahiri hata *NFRA* inaweza kuyanunua, labda ni utunzaji ndiyo muweke mazingira mazuri ambayo yale ambayo huwa yanakataliwa yanunuliwe kwa sababu huyu mkulima kama akimuuzia mwingine ananunulika basi yanunuliwe pia na *NFRA*.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine hili ni la jumla kabisa Mheshimiwa Waziri, mapinduzi ya kilimo ambayo tuliyasikia kwenye bajeti yako na pia tumemsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha akituletea ile Bajeti Kuu ya Serikali. Mapinduzi makubwa yanayofanywa kwenye eneo la kilimo yanaashiria kwamba tutakuwa na mazao mengi sana ya kilimo. Kama hivyo ndivyo, ni muhimu haya masoko tusiyaweke kwa namna ambayo yataanza kutafuta mazao sehemu nyingine kwa sababu hapa kwetu mazao hayanunuliki. Kwa hiyo, tuendelee na hayo kuyawaza kwa

mapana kwa sababu hicho kilimo ndiyo kimeanza katika mwaka huu wa fedha tusijejikuta huko mbele tuna mazao halafu watu wameshaelekeza macho yao sehemu nyingine. Hayo yote lazima tuyatazame kwa pamoja Waheshimiwa Wabunge lakini pia upande wa Serikali ili wale wakulima wanaohimizwa kulima kwa kisasa, wasije wakajikuta wamevuna vingi halafu hawana mahali pa kupeleka.

Waheshimiwa Wabunge, wale wageni waliokuwa wametangazwa ambao hawakuwepo sasa nimeletewa taarifa kwamba wapo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, yupo Dkt. *Reverend* Paul Eneche ambaye huyu ni Daktari Bingwa wa Binadamu, Mwandishi wa Vitabu na Kiongozi mashuhuri wa kiroho duniani mwenye jengo la Kanisa kubwa kuliko yote duniani la watu 100,000 kwa ibada ya wakati mmoja, haya karibu sana. *(Makofi)*

Hapa kwenye karatasi yangu haijasema huyu Kanisa lake liko wapi, lakini tunatambua mchango wake huo. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wengine ambao sikuwasoma kwa sababu nilipoanza kusoma wengi walionekana hawapo, yupo Profesa Jerry Mgwamba ambaye ni Kiongozi wa msafara wa *KLNT* na ni Mkuu wa Chuo cha *UIBC* karibu sana. *(Makofi)*

Nimeambiwa pia yupo Ndugu Gloria Shoo, karibu sana; yupo pia Ndugu Gladness Msemo, karibu sana; yupo pia Ndugu Joram Nkumbi, karibu sana; yupo pia Ndugu Godfrey Simbeye, karibu sana; na yupo pia Ndugu Emmanuel Shoo, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni ambao walikuwa hawajatangazwa wakati ule.

Sasa ataingia Mwenyekiti hapa muda siyo mrefu, lakini pamoja na muda wetu kwenda, nalazimika kuimaliza hoja ya Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kwa sababu Waziri

ameitolea maelezo hapo. Tutatumia muda mfupi hapo halafu Mheshimiwa Mwenyekiti ataingia.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya hapo niseme kwa ujumla kwa sababu ya mabadiliko ya ratiba yetu ya kuhitimisha Bunge, tarehe ya kupiga kura imebadilika, kwa hiyo, imerudi nyuma kwa sababu sikukuu imetokea hapo katikati na inatuletea changamoto kidogo kwenye hoja yetu hii ya bajeti. Kwa hiyo, wale Wabunge ambao walikuwa wamekusudia kuchangia Jumatatu wamerejeshwa leo. Huwa tunasemasema sana, lakini nadhani athari zitatokea leo.

Wabunge watakaochangia leo hawatapata muda kama Wabunge waliochangia hizo siku za mwanzo. Wabunge wanaochangia leo, watachangia dakika tano kila Mbunge, halafu jioni wataanza upande wa Serikali nao kupata muda wa kuchangia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha pekee ndio atakayeweza kuhitimisha hoja yake Jumatatu, na akishamiliza kuhitimisha tutaanza kupiga kura ili tuweze kuitendea haki Sheria yetu ya Fedha kwa mwaka huu.

Baada ya kusema hayo, nisikilize hoja ya Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ili Mheshimiwa Waziri aiweke sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nasikitika sana, Mheshimiwa Waziri ni kiongozi wetu…

**SPIKA:** Sasa ngoja nikuongoze vizuri ili twende sawa. Wewe wasilisha hoja yako kama vile hujamsikia Waziri ili sasa Waziri ndiyo aje akujibu, kwa sababu ukifanya hivyo, maana yake ni kama vile ameshaelewa hoja yako na hoja yako ilikuwa haiko Mezani. Sasa nimekupa nafasi, dakika mbili wasilisha hoja yako.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuongea hili jambo hapa nilimfuata Waziri nikamweleza hali halisi ilivyo kwa wakulima na wale wafanyabiashara wa mazao waliolipa fedha zao *CPB*. Nilimwambia kwamba, kuna wakulima wangu ambao mlitakiwa kuwauzia mahindi lakini inaonekana wewe Waziri umetoa kibali cha kuuzia *CPB* kuuza mahindi, kwa hiyo, wale wakulima wanaomba warudishiwe fedha zao, kwa sababu ni tangu Mei wakati mahindi kilo moja ikiwa shilingi 900. Waziri alinijibu hivi, "kweli nilizuia wasipewe mahindi kwa sababu mimi sikuwaagiza *CPB* wauze mahindi niliwaagiza wasage unga wa sembe." Kwa hiyo, sababu ya kuwazuia wasiwape wale mahindi ni hiyo, kwamba *CPB* walikiuka maagizo ya Waziri. Ninamshangaa anaposema wameingia mikataba hapa, wamefanya utapeli. Haya ni majibu ambayo Waziri alinijibu mimi. Sasa wakati ule *CPB* walikuwa wanauza mahindi wakiuzia wafanyabiashara na hawa ni wafanyabiashara walionunua mahindi *CPB*. Kwa hiyo, walishindwa kuwapa baada ya Waziri kuwazuia kwa sababu yeye anasema hawakufuata maagizo yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wale wananchi kuna mama mmoja amekopa fedha benki karibu Shilingi milioni 600 akapeleka *CPB* apewe mahindi, na anaanza kulipa. Wameshindwa kupewa mahindi kwa bei ya Shilingi 900/= ambayo walikubaliana wakati ule Mei, kabla bei hazijashuka. Wakaomba, basi kwamba kwa sababu hamjatupa mahindi yetu kwa wakati, turudishieni fedha ili nasi tukanunue mahindi kwa bei ya chini. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kesi wananchi, wasagaji wa Iringa, hata Mkuu wa Mkoa wa Iringa tumewasiliana juu ya hili jambo. Ni hivi, *CPB* tuliwaruhusu wachukue mahindi *NFRA* wakati bei ya mahindi na chakula imepanda ili wao wasage, wauze unga kwa bei ya shilingi 1,000. Hii ni kesi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kesi ya pili, tuliowakatalia wasiyaingize kwenda kuya- *trade* ni mahindi yaliyotoka *NFRA*. Hayo tumewazuia na hatutawaruhusu kwa sababu tumewapa kwa bei

ya ruzuku, wasage, wauze kwa bei ya chini ya unga kuliko bei iliyoko sokoni. Kwa wale waliofanyanao mikataba ya kuwauzia mahindi *CPB* tumewaruhusu wawape mahindi kutokana na mikataba yao. Tofauti na hapo, hatutakubali.

Mheshimiwa Spika, *National Food Reserve Agency* imempa *CPB* mahindi ya bei ya ruzuku kwa sababu ya kusaga unga ili auze unga kwa bei ya chini tofauti na bei inayouzwa mitaani, halafu tukiyaruhusu hayo mahindi tuliyowapa kwa shilingi 700 waya-*trade* kama mahindi kwa *traders* wengine, tutakuwa hatuitendei haki *National Food Reserve Agency*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa wale wafanyabiashara walioingia nao mikataba ya kuwauzia mahindi, tumewaagiza wawape mahindi, lakini mahindi yaliyotoka *National Food Reserve Agency* yatatumika kwenye vinu vya *CPB* yatasagwa, *CPB* atauza unga. Mahindi ya *trading,* wao watatakiwa kuwapa mahindi kama walivyosaininao mikataba.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo msimamo wa Wizara.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Nadhani hayo maelezo sasa yakaa vizuri kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kama kuna jambo lolote ambalo halijakaa sawa hapo, mtaweza pia kukaa pamoja na mlimalize.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete ambaye anaitwa Samweli Kitemba Malembera kutoka Wilaya ya Tarime, Nyamongo, karibu sana; pia ipo kwaya kutoka Hai na hii ni KKKT Usharika wa Mudio, Jimbo la Hai. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa anaingia Mwenyekiti kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu. Katibu.

**NDG. MONICA MWANGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma wajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wanasayansi wa zamani, *Hippocrates* na Thomas Edison waliwahi kusema madaktari wa karne ya 21 watatumia lishe bora katika tiba badala ya kutumia madawa ya kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua umuhimu wa lishe bora katika afya ya jamii. Niwakumbushe tu mwaka 2020 wakati wa ugonjwa wa Corona ulivyopamba moto katika nchi yetu, Watanzania mbalimbali wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa wenzetu Wabunge walitengeneza dawa asili kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa Corona na kusema kweli dawa hizo zilitusaidia kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja linanisikitisha sana ninapoona Serikali yetu inatumia kiasi kikubwa sana cha fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa hasa za chakula ambazo tunaweza tukazizalisha hapa nchini kwa ubora wa hali ya juu sana. Tunaagiza maziwa ya unga wakati Tanzania tuna ng'ombe wapatao milioni 23; tunaagiza juisi za matunda wakati Tanzania ina matunda ya kila aina yanaoyoharibika kwa kukosa

soko; tunaagiza mayai na kuku, wakati Tanzania tuna kuku wa kila aina; tunaagiza dawa ambazo tungeweza kuzitengeneza hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, jambo linalonisikitisha zaidi, watoto wa Watanzania ambao ni warithi wetu, tunawalisha vyakula ambavyo vina kiwango kikubwa sana cha sukari na protini yenye kiwango duni sana. Matokeo yake ni nini? Tunadumaza akili na miili ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kama Taifa kuingia katika karne ya 21 tukiwa na watoto ambao uwezo wao wa kufikiri ni umedumaa sana? Sasa niliwahi kusoma mahali, nikawa natafuta siri ya Waisraeli kuwa na watoto wenye kipawa cha hali ya juu sana na nikabaini kumbe hakuna siri, jambo lililo wazi ni lishe bora ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu nafikiri sasa wakati umefika sisi kama Taifa tufanye uamuzi wa kimapinduzi, tuiangalie mitaala yetu ya shule za udakitari na sayansi ile ya tiba, badala ya kusisitiza kwenye matumizi ya madawa yasiyokuwa na ulazima, tusisitize kwenye sayansi ya lishe na tiba ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nayasema haya? Inasikitisha sana unapokwenda hospitali kwa ugonjwa tu wa kawaida, mfano una upungufu wa madini fulani fulani, au upungufu wa vitamini, basi madaktari wanakukusanyia *multivitamin* chungu nzima. Unaweza kwenda hospitali tu una kikohozi au una mafua, badala ya kupewa orodha ya vyakula ambavyo vinaweza kukusaidia na kurudisha haraka afya yako, basi madaktari wanakukusanyia madawa chungu zima. Ndiyo maana napendekeza tuiangalie mitaala yetu, badala ya kung'ang'ania tu kufundisha masomo kama *pharmacology* ambayo yanasisitiza na kuendeleza soko la madawa ya kemikali kutoka nje, sasa tuweke mkazo kwenye sayansia ya lishe na tiba ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Marehemu Baba wa Taifa aliwahi kufanya mipango kwamba sayansi ya lishe na tiba

asili ziingizwe katika mifumo rasmi ya Serikali; matabibu wa hospitali, shule za utabibu kama nilivyosema, ziwe zinasisitiza juu ya masuala haya. Kwa bahati mbaya sana jambo hilo jema hatukulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu ana msemo wake maarufu sana na naomba niurudie hapa, anasema hivi: "Waafrika ni watu wa ajabu sana. Wanapoona Wazungu wanafanya jambo hata kama ni la kijinga, watalifurahia, lakini Mwafrika anapofanya jambo hata liwe la maana la kiasi gani, wanalipuuza." Sasa ndugu zangu mimi nasema masuala ya umuhimu wa lishe na sayansi ya lishe na tiba asili siyo jambo jipya, lakini kwa sababu tu pengine amelisema Thomas Edison na Hippocrates, tunaweza kuliona ni jambo la ajabu. Jambo hili babu zetu, wazee wetu walilitambua zaidi ya miaka 1,000. Sasa nasema wakati umefika jambo hili tulifanyie kazi na tulipe uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Waheshimiwa Wabunge kwa vile ni dakika tano, kengele moja tu ikilia ujue muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa David Kihenzile nilimtaja, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben wajiandae.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa uliyonipatia ya kuweza kuchangia na kwa sababu ya muda nitajitahidi niende kwa haraka haraka. Moja, ni kutoa pongezi kwa kazi kubwa ambayo inafanyika na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kule Mufindi tuna msemo wetu kwamba, mfupa ulioshindikana, Samia anautafuna, kwa sababu mambo mengi yaliyoshindikana yameanza kufanyiwa kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nashukuru hotuba nzuri sana ya Waziri wa Fedha. Kimsingi ni hotuba nzuri inayotoa uelekeo wa

Taifa letu na tuna imani kubwa sana na Wizara kwa namna mnavyomsaidia Rais wetu. Namshukuru sana Katibu Mkuu wa CCM kwa ziara zake kwa sababu kwenye Jimbo letu la Mufindi Kusini ametugusa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niungane pia na wengine wanaomwombea Spika wetu heri katika ushindi wa nafasi anayoiomba huko mbeleni kwa sababu amedhihirisha weledi mkubwa katika kuongoza Bunge letu. Tunaamini akiwa Rais wa *IPU* atafanya vizuri zaidi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya kwenye Mkoa wetu wa Iringa. Tunaona mipango mikubwa ya ujenzi wa uwanja wa ndege, tunaona barabara kubwa za *Ruaha National Park* na ndugu yangu hapa, jirani yangu wa pale Kilolo, naye barabara yake ya Ipogoro inakwenda vizuri, kwa kweli tunashukuru Mungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Mufundi Kusini, Mpango wa *EPC + F* ambao umeweza kufanyika umesaidia pakubwa sana, unaanza kujenga barabara yetu ya Mafinga kwenda Mgololo na maeneo mengine kama barabara ya Sawala, miradi ya maji ya Mbalamaziwa, Malangali, mradi wa Igowole pamoja na maeneo mengine mpaka kule Mgololo. Pia tunashukuru kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* pamoja na kiwanda kikubwa cha kuchakata parachichi katika eneo letu la Nyororo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi machache, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize kwenye eneo hili na atusaidie. Rais Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya ziara mwaka 2022 mwezi wa Nane, akaahidi barabara ya Mafinga – Mgololo na Nyororo – Mtwango. Tunashukuru kwanza Mafinga – Mgololo imeshaingizwa tayari na mkataba umeshasainiwa; Nyororo – Mtwango pia imeshatajwa kwenye bajeti, lakini imewekewa Shilingi milioni 500 tu, imeleta sintofahamu kubwa kwa wananchi wote. Hata ile furaha waliyokuwanayo kwa Rais wetu imeanza kuwa simanzi. Tunaomba unapoenda kuhitimisha Mheshimiwa Waziri wetu utuambie kuhusu barabara ya Nyororo – Mtwango kilometa 40, tusaidie angalau hata kilometa zianze hata kama

zikiwa 20 au 30 ili hatimaye iweze kukamilika barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ombi letu lingine kubwa ni kwamba tunataka wenzetu wa Wizara ya Mifugo watusaidie vifaranga angalau milioni tano kwenye mabwawa yetu, wakati huo wenzetu wa Wizara ya Maji tunaomba mtusaidie kumalizia ujenzi wa Bwawa la Iramba pamoja na Ihuwanza. Ninaamini Mheshimiwa Aweso yuko pale atakamilisha hoja hii na ataweza kutusaidia iwe kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa TAMISEMI, Jimbo la Mufindi Kusini ndiyo jimbo pekee ambalo halijajengewa kituo cha afya hata kimoja tangu miaka miwili tulipoanza. Tunaomba kituo cha afya cha Mgololo na cha Mtwango mtusaidie. Kama haitoshi, tunaamini na tunaomba kabisa kituo cha afya kwa wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani watusaidie pale Nyororo ili tuweze kuimarisha ulinzi na usalama kwenye eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu. Moja, kwenye upande wa mapato, tunalo eneo muhimu sana, hapa tunazungumzia kuhusu mapato. Nataka Serikali itujengee mambo yote haya. Yako maeneo ya kupata fedha mojawapo ni eneo la biashara ya *carbon.* Wenzetu wa Gabon tumeambiwa watapata shilingi milioni 150, wenzetu wa Ghana wana pato la shilingi milioni 4.9, Ndugu yangu Kakoso kule kwake ana vijiji nane tu, kapata shilingi bilioni nne. Sisi tuna vijiji 12,000 hivi hatuoni kama kuna mabilioni ya pesa hapa? Hebu tutazame Wizara ya Fedha tukatafute pesa hapa, tukafanye kazi ya wananchi na kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, naomba mtusaidie kwenye kuboresha biashara nchini. Tunahitaji kuongeza walipakodi kama ambavyo kwenye hotuba wamesema, *tax base* iongezeke, lakini mkakati wa kuwajali na kuwaheshimu walipakodi kwa kweli hauridhishi. Tunawaomba Wizara ya Fedha mtusaidie, acheni utaratibu wa kukimbilia kufungia watu maduka. Wale ni Watanzania wenzetu, kaeni nao chini, zungumzeni nao, wapeni

ushauri, wafundisheni. Hamkupelekwa shule ili kwenda kuzalilisha na kunyanyasa wafanyabiashara wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hoja hiyo pia nigusie kidogo kwenye ajenda ya upande wa Wizara ya Kilimo. Wenzetu wa Wizara ya Kilimo wana ajenda ya *twenty thirty* ni hoja ambayo ukiisikiliza inabeba maono makubwa. Wana mpango ikifika 2030 tuweze kupata tupunguze umasikini kwa takribani 64%. Tutakuwa tumefanya kazi kubwa lakini tunahitaji *17.3 trillion*. Naiomba Serikali ianze kutenga fedha kila mwaka ili hatimaye tuweze kuja kufikia hatua ya kuweza kuboresha na kufanya mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu na tunatambua kwamba tayari tumeshaongeza Bajeti ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mwaka juzi, mwaka jana ikafika shilingi bilioni 754, mwaka huu shilingi bilioni 970 lakini twende zaidi tufanye kilimo, mifugo na uvuvi kama ajenda namba moja kama tulivyofanya miundombinu kwa miaka mitano mpaka saba iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nipende kushukuru sana kwa kunipa fursa hii ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben na Mheshimiwa Juliana Masaburi wajiandae. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mwita hayupo nadhani nitakula na zake nipate 10, hiyo ni zali la mentali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa sana kwa kweli uliyoifanya kwenye kipindi cha Bajeti iliyoisha. Mheshimiwa Waziri ni Mbunge nina miaka saba humu ndani. Unaona mishale siyo mingi, kiukweli umefanya kazi kubwa sana katika kila Jimbo tuna kila sababu ya kukupongeza yaliyoko ni madogo madogo ambayo tunahitaji kukushauri uyafanyie kazi ili baadaye mwakani mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi tunapoenda kujiandaa na Bajeti nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushauri sana Mheshimiwa Waziri, Mchango wangu wa leo mwingi nitakushauri. La kwanza; unakumbuka tulikuwa wote pale kwenye vurugu za Kariakoo, watu waligoma tukashinda siku nzima pale na sisi tulishawaambia mapema humu, mkatanguliza mizaha sasa naomba nikushauri. Mbunge mwenzangu Kanyasu hapa alilalamika kuhusiana na utendaji kazi wa mtumishi wa *TRA* pale Geita anaitwa Bwana Njau kwamba ameshika mtu akiwa kwenye *drip* ya *diagnosis* ya kusafisha figo chini ya kiti yaani yuko kwenye stuli na akajibu majibu. Kesho yake mkafuta kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nikwambie sijui mnataka labda na Geita nako kuandamane kwa sababu mtendaji huyu ana miaka karibia nane pale na kila siku watu wanalalamika. Anaenda anafunga biashara ya watu yaani wewe akikuona una duka la piki piki linafanya vizuri anakuletea kodi, anakuchimba mkwara, anafunga *account* baada ya wiki mbili yeye anafungua duka la kwake. Ukienda ukiangalia watu wote wenye biashara ya bar pale Geita wanaombwa risiti toa hivi, kesho unafungiwa *account* yeye bar yake inafanya *twenty-four, seven* na haina hayo mambo ya risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuombe Waziri nimekutajia anaitwa Njau tunalalamika hapa kwa mara ya mwisho. Vinginevyo kitaumana kule. Kama ni mzuri mchukue mpeleke wilaya nyingine, kwetu Geita ametosha tuletewe watu wengine. Hatuhitaji kuendelea kulalamika. Tutachukua maamuzi maana na sisi wananchi wametuamini kule wametuamini tuwasemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; nataka kujiuliza na bahati nzuri Ndugu yangu Mwigulu yeye ni mchumi. Tunahitaji kuwa na viwanja vya ndege vilivyo na biashara kubwa. Kiwanja cha Ndege cha Mwanza hivi mmetuonaje yaani kila mwaka sisi mnatusomea tu takwimu, mnatupiga tu kanzu, tunasikia tu mabilioni, kiwanja kiko vilevile. Jengo limejengewa *speed* limewekewa vioo mpaka vimeanza kuanguka. Tumelogwa na nani Mheshimiwa labda utuambie tuna tatizo gani tulichowakosea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ndege kwa Tanzania hapa ukiondoa Dar es Salaam kiwanja cha pili kilicho *busy* ni Mwanza, tatizo ni nini? Haiwezekani, tulikuwa na Mkuu wa Mkoa Gabriel aliyefukuzwa anasema kiwanja kiwe cha halmashauri. Amekuja mwingine aliyepelekwa Morogoro na yeye yule yule. Nimuombe Ndugu yangu Makala na nikuombe na wewe Waziri. Tunahitaji kuwa na kiwanja cha kimataifa cha Mwanza. Kwanza mmenunua ndege kubwa hii ya mizigo. Mnaitoa wapi mizigo kama Kanda ya Ziwa uwanja hauendeki? Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tunahitaji kuwa na kiukweli Mheshimiwa Waziri usipokuja na jibu zuri kuhusiana na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, hii imeshakuwa ni *too much,* ni dharau. Tutasimama Wabunge wote wa Kanda ya Ziwa hatutakubaliana na kukupitishia bajeti yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa jengo lipo, ugomvi uliopo ni kati ya halmashauri. Halmashauri ilitoa shilingi bilioni mbili sijui Serikali rudisheni, unatoaje hela kulia unaweka kushoto? Chukua maamuzi tutengenezee uwanja. Tumechoka kupigwa swaga, mwaka wa saba kila mwaka tunaletewa Bajeti ya Uwanja halafu hivyo hivyo, eeh? Haiwezekani leo ndege zote za Tanzania hapa biashara kubwa iko Mwanza. Tunaingiza fedha mnatuona sisi mbahau tunaona tu watu wanaenda hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usipokuja na majibu mazuri Mheshimiwa, kutoka Mwanza kwenda Serengeti ni kilometa 90 tunataka kuona wazungu. Tunataka kuona wazungu wanatua Mwanza, hivi hamjiulizi hata matajiri wakubwa wanaotoka Ulaya

na *jet* wala hawaendi Kilimanjaro kwa sababu ni mbali. Kilometa zaidi ya 500. Ukitoka Mwanza wanatua Mwanza wanaacha *jet* wanaenda na ndege ndogo pale dakika 15 wanaona wanyama tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga mahoteli, tumejenga kila kitu na Serikali imewekeza hoteli kubwa sana pale *Kapripoint,* mmeliacha tu limekuwa jumba la kulala popo kwa sababu hamna mikakati mizuri. Nikuombe Mheshimiwa Waziri ili tusiumane huko mbele nikuombe sana Mheshimiwa Waziri unapokuja hapa ututambie Uwanja wa Ndege jengo lile hebu hata wewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ukipita pale Mheshimiwa Waziri unaona mashine kubwa kabisa zimeletwa pale wanalala bundi tu mle halafu tunakaa hapa kupiga makofi, hatutapiga makofi mwishoni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; suala la mafuta, kwanza Ndugu yangu Mwigulu una wakati mgumu sana na nikuombe uchukue maamuzi. Nilijua utakuja hapa na taarifa ya kutuambia umepandisha bei, umepandisha ushuru wa mafuta yanayotoka nje ili shemeji zangu wa Singida wale wanaoshinda barabarani maelfu na maelfu wamening'iniza madumu mafuta yao yaende bei kubwa. Hivi kweli watu walivyolima vile kweli ndugu zangu, shemeji zangu wa Singida wale tushushe tena mafuta leo yanarudi shilingi 40,000, shilingi 8,000 kwa lita tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri kuku kaangukia kwa *sheikh* kwa hiyo, inabidi uangalie unachinja kuanzia mguuni au unachinjia shingoni. Watu wanakuangalia tunahitaji kuona zao hili na wakulima hawa hawakatishwi tamaa na kushuka kwa bei. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho dakika moja...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, la mwisho lile kwa hiyo tayari umemaliza ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja. Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana sisi tunatoka kijijini. Nyumba zetu kule kijijini ziko hoi usije tena na swaga hapa *brother* ya kutuletea kutuambia unaongeza buku kwenye *cement* acha. Njoo na mawazo ya kushusha, tumechoka kulala kwenye matembe na sisi tunataka kuwa na mabati kama mlivyo watu wa Dar es Salaam na mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Nilimtaja Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, Mheshimiwa Juliana Masaburi, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu wajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nipate kuchangia Bajeti yetu ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Kwa sababu ya muda nitakimbia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshika kitabu cha Bajeti aliyoisoma Mheshimiwa Waziri wa Fedha tarehe 15 wiki iliyopita na ninataka nianze kwa kunukuu ukurasa wa 182 unasema. "Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii tena kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa uongozi wake bora na thabiti wenye mafanikio makubwa hususan katika kuleta mageuzi ya kiuchumi pamoja na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kikanda na kimataifa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. Hakika Mama apewe Maua yake." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Bunge hili nimeifuatilia kwa ukaribu sana bajeti hii na nimeisoma vyema sana *Finance Bill* ambayo tunaendelea Kamati ya Bajeti kuwasikiliza wadau.

Ninaungana na Waziri wa Fedha kusema Mama apewe maua yake kwa kupitia Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; mwaka jana tulikuwa na Bajeti ya shilingi trilioni 41.48. Bajeti hii tunayokwenda kuipitisha ni ya shilingi trilioni 44.39, hili ni ongezeko la shilingi trilioni tatu nzima na ni ongezeko la *almost* 7%. Ndugu zangu katika macho ya kibajeti na kitaalamu hili siyo jambo jepesi, ninasema Mama apewe maua yake. Miaka miwili iliyopita tulishauri hapa kwamba nchi yetu ifanyiwe *credit rating*. Serikali sikivu ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ikafanya jambo hilo. Hivi sasa ninavyozungumza nchi yetu iko *rated* na makampuni mawili makubwa duniani ya *credit rating,* Kampuni ya *FITCH* na Kampuni ya *MOODY'S. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mara baada tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kusoma Hotuba yako ya Bajeti siku zile, wenzetu ambao tumewapa kazi ya kutusimamia kwenye mambo haya ya fedha na kutushauri, Kampuni ya *MOODY'S* wametoa taarifa yao sijui kama umeiona. Taarifa hii na yenyewe imedhihirisha kwamba Mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenzetu wame-*appreciate* kwamba kwenye Bajeti yetu, mapato yameongezeka. Lakini la pili, hatua zote za kikodi ambazo zimechukuliwa zinatufanya Tanzania tuendelee kuwa nchi inayokopesheka. Kwa hiyo, tutaendelea kuaminika kwenye masoko ya kifedha makubwa huko duniani lakini kwa nini Mama apewe maua yake? Wenzetu wa *MOODY'S* hawa wanastaajabu. Wanashangaa kuna mambo makubwa matatu yanafanyika ndani ya nchi yetu pamoja na ongezeko hili la bajeti na pamoja na kipindi kigumu hiki cha uchumi kwa dunia nzima. Jambo la kwanza wanasema, wanalishangaa, linawezekanaje kwa Tanzania kufanyika? La kwanza; *higher spending for ongoing infrastructure projects. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *MOODY'S* wanashangaa inawezekanaje Tanzania inaongeza bajeti na inaenda kuongeza makusanyo ili hali inapeleka fedha nyingi sana

kwenye miradi mikubwa ambayo kwa ukanda wetu wa Afrika na hasa hasa Kusini mwa Jangwa la Afrika haipo miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza ni reli ya *SGR* na ambayo inajumuisha ununuzi wa vichwa na mabehewa. Kwenye hili ushauri wangu kidogo tu tutafute vichwa na mabehewa angalau kwa *root* moja tu kwa Serikali halafu tuwaachie *private sector*. Tuwe na *line* moja tu inayoweza kutusaidia kufanya kui-*regulate* biashara lakini tuwaachie *private sector* ifanye eneo hilo la vichwa na mabehewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo wanatushangaa ni ujenzi wa Bwawa kubwa la Mwalimu Nyerere. Kote huko kunakwenda na *trillions.* Wanashangaa ujenzi wa Daraja la Busisi kule Kigongo. Wanashangaa skimu kubwa za umwagiliaji ndiyo maana wamekuja na taarifa wanasema Mama apewe maua yake wanaungana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na mimi naungana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wanashangaa sana fedha zinatoka wapi za kujenga miundombinu kwenye Mji wetu wa Kiserikali pale Mtumba. Unajua, *you cannot know what you have until you lose it.* Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ni mwalimu wangu lakini leo naomba nisione haya nikupongeze mbele ya Watanzania. Nakupongeza na ninataka nikwambie una bahati kufanya kazi kuwa Waziri wa Fedha chini ya Rais wa aina hii ambaye tunaye. Naomba nirudie hii *statement,* Mheshimiwa Dkt. Mwigulu una bahati sana kuwa Waziri wa Fedha katika kipindi ambacho tuna Rais wa aina hii Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanaendelea kushangaa wanasema inawezekanaje Watanzania wanayafanya haya wanapeleka miradi ya barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesaini hapa miradi ya barabara mingi sana lakini na mwisho kwenye miradi hii mikubwa mikubwa wanasema wanashangaa kuona miradi ya huduma za kijamii. Hakuna mahali Tanzania hii ambapo hapajengwi kituo cha afya, hakuna mahali Tanzania hii hapajengwi hospitali, hakuna mahali

Tanzania hii hapajengwi shule, hakuna mahali Tanzania hii hapapelekwi umeme. Hakika Mama apewe Maua yake na kwenye hili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Juliana Masaburi, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Bakar Hamad, Mheshimiwa Emmanuel Shangai na Mheshimiwa Riziki Said Lulida wajiandae.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi niungane na wenzangu Wabunge wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini kipekee pia kumpongeza Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Kusema ukweli wote mnastahili maua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwa haraka haraka kwa ajili ya muda. Kwanza napenda kuchangia kwenye mambo matatu. Jambo la kwanza ni *cargo consolidation* na *deconsolidation* kusajiliwa kwa *store* na mfumo wa *EFD Machine*. Nikianza kwenye *consolidation* na *deconsolidation*. Kuna tatizo hasa kwenye hawa wasafirishaji wa mizigo ambao wafanyabiashara wakienda kwa mfano China, Uturuki, Marekani nchi yoyote wanaenda kununua mizigo kwa ajili ya kuleta nchini kwa ajili ya mauzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa wafanyabiashara wengi wanatumia wasafirishaji wa mizigo ambao kitaalam kwa lugha yao *TRA* wanaitwa *consolidation* na hao *consolidation* kazi yao kubwa inakuwa kukusanya mizigo ya wafanyabiashara wengi na

kuweka kwenye *cover* moja au *container* moja. Sasa nachangia kuhusu hili kwa sababu gani? Kwa ajili ya mgogoro mkubwa uliotokea kama mwezi uliopita pale Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *consolidators* ambao wanafanya biashara ya kukusanya mizigo ya wafanyabiashara wadogo wadogo na kuingiza nchini mfumo huu Serikali ilikuwa na nia njema kabisa kwa ajili ya kuandaa mfumo huu wa hawa wasafirishaji kukusanya mizigo ya wafanyabiashara. Walikuwa na nia njema kabisa na walikuwa sahihi lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha mfumo huu ndiyo unawasababishia kukosa kodi halisi, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara anapoenda Guangzhou au nchi yoyote ile anaenda kununua mzigo anapewa risiti kwenye manunuzi yake. Anaenda kwenye maghala kule Guangzhou au Beijing au popote, *consolidator* anachukua ule mzigo kwa nia ya kumsafirishia mpaka nchini kwake na *consolidator* anapofika hapa nchini anaingiza ule mzigo kwanza kwenye forodha anaingiza ule mzigo anasema yeye ni *consolidator,* anaingiza kwa pamoja lakini kwenye ulipaji wa kodi Mheshimiwa Waziri wa Fedha hawa *consolidators* wanatumia mbinu za kukwepa kulipa kodi halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale kwa kamishna wa *TRA* wa kodi za ndani wakiwa wanakaguliwa wanaingiza hii mizigo kwa majina yao au kwa kampuni zao na *remind you* Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakishaingiza hii mizigo kwa majina yao kwa kampuni zao wanalipia ile mizigo wao wenyewe pale *TRA*. Wakishailipia ile mizigo wanaenda sasa nje kwenye maghala yao mizigo ikishatoka wanawapa wafanyabiashara wale mizigo yao bila kuwapa risiti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linakuja sasa afisa *TRA* anapoenda Kariakoo kukagua mahesabu ya wafanyabiashara au mizigo tatizo linakuja wale wafanyabiashara wanakuwa hawana risiti halisia kabisa na ndiyo maana wanapokuwa wanakisiwa kodi wanasema wanaonewa kwa sababu kiukweli wanakuwa hawana kumbukumbu ya risiti na risiti zinabaki kwa

msafirishaji. Nia ilikuwa njema lakini naona inafanyika vibaya sana sasa hivi.

**TAARIFA**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba taarifa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa mchango mzuri Mheshimiwa Mbunge. Nataka nimwambie sababu hiyo ndiyo inayofanya ulipaji wa *VAT* uwe mgumu kwa sababu kodi ya *VAT* ni *input tax* na *output tax*. Sasa bila kuwa na *VAT* uliyolipa wakati ukiingiza mzigo huwezi ukatoa risiti kwa minajili ya kulipia *VAT* wakati ukiuza na ndiyo maana kuna bei ya bila risiti na bei ya risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Masaburi unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa hiyo ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni Mheshimiwa Abbas Tarimba. Sasa kama Mheshimiwa Abbas Tarimba alivyosema kwa hiyo hapa kuna tatizo Mheshimiwa Waziri na ninakuomba sana ili pia uwaziri wako siku ukiondoka uache *legacy* hili suala linatakiwa kushughulikiwa haraka na ipasavyo na hili suala la hawa *consolidators* unawaona hata wafanyabiashara wenyewe hawalalamiki kwa sababu kwanza wanapata faida. Wanapata faida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kariakoo nilienda kuhudhuria sijamsikia mtu kulalamikia kuhusu hawa wasafirishaji *consolidators* kwa sababu *they know* wanapata *profit, I mean triple.* Umeona Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu ni nini? Ushauri wangu sawa kuwe na hawa *consolidators* wasafirishaji hawawezi

kuepukika kwa ajili ya urahisi wa kusafirisha mizigo ya wafanyabiashara lakini Wizara yako na *TRA* waone njia sahihi ya ku-*accommodate* hawa wasafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza mfanye kama ile *bonded warehouse* ya magari. Mizigo ikishafika ikae waipeleke kwenye *bonded warehouse* kila mfanyabiashara akafutae mzigo wake apewe risiti zake, akalipe kodi mwenyewe. Hii itasababisha kwanza Serikali nyinyi kupata kodi zenu halisi lakini pia wafanyabiashara kutoogopa kwamba kuwe na *point* kwamba kuna mlolongo wa watu au foleni au nini lazima kila mfanyabiashara alipe kodi kwa sababu ya mahesabu ya kampuni yake au biashara yake kuwa safi na sahihi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, Juliana Masaburi tunaendelea na Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kwa niaba ya watu wa Masasi ningependa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo. Pia nikishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kinachoongozwa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupigania Watanzania lakini kipekee kwa kunipigania mimi Mbunge wao kule Masasi kwa kuhakikisha kwamba changamoto za Masasi zinaondoka. Na Masasi sasa hivi ni mpya, na kila mmoja anaiona kwamba Masasi inang'ara. Hiyo yote ni juhudi za Mheshimiwa Rais kuniunga mkono mimi kama Mbunge wake tukishirikiana na Mheshimiwa Madiwani ambao niko nao kule Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ningetamani nichangie kwenye bajeti hii ambayo imewasilishwa

na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Tunafahamu kwamba bajeti ni makadirio ya mapato na matumizi, ni makadirio tu. Kwa hiyo nina michango kwenye maeneo haya mawili; mapato na matumizi. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize, najua itamsaidia. Na kwa sababu muda ni mdogo nitajitahidi kwenda haraka haraka. Yeye ni mchumi mwenzangu, anajua, kwamba nikizungumza kitu basi ajue namna ya kuki-*pick.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, na hii naendelea kusisitiza sana; *any sense to the government, the first concern* ni *employment* ya vijana wake. Tukitengeneza fursa pana za ajira kwa vijana tafsiri yake tunaongeza *direct tax payment*. Kwa upande wa wale vijana wanalipa kama *pay as you earn,* ambayo ni *personal income tax* kutoka kwenye mishahara yao lakini pia makampuni na shughuli watakazokuwa wanazifanya nazo zinalipia *cooperate income tax,* ambayo ni *direct tax* ambayo ni ya uhakika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukifanya hivyo tunaweza tukahakikisha kwamba tunatoa fursa pana zaidi kwa Serikali kukusanya kodi ambayo inaweza ikasaidia kwenye upande wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaendana na adhma ya kupanua *tax base*. Amezungumza Mheshimiwa Kihenzile hapa inasumbua kidogo; na bahati nzuri nilihudumu kidogo kwenye Bodi ya *TRA*. Tunaolipa kodi ni wachache sana kwenye nchi hii. Sensa imeonesha kwamba tuna watu milioni 61 lakini walipa kodi hapa ni kama milioni tatu tu wale wenye *active TIN Number,* wako milioni tatu tu; na hiyo ni watu binafsi pamoja na kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo ni watu wachache sana wanaolipa kodi, matokeo yake *concentration* inakuwa kubwa kwa sababu wachache wanaolipa kodi wanalazimika kulipa kodi sana na wanalazimika kukamuliwa sana ili kufikia malengo ya kitaifa, lakini tungetanua *tax base* tungerahisisha na kufuata zile *rules* tano za usimamizi wa kodi. Kwamba kodi lazima kuwe na *fairness,* kodi lazima kuwe na *adequacy,* kodi itoshe kuitosheleza

Serikali lakini kuwe na *simplicity,* kuwe na urahisi wa ulipaji kwa yule mlipa kodi kwa sababu ya *compliance* iko juu lakini lazima kuwe na *transparency* la mwisho lazima *administratively* kuwe na *easiness*, kuwe na urahisi wa kukusanya hizo kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natamani nigusie kwenye maeneo ambayo tunaweza tukasaidia hawa vijana kupata ajira nyingi pia tupate kodi za kutosha. Eneo la kwanza; tunafahamu kuna ule mradi wa Mkurabita nchi yetu sisi *structure* ya uchumi wetu asilimia 60 mpaka 70 ni *informal sector*, kule kodi huwa hazipatikani kirahisi kwa sababu si sekta rasmi. Kwa hiyo Mkurabita nafikiri imeshakufa. Lengo kubwa lilikuwa ni kuweza kutengeneza utaratibu wa kampuni mbalimbali na watu binafsi shughuli zao ziweze kurasimishwa ili waingie kwenye *tax net* waweze kulipa *taxes* kwa kuwa *tax payers.* Kwa hiyo nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Waziri arudi kwenye ku-*reform informal sector* ili ziwe *formal* kupitia mikakati mbaliambali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, mwaka wa jana Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Mwenyekiti lilipitisha azimio kutoka kwenye Kamati yetu ya *PAC* la ku-*undertake a comprehensive tax system regime of view* ambayo ilifanyika mwaka 1992 ambayo ndiyo iliyotengeneza mifumo ya kuanzishwa kwa *TRA*. Kwamba ni *structure* ya aina gani ya kodi tulipe, nani alipe, aina gani ya shughuli zitozwe na viwanda vikoje. Yaani tupitie upya huo wigo mzima wa kikodi ili tuhakikishe kwamba tunapata walipa kodi sahihi aina ya kodi sahihi pia na mfumo wa ukusanyaji ambao uko wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni uwajibikaji wa wizara zingine zote za kisekta kumsaidia Waziri wa Fedha kukusanya mapato, kumsaidia kutengeneza mapato. Kazi ya wizara hizo ni kutengeneza vyanzo vya mapato kwa ajili ya Wizara ya Fedha. Kwa hiyo kila Wizara ingetakiwa kuwa na lengo inayopewa iwe ni *four trillioni*, wewe *five 5 trillion*, wewe *three trillion*. Wakae na kuona; yale maeneo ambayo Waziri wa kisekta ana changamoto nayo anamwambia Waziri wa Fedha ili nikuletee *four trillion* naomba labda *10 billion* kwenye eneo hili. kwa mfano Mheshimiwa Waziri Bashe anaweza kabisa kuweka mkakati wa

kufufua viwanda vya korosho kule Masasi, Tunduru, Lindi na kwingineko; ili ajira zikiwa nyingi pamoja na kuongeza thamani kodi inakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunafahamu kwamba tuna mradi mkubwa wa *Mtwara Development Corridor* ambao unatakiwa kuchochea kule ikiwemo Liganga na Mchuchuma pamoja na ujenzi wa ile reli ya kule Kusini. Tukifanya hayo na matumizi sahihi ya Bandari ya Mtwara tutakuwa na trilioni ya fedha ambazo tutazikimbia. Lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja asilimia 100 na sisi watu wa Masasi tuko Imara kuweza kuhakikisha kwamba tuna-*support* Chama cha Mapinduzi kiweze kupata maendeleo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia bajeti yetu ya Serikali iliyowekwa mezani na kaka yangu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na Naibu wake ndugu yangu Chande.

Kwanza nitumie nafasi hii sana kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nilikuwa nanukuu hapa sentensi iliyoandikwa na Kamati ya Bajeti, ikanipendeza sana; niinukuu; "Napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuonesha kwa vitendo nia yake thabiti ya kuondolea Watanzania umaskini na kuwaletea maendeleo. Aidha utu wake katika kuleta mapinduzi *ya* kiuchumi,

kisiasa na kijamii umekuwa ni msingi imara katika kutekeleza kauli yake mbiu ya kazi iendelee."

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maneno ambayo kila Mtanzania hawezi kuyabishia. Ni maneno sahihi ambayo anastahili kupewa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ziada nimpongeze pia Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa jinsi wanavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza yale ambayo ameahidi kuwafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka kwa sababu ya muda nitajielekeza kwenye maeneo machache tu. Jambo la kwanza lilisemwa wakati tunachangia bajeti za kisekta, Wizara ya Afya; suala la urasimishaji. Nipongeze sana Serikali katika hatua sasa hivi iliyofikia ninao mkopo wad ola milioni 150, takribani bilioni 345 ambao utaenda kusaidia maeneo mengi kwenye eneo la Wizara hii ya Ardhi. Niombe sasa, utekelezaji huu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ujielekeze kule, kama wenyewe walivyosema, fedha zitoke ziende zikamalizie mgogoro wa urasimishaji ndani ya mitaa iliyopo ndani ya Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara ya kisekta inasema itatatua mitaa 559 mimi nina mitaa 42 hivi; kwa hiyo ipo tayari kwenda kumaliza. Mwakani naamini wakati tunapitisha bajeti yetu ya Serikali sitoongea tena mambo ya ardhi. Nina imani sana mambo mazuri yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine niipongeze tena Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni eneo la barabara. Tumepiga kelele humu kwenye bajeti za kisekta; lakini hata hii bajeti kuu imeeleza vizuri juu ya barabara kubwa za kimkoa, kiwilaya na miradi mingine itakayoendelea. Kule ndani ya Jimbo la Kibamba barabara za chini ya *TARURA* na *DMDP* tayari, tunaishukuru sana Serikali. Tumeshasaini na wakandarasi na washauri *(consultants);* vilevile na *stakeholders,* tumefanyia Dodoma na Dar es Salaam. Leo wananchi wanajua kwamba miradi inaenda kutekelezwa kuanzia mwezi wa nne mwakani.

Barabara ya Kingongo inaenda kutengenezwa kwa lami, tunaendelea. Barabara ya Msumi kilometa nane inafungua kutoka Madale hadi Stendi ya Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kwa Shija kilometa 4.2, pia na Barabara ya Konoike kule ambako kuna tenki kubwa la mshikamano ambalo tumejengewa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo mambo ni mazuri. King'azi – Malamba Mawili kilometa mbili za lami zinaanza mwezi wa nne kwa hiyo hili ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Barabara, niliuliza swali la nyongeza asubuhi. Kuna ahadi nyingi. Bajeti yako inasema moja ya vigezo ukiondoa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na mambo mengine lakini ahadi za viongozi wa kitaifa ni eneo ambalo linazingatiwa. Hili nimesema asubuhi chini ya asilimia 50 embu tukaliangalie ili tuendelee kuwaheshimisha viongozi wetu hawa. Wanakwenda kutembelea maeneo wakitoa ahadi zitelekezeke. Ni vizuri sana kuangalia zote za miaka ya nyuma muweze kuzitengea fedha na kuzitekeleza zile ahadi za viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la maji. Mheshimiwa Waziri taarifa yako imesema na yenyewe vizuri, niendelee kuwapongeza. Dar es Salaam Jimbo la Kibamba mambo ni mazuri na tunaendelea kuunganishiwa maji. Lakini shaka yangu, wakati wa kiangazi tunakosa maji ya Ruvu ambayo ni tegemeo katika miaka tangu tunapata uhuru. Leo *population* ni kubwa, zaidi ya watu milioni 5.4. Haiwezekani wakategemea chanzo kimoja, tunajua tumewekeza kwenye Bwawa la Kidunda basi niombe sana utekelezaji wake uende haraka ili sasa wananchi hawa katika mikwazo ya vipindi vigumu tuendelee kuwapatia maji safi na salama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu. Nilimtaja Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru Mungu kwa kunifanya niweze kuzungumza hapa leo. Kipekee kabisa nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kupendekeza nifike huku Bungeni kuwasemea, na nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kuruhusu jambo hilo likawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, muda ni mchache, lakini naomba kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti hii ambayo imekuwa ni bajeti yenye furaha katika Tanzania yote na kila mtu anasherekea. Mimi pia nimesimama kuipongeza bajeti hii pia kwa kuleta mapendekezo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake na wote ambao wamehusika kwenye hii bajeti na niunge mkono pendekezo kutoka katika Kamati yangu ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa yetu ya mwaka 2022 imetufungua na kutuonesha mambo mengi wananchi wa Tanzania tuko milioni 62 na ushee. Na niseme kwamba bajeti hii iliyoletwa hapa mbele yetu imekuja ili sasa ipatiwe au trilioni 44 na ushee ziweze kupitishwa kwenda kutekeleza mengi. Mimi niseme rasmi kabisa kwamba naunga mkono tuweze kuipitisha kwa pamoja na kwa uzito mkubwa. Hii ni kwa sababu ametusomea Waziri wa Fedha; kwamba tunakwenda sasa kukuza uchumi, kuzalisha ajira na pia kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi ambayo naweza kuyagusa lakini ningependa nizame kwenye eneo la kilimo, uvuvi na ufugaji. Niombe sasa twende kufanya kilimo

chenye tija na uvuvi wenye tija pamoja na ufugaji wenye tija. Wenzetu Israel wanazalisha kwenye ekari moja tani 20, 000 za ndizi lakini sisi tunazalisha mikungu kadhaa inayohesabika. Sio hiyo tu lita 40 za maziwa kutoka kwenye ng'ombe mmoja sisi tunazalisha lita tatu zikizidi sana lita tano. Sasa tuna wasomi kutoka SUA na kwingineko; ni wapi tunapokosea? teknolojia haipo. Nimwombe sana Waziri wa Fedha aweze kusaidia anapotoa fedha hizi ziende nyingi kwenye *research* ili watu wengi waweze kwenda kujua nini kinafanyika na wenzao na *research* hizo zishuke sasa, zikasaidie wale wanawake wanaofuga na wale wote wanaofuga twende kwenye ufugaji wa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule ukurasa wa kitabu cha bajeti ule ukurasa wa 108. Kuna ile *roman three,* inaleta ukakasi kutoza ushuru wa bidhaa wa kiwango cha shilingi 20 kwa kila kilo moja ya saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi. Najiuliza hivi hii inayozalishwa ndani ya nchi wanaaminia kweli nasema hivyo kwa sababu gani? nyumba sio hitaji la *luxury man slop* kwenye hiyo *rank* of *needs* alisema *food, shelter anda clothing.* Sasa hii ni *shelter* hatutaki mwananchi wa Tanzania alale nje. Nilikuwa naomba hili pendekezo ni zuri kwa sababu saruji inachafua au pia siku nyingi sana hawajagusa, Serikali haijagusa ni kweli haijagusa lakini mbona kuna maeneo mengi ambayo tungeweza tukafidia jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwarudishe nyuma mwaka jana tulisimama hapa tukasema magari ya Serikali yasingurumishwe wakati viongozi wameshuka, wamejirekebisha; sasa hivi magari ya Serikali yakisimama yanazimwa. Lakini kuna maeneo mengine hayo hayo kwenye Serikali yangeweza pia kuangaliwa. Kwa sababu gani? gari linakaa mpaka linachakaa hatuoni marekebisho mazuri. Je, vipuri vinavyowekwa ni vizuri? Yaani naomba Serikali nayo pia iangalie kwenye maeneo yanayowahusu. Wewe *cost conscious* kama wataweza kubana matumizi huko hakuna haja ya kumtoza maskini au mtu ambaye hana uwezo. Hizo fedha zote hizo shilingi 1,000 kwenye mfuko wa saruji mtu ambaye hajajenga nyumba. Kuna familia au kuna *culture* ambazo mtu hawezi kwenda kuzikwa kaburini bila kuingizwa kwenye nyumba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna nyumba za mitembe ziko huku Dodoma kuna nyumba za *full suit* ziko Kilimanjaro. Hivi kweli mtu miaka yake 70 aliyopewa na Mungu aishi kwenye dunia kama hii kwenye utawala mzuri kama wa Dkt. Samia Suluhu Hassan bila kuwa na nyumba nzuri, nyumba nadhifu, nyumba ya matofali. Mimi naomba sana huu ujenzi wa nyumba uonekane ni hitaji na siyo *luxury*. Tupangishe kwingin,e kupo mahali pengi. Na niombe sana Serikali iangalie pia watu binafsi wanawezaje kubana matumizi na kwa nini wao washindwe. Naomba sana hilo ni ombi naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja tena.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond nilimtaja Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Bakar Hamas ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya uchache wa muda tuliopewa, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tukiwa kama Wabunge sisi tuna nafasi ya kusema vitu ambavyo vinatoa *direction* ya nchi. Kwa dhati ya moyo wangu niseme mafanikio yote tunayoyazungumza ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, sisemi kwa sababu Waziri huyu wa Fedha ni kaka yangu. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kaka yangu nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu umeitendea haki sana Serikali ya Awamu ya Sita katika masuala mazima ya usimamizi wa *fiscal policy and monetary policy* na ndiyo maana tunapoangalia hali ya uchumi wa nchi za Afrika ya Mashariki ukiangalia masuala mazima ya *inflation*, bei za vyakula na bidhaa Taifa la Tanzania ndilo nchi peke yake *stable* katika mataifa yote ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *credit* kama hizi hatuwezi tukaku-*ignore* kaka yangu Mwigulu. Niseme kwa dhati ya moyo wangu, unamfanya Rais wetu kuwa *proud,* na sisi kama Wabunge tunalisema mchana kweupe, wewe ni moja ya mawaziri bora kabisa kuwahi kutokea katika sekta ya fedha katika nchi yetu, *keep it up* kaka yangu kaza Kamba kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nalotaka kulisema; kuna maneno mengi yamesemwa mtaani, kuna watu wamefikia hatua ya kutaka kuligawa Taifa, na hili nalisema kwa sababu ni Bajeti Kuu ya Serikali. Rais anahangaika kutengeneza *base* za kuleta kodi kwenye nchi, uwekezaji unaozungumzwa, Rais wetu anahakikisha ili tuache kukimbizana na mikopo Taifa liwe na *revenue* zake. Rais amefanya mipango kupitia Serikali, tunao watu wa *DP World.* Kuna watu wamekwenda kusema nchi imeuzwa. Mimi nataka nisome vipengele vya kisheria ambavyo vinaonesha upotoshwaji uliofanywa mtaani ulikuwa ni makusudi na lengo la kuchafua na kuleta *instability* ya umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma *Article One* ya Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai ukurasa wa 9 katika *land right;* kwa sababu unaposema nchi inauzwa unamaanisha tumeuza mamlaka ya nchi na tumeuza ardhi. *Article* 1 inasema "*land right shall mean all those rights excluding the right of ownership of land*", huu mkataba. Sasa hoja ya kusema nchi imeuzwa inatoka wapi? mkataba unasema *right of ownership, exclusion* imewekwa kwenye *right* ya *ownership* ya ardhi. Acheni kudanganya watu, achene kuchafua nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Rais hawezi kuliuza hili Taifa na ndiyo maana ni Amiri Jeshi Mkuu. Tumemwamini, tumempa madaraka na hafanyi maamuzi kwa sababu ni Mzanzibar. Nataka niwaambie, Mzanzibar ana haki ya kuwa Waziri kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hatma iko kwenye muungano huu. Haiwezekani tukaanza kuleta mambo huyu Mzanzibar, tutavunja muungano wetu. Tunaomba wanaofanya hayo wakome mara moja Mama apewe maua yake kwa kuleta kampuni hii kuja kufanya uwekezaji utakaoleta tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na mambo mengine kwenye mkataba wamezungumzia *article* 22 wanasema mkataba huu tumejifunga, *amendment* zimezungumzwa kwenye *article* 22. Jambo lingine wamesema mkataba huu, sheria sijui tukishtakiana wapi *article* 21 imesema *governing laws* zitakazotumika ni za Serikali ya Tanzania. Mheshimiwa Waziri nataka niwaambie kafanyeni kazi, sisi kazi yetu tulihaidi, sisi ndiyo tuna Ilani, msitishwe na mtu, tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kumshauri kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Serikali. Wananchi wetu na viwanda vimekuwa vikilalamika, bei ambayo imekuwa ikitozwa katika *electronic stamp* imekuwa ikisemekana ni kubwa. namshauri Mheshimiwa Waziri kwa nini wasiwaite wawekezaji wa *SICPA* wakae nao, wawaombe washushe bei ili kusudi wafanyabiashara waweze kuwa na manufaa katika gharama hizi zinazozungumzwa. Najua wamefanya kazi kubwa pamoja nao ya kizalendo, mapato ya Serikali yameongezeka, uchumi wa Taifa unakua, miradi inaendelea kuwa *financed* kwa sababu ya mapato anayokusanya kaka yangu. Wakae na watu wa *SICPA,* wazungumze nao ili washushe gharama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nakuomba radhi sana dada yangu. Jambo la mwisho nataka niseme kama alivyosema kaka yangu Kwagilwa Mama Samia apewe maua yake. Ripoti zinaonyesha mwaka 2001 *net in flow* ya *foreign direct investment* ilikuwa asilimia moja. Mwaka mmoja baada ya Mama kuingia madarakani ikapanda mpaka 1.4

Mheshimiwa Spika, *UNCTAD* wametoa ripoti wanaonyesha uwekezaji kwenye Taifa umeongezeka kwa asilimia 34, ripoti ambazo alikuwa anasema kaka yangu, inaonyesha kwamba Taifa limepanda katika *ratio* za kimataifa katika masuala mazima ya kiuchumi. Nani kama Mwigulu jamani? Hivi kweli tutasema hatuna Waziri imara wa Fedha. Naomba kaka achape kazi, Wabunge tunamuunga mkono, Rais tuko nyuma yake,

waharakishe katika uwekezaji wa bandari, wasitishwe, tutatoka hapa, tutakwenda mtaani, tutawaeleza wananchi umuhimu na manufaa ya uwekezaji huu kwa maslahi ya Taifa letu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu. Nilimtaja Mheshimiwa Bakar Hamad, Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Anatropia wajiandae.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niwe mchangiaji kwenye Hotuba yetu hii ya Bajeti ya Serikali. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kutenda mema kwa Watanzania, lakini nimshukuru na nimpongeze kwa bajeti hii ambayo jumla ya zaidi ya trilioni 44 ambayo ametuletea mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia na nimpongeze kwa utendaji kazi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo afya, ikiwemo elimu, ikiwemo ujenzi wa Barabara, lakini reli ya kisasa ambayo inaendelea kujengwa, lakini nimpongeze kwa mambo mbalimbali ambayo yanaendelea kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitatenda haki kama sikumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa namna ambavyo wanaendelea kushirikiana kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ambayo Watanzania wamewakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze na niwashukuru sana kwa namna ambavyo wanaendelea kushirikiana na Wizara inayohusika na Fedha na Mipango ya Zanzibar. Kwa kweli kulikuwa changamoto nyingi ambazo ziko kwenye maeneo yao, walipoingia wao wamekwenda kushirikiana katika utatuzi na leo hii tunazungumzia mambo mengi ambayo yamefanywa mazuri kwenye ushirikiano huu wa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatie moyo na niwaombe Wizara hii waendelee kupiga kazi. Sisi tuko pamoja nao na tunawaunga mkono, tunawaombea sana Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya bora, lakini pia hekima iendelee kuwatawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uwekezaji. Hatuwezi kuongeza idadi ya walipakodi, hatuwezi kupiga hatua ya kuongeza watu wenye ajira kwenye nchi yetu kama hatukuhamasisha, kama hatukuendelea kujenga mazingira rafiki, kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwekezaji haliepukiki, ni lazima nchi yeyote kwanza iangalie wananchi wake na hususani kundi kubwa la vijana. Vijana hawa lazima tuwaangalie kwenye suala la ajira na kwenye suala la ajira hatuwezi kwenda kwenye ajira kama hatukuweza kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali ambayo yanazalisha ili kuweza kuwapa vijana wetu ajira. Tunapoongeza ajira maana yake tayari tunaongeza walipakodi na hapo ndipo tunapokwenda kuzungumzia suala la upunguzwaji wa viwango vya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza sana kwamba viwango vya kodi bado viko juu, lakini tutafanyaje kwa idadi hii ya walipakodi ambao wanahudumia Watanzania walio wengi? Hatuwezi kupunguza viwango hivi, lakini nadhani dawa ya jambo hili ni kuongeza walipakodi hasa wa kuwekeza maeneo mbambali ili kuweza kupunguza *rate* ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ifike mahali Tanzania tuache, tubadilike na tubadilishe *mindset* zetu, tukiona tu hatuwezi kumwona tu Mzungu yeyote au mtu mweupe yeyote tu hapa nchini halafu tukawa tunadhania amekuja kutuibia. Dhana hizi potofu ni lazima tuzipige vita, ni lazima wananchi wa Tanzania wabadilike, hakuna, haiwezekana kwamba nchi yetu sisi tuwe sisi tu wenyewe tu tumejifungia, haiwezekani. Tuna-*lack of experience* katika mambo mengi sana, tuna-*lack* mitaji kwa mambo mengi sana lakini tuna-*lack* teknolojia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wana fedha, wenzetu wana teknolojia nzuri, wenzetu wana uwezo wa kuweza kutekeleza mambo mbalimbali, lazima tuweke mazingira rafiki na lazima tuwavutie. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa hakika anaendelea kufanya kazi kubwa kwenye kuwavutia wawekezaji kuja nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo moja ambalo mchango wake mpaka sasa ni mdogo kama vile limesahauliwa. Suala la uvuvi, bado rasilimali tuliyonayo kwenye bahari ni kubwa sana, lakini ukiangalia mchango unaochangiwa kwenye sekta ya uvuvi ni asilimia 1.8. Kwa kweli katika eneo hili ni lazima tuendelee kuwekeza ili kuweza kuongeza, kuweza kutumia bandari yetu au kuweza kuitumia bahari yetu katika kuongeza pato la Tanzania, kuongeza ajira, lakini pia kuweza kupunguza ile *rate* ambayo nimezungumza pale mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bakar Hamad. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Anatropia Theonest wajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Nianze kwa kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiona yote yanayofanyika kwenye nchi yetu ni kwa sababu ya uongozi imara wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini hawezi kufanya kazi mwenyewe lazima wawepo washauri. Kwa upande wa fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ameonekana kujipambanua na kumshauri Rais ipasavyo. Kwa hiyo nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwenye bajeti yetu tumeweka vipaumbele vingi, lakini ili tuweze kutekeleza yale yote

ambayo tumesema ni lazima tusimamie makusanyo na fedha na tuweke nguvu kwenye Mamlaka yetu ya Mapato *(TRA)*. Kuna maeneo ambayo tunaona hatukusanyi vizuri na ili tuweze kutekeleza yote kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni lazima tuwe na fedha ambazo zinatosheleza kutekeleza miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja nimwombe Mheshimiwa Waziri, kila siku tumekuwa tukizungumza *he is a humble person.* Nimemwambia kule Loliondo tunahitaji Kituo cha Forodha eneo la Olaika, Ololosokwani ambapo wananchi wanatoka kilometa 500 mpaka Namanga ndiyo wakapate huduma. Wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro na unavyojua sisi hatuna barabara ya lami ni Wilaya ya Ngorongoro tu ndiyo bado hatujaunganishwa na Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *imagine* mtu anatoka Waso – Loliondo mpaka Namanga kilometa 501.5 kwa ajili ya kufuata huduma. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nimwombe *TRA* walishafanya upembuzi yakinifu mwaka 2016, wameweka mpaka miundombinu ya maji, lakini mpaka leo hawajajenga, nimwombe sana atafute fedha popote atejengee kituo cha forodha. Wananchi wa Ngorongoro watamshukuru na watamshukuru Mheshimiwa Rais kwa yote ambayo wanatenda pamoja na hicho kituo cha forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Wilaya yetu ya Ngorongoro bado hatujaunganishwa na Mkoa wa Arusha. Ukijaribu kuangalia wilaya zingine zote saba zimeunganishwa kwa lami na mkoa, lakini sisi hatujaunganishwa. Tunahitaji na ukijaribu kwenda kule kwetu usafiri ni wa shida. Hata leo Mawaziri ukiwaambia njooni Ngorongoro, ukimwambia atatembea kilometa 300 *rough road* anaanza kufikiria hapo kweli nitarudi salama? Naomba basi na sisi watukumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu wa Rais aliagiza kwamba kilometa 39 kutoka Ngaresero mpaka Engaruka ziingizwe kwenye bajeti, zimeingizwa. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akiona tu Barabara ya Loliondo kwa ajili ya lami naomba apitishe usiku hata asisubiri asubuhi kwa sababu wale wananchi wanateseka.

Unaambiwa sisi tuna gari moja ya Loliondo *Coach,* ndiyo inatoka Arusha kila siku kwenda Loliondo, kwa sababu magari mengine yakija, kesho yake hayawezi kurudi kwa sababu ya miundombinu iliyopo. Kukodisha gari kutoka Arusha mpaka Loliondo kwa ajili ya huduma ya wananchi na biashara wananchi wanashindwa kufanya biashara na kuboresha maisha yao kwa sababu ya ughali wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata barabara hii itatusaidia na sisi kuongeza uchumi wa wilaya yetu na huku pia tukijua kwamba barabara ile kutoka Kigongoni kupita Oldonyo Lengai mpaka Loliondo ndiyo watapita watalii wataenda mpaka Serengeti. Kwa hiyo niwaombe sana Serikali, tujaribu kuangalia namna tuharakishe barabara ile, tuweke hata kwenye mpango wa *EPC+F,* itatusaidia kuboresha maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Wilaya ya Ngorongoro tuna kata 28, lakini mpaka leo tuna vituo vya afya sita tu, zahanati tunazo 31 kati ya vijiji 62. Tulikuwa na huduma na *fly medical service, TCIAA* wanasema kwamba ni lazima wasajiliwe nchini, *SMS* wameweza kufanya kazi kwa miaka 40. Leo Wilaya ya Ngorongoro vifo vya akinamama na watoto vimeongezeka ghafla kwa sababu ndege ile ndiyo ilikuwa inawasaidia. Kwa hiyo nimwombe sana Waziri, wanasema lazima tulipe kodi, niombe washirikiane na Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Afya, wale watu tuwape kibali cha kutoa huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo mtu amekuja, amefanya kazi miaka 40, halafu leo unakuja kumkatisha kwamba tunataka ujisajili, tunataka ulipe kodi na anatoa huduma ambayo Serikali imeshindwa kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Shangai. Nilimtaja Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Husna Sekiboko wajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia hii nafasi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri Mheshimiwa Chande, lakini vilevile nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya na kuhakikisha ile miradi ambayo endelevu ya kutoka Awamu ya Tano kwenda katika Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Tunamwona muda wote yuko mbioni akihakikisha kuwa maeneo mbalimbali ambayo yana utata, yeye anakwenda kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaishukuru sana Serikali kwa ajili ya Mkoa wangu wa Lindi. Mkoa wa Lindi ni mkoa Tajiri, lakini ulikuwa nyuma hasa katika maendeleo kwa vile ulikuwa hauna miradi. Sasa nitaitaja miradi ambayo ni mikubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameipitisha katika mwaka huu. Mradi wa kwanza umesainiwa Mradi wa *LNG,* huu mradi ni mkubwa ambao unakwenda katika eneo la Likong'o katika Jimbo au Manispaa ya Lindi. Utaleta mafanikio makubwa katika nchi yetu, lakini ningeomba sana katika huu mradi Wabunge tuje tupewe taarifa nini kinaendelea katika *LNG?* Mafanikio ya *LNG,* lakini vilevile tunataka wananchi wetu kule wajue wanatuuliza maswali mengi ili kujua nini kinaendelea katika *LNG? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Waziri mwenye dhamana aje afanye semina na Wabunge, aende Lindi na Mkoa wa Lindi na Mtwara tuunganike tujue lini *LNG* inafanyika? Maendeleo yale yawazindue wananchi ili wajitambue katika suala la *local content* na miradi ya *corporate social responsibility* ili na wananchi wajiandae kibiashara kwenda na maeneo hayo. Tunahitaji mahitaji ya *smart city* kwa ajili ya wale wanaokuja kuwekeza wasije kwenda mikoa ya jirani kwa vile Lindi hatuna mahoteli ya kutosha. Tunaomba uwekezaji mkubwa wa mahoteli na maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi mkubwa vilevile ambao umezinduliwa mwaka huu Ikulu, Mradi wa Madini ya *Graphite* Ruangwa – Chilola. Huu ni mradi mkubwa na Lindi ambayo ilikuwa ya maskini, itakuwa ni Lindi ya matajiri. Ni mkoa ambao una ufanisi mkubwa katika madini. Ni matumaini yangu Wanalindi tumefika muda sasa hivi kuwa tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha hatutakuwa tena ni mikoa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa tatu, miaka nenda tulikuwa tunalia barabara Nangurukuru, Liwale, Masasi, mwaka huu wameshasaini tayari barabara ya lami na nina imani itatoa kero na uzia mkubwa na ambao tulikuwa nao kwa ajili ya barabara hizi ambazo zilikuwa hazipitiki. Ilikuwa Mbunge wa Liwale kipindi cha masika hawezi kwenda Liwale, lakini huu ukombozi wa kutupatia huo mradi mkubwa wa kupitisha barabara nasema Mwenyezi Mungu azidi kumbariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati juzi tulitembelea Arusha, tumepata taarifa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa *Royal Tour* imeleta mafanikio makubwa sana. Watalii wamejaa Arusha ila tuna changamoto hatuna hoteli. Tunaomba wawekezaji wakubwa, tunahitaji uwekezaji, hakuna kupinga uwekezaji. Uwekezaji uliokuwa umetukuka na mikataba mizuri ijenge mahoteli, hii *Royal Tour* ambayo tumeleta watalii wengi wapate mahali pa kukaa na kuweza kujisikia raha katika utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe *TANAPA* wajenge mahoteli, tuwaombe Ngorongoro wajenge mahoteli, wachukue mikopo wajenge hoteli kwa sababu sasa hivi watalii wanahangaika, wanakwenda kulala katika mahoteli ya chini kabisa na kwa kweli Arusha imefurika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa Bandari; sisi tunahitaji uwekezaji. Mikoa ambayo inazungukwa na bandari tunahitaji ufanisi mkubwa sana katika uwekezaji. Hizi changamoto wanazolalamikia wananchi kama sheria mbalimbali zifanyiwe marekebisho na ni matumaini yangu ushirikishwaji wa bandari na uwekezaji umeshirikisha Bunge, umeshirikisha Mashirika ya Dini,

Waziri Mkuu vilevile amekwenda kutoa ufafanuzi, sijawahi kuona eneo ambalo limeingia mradi limeshirikisha wananchi kama mradi huu. Nini faida yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kwanza *SGR* itafanya kazi, tutakuwa na mzigo wa kutosha ambapo reli hii tunayotengeneza itapata mzigo hapa kupitia huu Mradi wa Bandari. La pili, *TAZARA* ambayo imekuwa haina mzigo, mizigo itakayokuwa inakwenda Zambia itakuwa inapita katika reli ya *TAZARA*. Ni kitu ambacho ni kizuri, lakini kwa nini watu wanapiga kelele? Kuna maeneo matatu yana changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao ni *competitor,* hawakubaliani na huu mradi hata siku moja. *Competitors* kwa vile mizigo mingi ilikuwa inakwenda nchi za Jirani, hawatakubali Tanzania iweze kupata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mawakala, kuna mawakala wamo mle ndani ambao walikuwa wanafanya biashara ya kupitisha mizigo bila kufuata sheria. Anasema mzigo huu ni wa *transit,* anapiga mihuri humu njiani mote, lakini mzigo uko Dar es Salaam. Wale wanaona kabisa katika kuleta ufanisi huu, katika uwekezaji na wao watapata changamoto na ulaji wao utakuwa haufanikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira katika bandari zetu za Mtwara na Tanga. Mkoa wa Mtwara ile bandari ilishasimama kwa muda mrefu. Ni imani yangu uwekezaji huu, utafufua uchumi katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Mzigo ambao unatoka Zambia, unaotoka Malawi, badala ya kuja Dar es Salaam utakatisha Makambako kuja Lindi, kuja Mtwara. Kwa kweli sisi hatuna cha kusema zaidi ya kusema, yale ambayo yanatakiwa kufanyiwa marekebisho yafanyiwe marekebisho na ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Rais anawapenda wanawake, anawapenda Watanzania, hathubutu kufanya kitu ambacho hakitaweza kumfanya yeye apate nanii, mama ni mlezi, wakati wote mwanamke ni mlezi, hawezi mwanamke mwenye ulezi wake akataka kuiangamiza. Huu mradi naomba Mwenyezi Mungu

ausimamie na katika kuusimamia kwake, Watanzania tutakuja kufarijika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri, yeye ni Balozi wa watu wenye ulemavu, ametoa bilioni 1.0 kwa ajili ya kusaidia watu wenye ulemavu na kutuwekea Mfuko watu wenye ulemavu. Walemavu wanasema yeye ni Balozi wao na hawatamwangusha, tuna kila namna ya kusema ahsante kwa niaba ya walemavu wote Tanzania, nasema Mwenyezi Mungu azidi kumbariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida. Nilimtaja Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Husna Sekiboko ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi niweze kuchangaia katika bajeti iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa maombi. Ombi langu la kwanza niliuliza swali siku moja hapa ni kwa kiwango gani Mkoa wa Kagera unachangia kwenye Pato la Taifa, nilijibiwa kwamba tunachangia kwa asilimia 2.3 na swali langu la nyongeza nilisema hatutendewi haki kama Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kagera ina rasilimali za kutosha na inaweza ikachangia sana kwenye Pato la Taifa na sababu kwa nini haichanagii, Moja, hakuna viwanda lakini tunazo rasilimali za viwanda. Ni kazi sasa ya Serikali kuvutia wawekezaji kwa kuweka zile *pull factors,* kupunguza kodi kadha wa kadha lakini na masharti ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni miundombinu na ndiyo ninachotaka kuongea leo. Ninaiomba Wizara kwa namna ya pekee, tunaomba barabara ambayo inaenda Murongo kutokea Mugakorongo iweze kutengewa na kupatiwa fedha sasa wananchi walipwe fidia na barabara ianze kujengwa. Barabara ya pili ni barabara ya Omurushaka ambayo ni Bugene kuja Nkwenda kuja Kaisho mpaka Murongo. Tuweze kuunganisha hizi barabara mbili tuweze ku – *boost* uchumi wa Mkoa wa Kagera na sisi tutafurahi kupitia kahawa, kupitia mahindi, kupitia mazao yote ambayo kama Mkoa tunazalisha, tuweze kuchangia hata asilimia 10 kwenye pato la Taifa. Uwezo huo tunao, tuna misimu ya mvua miwili na mambo kadha wa kadha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nitaongelea. Tunaongelea bajeti leo ambayo ni ya trilioni 44 *point something,* lakini ukiangalia ile bajeti ya trilioni 44 *point something,* bajeti ya fedha za maendeleo imeshuka. Ukiangalia bajeti ya trilioni 41 fedha ya maendeleo ilikuwa juu kidogo ilikuwa ni trilioni 15 lakini leo tuna bajeti ya trilioni 44 lakini fedha za maendeleo zinakuja kwenye trilioni 14. Unaona kwamba kuna kushuka, sasa hatuwezi kuji–*confine* kwenye kutumia ni lazima tuji–*confine* kwenye kuendeleza vitu tulivyonavyo, kujenga barabara na vitu kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunchopaswa kufanya ni kuanza kama siyo kufunga mkanda basi ni kuongeza *tax base* na hilo ndiyo nataka nilitoe. Bajeti ya sasa inaonesha kwamba asilimia 68 itaenda kwenye matumizi, hiyo nadhani haiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho wengi wameeleza na mimi nieleze, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana, lakini katika kumpongeza Mheshimiwa Rais ni *task* kwenu. Alichokifanya Mheshimiwa Rais ndio alichokifanya Yesu siku ya Alhamisi Kuu aliwanawisha miguu Mitume baada ya ya kuwanawisha miguu wakasema nenda fanya na kwa wengine. Rais alivyozindua *Royal Tour* hakumaanisha yeye aendelee kuandaa *Royal Tour* na kufanya *films.* Alitaka ninyi wasaidizi wake nendeni mfanye kama

alivyofanya yeye, amefanya mara moja ameweza ku-*boost* sekta ya utalii zaidi ya asilimia 109 kwa utalii wa ndani, lakini pia na utalii wa nje umekua kwa zaidi ya asilimia 59. Ninyi ambao mmeoneshwa ninyi mitume mmefanya nini? Hilo ni swali kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ninalolileta kwenu. Bado tuna nafasi ya kufanya kwa ajili ya kuongeza, mimi lengo langu ni tuweze kukusanya zaidi. Nimesikitika Halmashauri zetu zaidi ya 180 kushindwa kukusanya hata trilioni moja. Leo *projection* imeonesha twende mpaka trilioni moja *point something,* lakini kwa Halmashauri nyingi tulizonazo kushindwa kukusanya trilioni moja siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana na ukweli ni kwamba hela inapatikana kwa watu masikini lakini fedha inavuja. Mheshimiwa Waziri umeeleza Mama Samia, Mama yetu hapendi rushwa na ameagiza watu wale waliohusika kwenye ufisadi washughulikiwe. Tunataka taarifa kamili watu wote waliohusika kwenye Halmashauri kutorosha fedha mbichi, kutorosha fedha za hao walipakodi, wameweza kushughulikiwa kwa kiwango gani ili tuweze kupunguza kukopa? Hilo ndilo nalileta kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo yafuatayo: -

Kwanza; kama Wizara au Serikali lazima m–*build trust* kwa walipa kodi. Siyo ku–*build trust* lakini m–*prove* kwamba kodi mnazokusanya zinatumika sawasawa. Huo ndio ushauri wangu wa kwanza. Kwa kuziba mianya yote ya kodi.

Pili; ni lazima tuwe na mfumo wa ukusanyaji kodi ambao ni rahisi na rafiki kwa kila mtu.

Tatu; ni lazima twende kwenye *digital* kwenye kukusanya mapato. Tumeongelea suala la *TAUSI* kwenye Halmasahuri, ni kwa kiwango gani halmashauri zimekuwa zikitumia Mfumo wa TAUSI katika kukusanya mapato. Tumeendelea na mifumo ambayo ni *manual* inaruhusu watu kuendelea kuchezea mapato ya Serikali, siyo sawa. *(Makofi)*

Nne; ni lazima tuongeze *tax base*. Huu mfumo ambao nimekuwa nikieleza mara nyingi wa 28 *rules* inasababisha watu wakwepe kulipoa kodi. Moja, walipakodi ni wachache na wanapaswa kutoa mzigo mkubwa, kwa hiyo lazima watakwepa. Tutengeneze mfumo ambao katikati walipakodi ni wengi. Walipakodi wawe wengi na kodi zitakuwa nyingi lakini hapo hapo tuondoe mianya ya usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna changamoto ya *compliance* kwa sababu ya ugumu. Tuliongelea *blue print* hapa kwa nini hamjaleta *blue print* ili tuweze kupunguza urasimu, usumbufu katika ufanyaji wa biashara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni machache nakushukuru, muda ni mchache sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest, nilimtaja Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mheshimiwa Asha Juma ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia mchana wa leo. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutubariki sote kupata nafasi ya kuongea siku hii ya leo. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa bajeti nzuri sana ambayo imewasilishwa kwetu na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu bajeti ambayo umewasilisha kwetu, imeleta matumaini makubwa na tunaamini katika mwaka huu wa fedha, kuelekea hata 2025 mambo ya Chama cha Mapinduzi yatakuwa barabara, kwa nini? Kwa sababu bajeti imejielekeza zaidi katika kutatua kero na changamoto za wananchi, kwa nini? Kwa sababu bajeti ambayo umewasilisha inakwenda kupunguza mzigo wa maisha kwa akina mama masikini waliokuwa wanasomesha watoto wao kwenye elimu ya kati kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliwahi kuishi Mtume Mohammad *S.A.W* katika maisha yake aliyowahi kuishi zama hizo na maswahaba wenzake. Maswahaba wakawa wanamuuliza, walikuwa wakimuona kila muda anatembea na tasbihi anamuomba Mwenyezi Mungu *maghfilla* amsamehe, lakini yeye tunaamini katika sisi waislamu ndio kiongozi ambaye ni mwema zaidi katika sisi wanadamu wa kiislamu. Kwamba ni kiongozi wetu katika dini. Wao waliamini ni katika yule ambaye hana makosa, hana dhambi, ni mtu mwema mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini muda wote alitembea na tasbihi na kuomba *maghilla Eh!* Mwenyezi Mungu nisamehe. Wakamuhoji wewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tunajua wewe unaswali unafunga, unafanya sadaka unafanya kila jema ambalo Mwenyezi Mungu ameamrisha lakini mbona muda wote wewe *astaghfirullah* inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtume Mohammad *S.A.W* akawajibu maswahaba kwamba, bora ni yule anayemjua na kumwabudu Mwenyezi Mungu, bora siyo huyo unayemuona kwamba wewe ni kiongozi wetu lakini yule anayemuogopa mwenyezi Mungu ndio bora. Lakini akasema Mungu tunaemuabudu anapenda kutajwa sana, anapenda kuimbwa, kuombwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie tumpe sifa anayostahili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yeye hana sifa ya Mungu kwamba anapenda kusemwa sana, lakini yeye anastahili kusemwa sana kwa nini? Kwa sababu ya yale mema mazuri ambayo anayafanya katika Taifa letu. Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha, na hapa ninukuu maelezo aliyokuwa ametangulia kusema Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, amezungumza vizuri sana, ame-*narrate* vizuri kazi kubwa ambayo inafanyika kwenye Wizara ya fedha. Lakini nataka niseme wewe ni katika watu pia ambao wanastahili kusemwa vizuri, siyo kwa sababu unapenda kusemwa lakini unastahili kwa yale mazuri ambayo unayoedelea kuyafanya katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesema hapo mwanzo Mungu alisema yeye anapenda sana kuombwa na hivyo hata viongozi wetu wa kidunia msichoke, mpende kuombwa na mimi nakuja sasa kwenye ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi Serikali imefanya *allocation* ya wanafunzi kwenda kidato cha tano katika mashule yetu. Jambo la kusikitisha kweli kweli wapo wanafunzi wenye ufaulu mzuri sana *division two,* wamekosa nafasi za kwenda kusoma *boarding* wamekosa nafasi ya kwenda kidato cha tano hata *day*. Nina mfano wa wanafunzi ambao nimeletewa, lakini nina mwanafunzi hapa ana *division two* ya *point* 21 ana *C* ya *Chemistry*, ana *C* ya *Biology,* ana *C* ya masomo mengi na *combination* zaidi ya mbili zime – *balance,* amekosa shule. Nimefanya *consultation* kwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Nimezungumza na Naibu Waziri wa Elimu, nimeongea na Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI maelezo ninayopewa hakuna nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kosa lake yeye ni nini? Kufaulu kupata *division two* ya *point* 21 ndiyo kosa lake? Kosa lake ni nini mwanafunzi wa namna hii? Tunapotaka kutengeneza nchi ambayo ina elimu tutakayotaka kuifanya iwe chachu ya kuchachuza uchumi wa nchi hii, lazima tuheshimu maono maombi na fikra za watoto wanazoziweka kwenye malengo yao ya kupata elimu. Mtoto amefaulu vizuri amekosa nafasi ya kwenda shule, je, kosa la kwake ni lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikizingatiwa mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan anatoa elimu bure kwa kidato cha tano na cha sita. Huyu mtoto wa masikini mama yake anachoma vitumbua, anauza magimbi mtaani, amekosa nafasi ya kupeleka mwanae shule. Mwanae aliyefaulu kwa *division two,* tunamuweka katika kundi gani? Ninaiomba sana Serikali itoe maelekezo mahsusi kwa watoto ambao wamefaulu vizuri, watoto ambao wanastahili kwenda kidato cha tano kwa mwaka huu watafutiwe nafasi waende, kwa sababu ukimpeleka mtoto huyo kwenye chuo cha kati, siyo lengo lake na nina mfano wa mtoto mwingine ambae amepangiwa Chuo cha Uhasibu Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umewasha *mic* lakini nirihusu nimalizie. Mtoto amepangiwa Chuo cha Uhasinu Arusha ana *F* ya hesabu, hajawahi kusoma masomo ya biashara, alifaulu masomo ya *arts* na masomo ya sayansi. Je, unampeleka kwenye *accounts,* kwenye chuo cha biashara unategemea akafanye muujiza gani? Je, ule mtaala mpya tunaopigia chapuo humu ndani kwamba tuende kwenye mtaala mpya wa elimu. Je, kama tutawapeleka watoto kwa mtindo huu, amesoma amasomo haya, *interest* yake ni kusoma kitu hiki wewe umempeleka kitu kingine tofauti. Tunategemea nini kwenye Taifa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema ni vyema tukaheshimu maono na maombi ya wanafunzi, kwa sababu kila wanavyomaliza shule huwa wanajaza fomu kipaumbele chake ni kwenda wapi, anapojaza anataka kwenda kidato cha tano. Mtoto apelekwe akasome ili tuweze kuendeleza vipaji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atamalizia Mheshimiwa Zahor Mohammed.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu alienijaalia uzima na afya leo kusimama hapa kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi ya mwanzo kabisa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyosimamia utekelezaji kwa umahiri, uhodari, uadilifu na weledi. Nchi inakwenda vyema na imetulia na ninaomba kwa kupitia hadhara hii niwalaani sana wale ambao wanabeza juhudi zake na ambao wanataka kuleta utengano katika nchi yetu hii Tanzania ambayo ilikuwa imara. Hawa watu nawaombea Mungu walegee sehemu zote na wapotee kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuunge mkono Mama yetu naomba sana hawa watu wanaofanya ufukunyuku wa kuleta maneno kubeza jitihada za Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan walegee sehemu zote na wapotee kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu amefanya mambo mengi katika nyanja mbalimbali na tunayaona. Amejikita vizuri kwenye miradi ya kimkakati na kwenye masuala ya kiuchumi na kabla sijaendelea mbele baada ya kutoa pongezi nyingi kwa Rais, nampongeza sana Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake. Dkt. Mwigulu wewe ni Mchumi mahiri, ni mchumi thabiti, ni mchumi hodari wewe ni mchumi mchuma. Mwigulu ni mchumi mchuma. Kazi zako unazofanya kumsaidia Mheshimiwa Rais ni kubwa sana na zinaonekana na mara hii umethubutu kuleta bajeti hii ya karibu trilioni 44.1 ambayo imekuwa ni bajeti elekezi, inayohusisha zaidi uzalishaji na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii mimi nataka nijikite kwanza kwenye sehemu ya kilimo. Bajeti ya kilimo imeweza kutoka kwenye 294 mwaka wa fedha 2021 mpaka 970.0 mwaka huu wa fedha. Hizi ni fedha nyingi sana zinazoweza kuleta mageuzi makubwa katika sekta hii. Kwa kuwa, uchumi wa nchi unategemea sana kilimo, basi ningependa kutoa nafasi hii kujielekeza zaidi katika kilimo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo kinchukua nafasi kubwa, kilimo ni biashara, kinategemewa na wengi na kinaweza kuondoa Taifa letu hili kutoka sehemu hii kuipeleka sehemu kubwa zaidi. Nasisitiza kwamba iko haja ya kutilia mkazo zaidi kilimo hai, kwa kuwa kinaweza kuongeza ajira hasa kwa vijana. Mfano kuwapa nafasi ya kutengeneza viuatilifu vinavyotokana na mimea asili ambayo tunayo kwa wingi, kuanzisha kuliko kutumia kemikali za kutoka nje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na wakulima wataweza kutengeneza mbolea hai, viuatilifu hai, ikiwa ni sehemu ya kutengeneza ajira kwa vijana. Pia sehemu ya kupunguza gharama kwa Serikali kwa kuagiza kemikali kutoka kwenye makampuni ya nje. Nashauri Serikali waone fursa ya kuongeza

kipato cha uchumi wa nchi hii kwa kupitia kilimo hai. Kidogo kidogo tunapendekeza Serikali ipange na iipe kipaumbele kilimo hai kama yanavyofanya mataifa mengine. Kilimo kina uwezo wa kuchangia fedha nyingi na hivyo kubadili hali za wakulima. Serikali Kuu inaweza kuchangia wakulima kwa kuweka kabisa bajeti maalum kuchangia wakulima kuondokana na kilimo cha kemikali. Mfano, *USA* inatenga bajeti maalum kwa ajili ya kilimo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni kupanua na kuongeza uzalishaji wa mbegu asili za mazao ambayo yanaonekana kupotea. Serikali ijikite kusimamia uzalishaji wa mazo kwa *blocks,* siyo kila mahali mtu analima, mwenye korosho nchi nzima, leo umeambiwa alizeti itapanda bei unalima, kesho alizeti inaanguka bei. Kwa hivyo, Serikali ijikite vizuri kusimamia mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo nataka kulisimamia kwa muda wa haraka ni kwamba Serikali naipongeza sana kwa hatua zake za kuondoa ada ya elimu kutoka darasa la kwanza hadi *form six* na kwa sekta hii kwa kutambua jambo hili na umuhimu wa vijana hawa kupata elimu bila kikwazo sasa hapa naomba maua mama apewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa shilingi trilioni 1.44 kwa wanafunzi wa elimu ya juu, hii ni kujenga *base* nzuri ya kutengeneza wataalam ambao watakuja kusaidia nchi yetu kuipeleka mbele. Vilevile ni kuondoa ada, jambo zuri jingine la kuondoa ada vyuo vya ufundi. Hili jambo tunalipongeza sana, lakini tunaomba ada hii iondolewe kwa vyuo vyote vinavyofanya *study* hii ya kiufundi isiwe kwa vile ambavyo Serikali peke yake imeweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine nataka kuiomba Serikali ifikirie ni kupunguza tozo kwenye saruji ya kujengea, kwa kuwa hapa wananchi wa kipato cha chini wengi sasa hivi wamehamasika kujenga nyumba bora ambazo zinatumia *cement,* sasa kuwaongezea hii inakuwa kuwakwamisha. Kwa hivyo Serikali itafute *tax base* nyingine ya kuweza kupata hii fidia ili bei ya saruji isipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kusema kwamba kodi ni lazima kwa sababu kodi inaendesha nchi yetu, lakini tujitahidi tuweze kulipa kodi kama inavyotarajiwa lakini ulipaji na uhamasishaji kwa mamlaka uwe wa kirafiki zaidi, siyo kuendeshana mbio mpaka tena Waziri Mkuu aende Kariakoo akaeleze, akatulize hali. Jambo lile halipendezi sana. Kwa mamlaka ya kodi ijipange vizuri kuwa na lugha rahisi na kuwawezesha watu kulipa kodi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuomba mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja mchangiaji wa mwisho Mheshimiwa Zahor Mohammed.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya upendeleo. Mimi ningeomba kuchangia mambo machache ili kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi yake kubwa ya kuendelea kulitumikia Taifa, na kwa kazi yake kubwa ya kuendelea kutafuta vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Ni kazi kubwa, ngumu, inahitaji ujasiri, uimara na umakini wa ku-*focus* wapi Tanzania iende. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wasaidizi wake wawili ambao kwa kweli ili nchi yetu iendelee inahitaji vijana makini ambao kwa kweli watatusaidia na watalisaidia Taifa kwa kufanya kazi chini ya mama ili kuhakikisha kwamba nchi inaendelea. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako wote. Hakika mnafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwatie moyo, kwa sababu, kama Taifa linahitaji kusonga mbele; na ili Taifa lisonge mbele lazima tuwe na vyanzo vya mapato kutoka maeneo mbalimbali ambavyo vitalisaidia Taifa, ili kuweza kutimiza mahitaji

ya Watanzania. Moja kati ya hayo, mlituletea hapa Muswada na tukaupitisha kwa ajili ya kuiunga mkono Serikali ili iendelee kutafuta wawekezaji. Naomba sana kwenye hili msirudi nyuma kwa sababu tunafanya uwekezaji mkubwa ikiwemo kujenga *SGR,* na kufufua reli zetu zote pamoja na reli ya *TAZARA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* kama hesabu zangu zinaniambia sawasawa, wametuambia inahitaji mzigo wa tani milioni 25 kwa mwaka, leo tuna uwezo wa chini ya tani milioni 20. Kwa hiyo, tuna *SGR,* tuna Reli ya Kati, tuna *TAZARA,* tuna reli nyingine na Barabara. Zote hizi zinahitaji mizigo. Sasa kama tunahitaji kuendelea, lazima tuwaunge mkono wenzetu ili waweze kutafuta mizigo zaidi ili Serikali iweze kuwahudumia wananchi. Naomba hapa msivunjike moyo, kwa sababu ili tuweze kuwahudumia wananchi ni lazima tutekeleze au tutimize ahadi zetu kama Serikali ambayo inasimamiwa na Chama cha Mapinduzi, msirudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kelele za mlango huwa hazimzuii mwenye nyumba kulala. Tuendelee kuchapa kazi kwa sababu ndio wajibu wetu. Tumeaminiwa na wananchi, tuhakikishe kwamba lazima tunawahudumia. Ndiyo Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, tuendelee ku-*stick on the game. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba univumilie, mimi nina kawaida ya kusoma hiki kitabu, maana ndiyo nilichokikuta. Naomba ninukuu Katiba yako hii ya mwaka 1977 ya Jamhuri ya Muungano, kwenye Sura ya Kwanza ile inasema: "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano," lakini kifungu cha pili inasema: "Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo la Tanzania Bara na eneo la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya Bahari ambayo Tanzania inapakananayo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa naomba kutoa angalizo, hasa kwa wenzetu wote, wale ambao wanadhani kwamba chama chetu na Serikali yetu haishughuliki na matatizo ya Watanzania. Ni kweli Katiba hii imetoa nafasi ya kutoa maoni, nafasi ya vyama vingi, lakini haikutoa nafasi ya kuvunjiana heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuwakumbusha wenzetu, sisi wa umri wetu, kwa mujibu wa *data* zilizopo, zaidi ya asilimia 70 ni vijana ambao wako chini ya miaka 50. Maana yake tunachokijua ni Katiba hii ni ya Tanzania, ndicho tunachokifahamu. Kwa hiyo, wenzetu msitengeneze maneno ya kuligawa Taifa hili. Taifa hili limepiganiwa na Taifa hili linaitwa Taifa la Tanzania. Hakuna Mtanzania nusu, wala hakuna Mtanzania kipande, msituvuruge. Nawaombeni sana, wala msimvunje moyo mama kwa sababu analihudumia Taifa. Analihudumia kama Mtanzania mwenye haki kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna mmoja anadhani yeye ni Mtanzania zaidi kuliko mwingine, ajitathmini. Kwa sababu haiwezekani, Katiba hii imetupa haki sawa sote kama Watanzania. Kwa hiyo, asijitokeze mmoja kwa sababu ya ulevi, kwa sababu ya kulewa madaraka, akadhani yeye ana haki zaidi kuliko mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo haki zote kama Watanzania. Kwa hiyo, nawaomba sana, tuheshimu matakwa ya Katiba hii, na pia tuheshimu haki ya kila Mtanzania. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, jitihada zinazofanyika zinafanyika ili kutuondoa Tanzania tulipo ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana mama yetu ambaye ni Rais wetu, mama usivunjike moyo. Tulikuahidi hapa, tunakuunga mkono, tutaendelea kukuunga mkono kwa sababu dhamira yako tunaielewa sisi watoto wako kwamba ni kuiongoza Tanzania ili iweze kupiga hatua. Shika kamba, endelea, tunakuunga mkono. Sisi vijana wako, Wabunge wenzako, tuko pamoja na wewe kuendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuliko yote naomba sana hili tulizingatie kwa sababu sisi kama Watanzania hatuna Taifa lingine. Sisi kama Watanzania tunao wajibu wa kulilinda Taifa hili ili vizazi vyetu vije kurithi Tanzania iliyo bora kuliko iliyo leo. Kwa hiyo, tusiwavunje moyo. Wale wanasiasa wenzetu ambao wanajifunza kufanya siasa, kwa sababu, wako vijana wanajifunza kufanya siasa, siasa siyo kuwadanganya watu, siasa ni kutekeleza

matumaini ya watu kwa kutumia vyanzo vilivyopo ili kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tujiheshimu, tuheshimu Katiba, tuheshimu viongozi wetu, na pia tuwape nguvu ili waweze kufanya kazi ya kulihudumia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naiunga mkono sana bajeti hii. Asanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor Mohammed kwa kuwa mchangiaji wa mwisho kwa asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu mchana huu umekwisha. Kuna angalizo moja tu; kna baadhi ya Wabunge wachache ambao katika michango yao wamekuwa wakitaja kushika shilingi, sasa naomba tu niwakumbushe kwamba kwenye Bajeti Kuu hakuna kifungu cha kushika shilingi. Turudi kwenye Kanuni ya 126 mtaona kwamba Bajeti Kuu ni kupiga kura za wazi kwa kutajwa Mbunge mmoja jina lake. Kwa hiyo, kila mmoja atakuwa anapiga kura kwa namna hiyo. Kule kwenye vifungu vya kushika mshahara, kwenye Wizara, tumemalizananao. Kwa hiyo, naomba nikumbushe hilo tu.

Pia angalizo la pili ni kwamba jamani siku za mwanzo za michango tujitokeze kwa wingi. Sasa mnaona mwisho wa siku tunamaliza na watu wanakuwa wengi zaidi na muda unakuwa ni mchache. Kwa hiyo, mara nyingine basi tujitahidi pale siku ya mwanzo, ya pili na ya tatu tuwe kwa wingi ili tusipoteze wakati wetu.

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo dogo la wageni hapa, naomba nimalizie.

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni sita wa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Hombolo kutoka Hanang, Mkoa wa Manyara, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. Naona hawakupata fursa ya kuingia. *(Makofi)*

Kuna wageni sita wa Mheshimiwa Hamisi Taletale kutoka Jijini Dar es Salaam, wale pale, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Kuna wageni 54 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni wanakwaya kuu kutoka Kanisa la KKKT, Usharika wa *Arusha Road* na Kwaya ya Kanisa la KKKT Usharika wa Mkimbizi, Dayosisi ya Iringa, Jimbo la Kaskazini, karibuni sana wanakwaya wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni 150 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo kutoka Haradali Shule ya Awali na Msingi ya Jijini Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna wageni 46 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kutoka Chuo Kikuu cha Mt. Augustino cha Jijini Mwanza, karibuni sana wageni wetu kutoka Mwanza. *(Makofi)*

Kuna wageni 31 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni wanakwaya wa KKKT Usharika wa Mudio, Hai. Hawakupata fursa ya kuingia, nafikiri. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Zacharia Issaay kutoka Mbulu Mjini, karibuni sana wageni wetu kutoka huko Mbulu; na vile vile tuna mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete, Kada wa CCM kutoka Tarime, Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho ajiandae.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge hii Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kufika hapa leo nikiwa hai, salama salmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, na wasaidizi wake pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Imeweza kusimamia vyema kabisa na tunaona mambo yakiwa yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia katika sehemu mbili tatu, lakini nianze kwenye upande wa afya. Tumeona ambavyo bajeti imeongezeka kwenye Wizara ya Afya, lakini tumeona jinsi ambavyo Serikali yetu imeweza kuongeza vituo vya afya, hospitali pamoja na zahanati kwa wingi sana. Hatuna budi

kupongeza hilo, hatuna budi pia kuchangia au kutoa mawazo yetu kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tuna vituo vya afya vingi sana, pia tuna zahanati nyingi pamoja na hospitali. Lakini tuseme ukweli, huduma za afya bado hazijatengamaa, hazijawa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge atakayekuwa anachangia humu ndani atakuwa anajua na atakuwa anajua changamoto ya jimboni kwake. Kikubwa zaidi watumishi wa afya kwenye hospitali zetu au kwenye zahanati zetu bado ni hafifu, japo Serikali imeajiri lakini bado. Ni lazima Serikali itupe jicho la tatu kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia dawa bado ni changamoto, wananchi wetu tunawahamasisha wakate bima za afya lakini dawa bado ni changamoto. Lakini vifaa tiba bado ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikumbushe tena, ni mara yangu ya pili nachangia kwenye Bunge hili, niliwahi kusema Jimbo langu la Ulanga kuna changamoto kubwa ya afya kwa sababu hospitali ya wilaya imekuwa ndogo, lakini pia ongezeko la watu limekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kupata wawekezaji wengi kwenye Jimbo la Ulanga. Leo tutashindwa kuhudumia kwenye sekta ya afya, waende kwenye wilaya nyingine au waende mkoani kwenda kutibiwa, tutaonekana kwamba sisi pia hatuko *serious.* Kwa hiyo, naomba mlichukue hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana baada ya Bunge hili kuisha, ningependa sana Waziri wa afya aje jimboni ili aje kujionea haya ambayo nazungumza. Leo ni mara ya pili au ya tatu nazungumza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini; kuna maamuzi yalitoka ya kuhamishia biashara ya tanzanite kwenda kufanyika

Mererani. Niseme ukweli kabisa maamuzi yale hayakuwa sahihi, na mtu mzima akivuliwa nguo huchutama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruhusuni biashara ya tanzanite ifanye Watanzania wale mazao ya nchi yao. Maamuzi yale yalikuwa yanakwenda kuwanufaisha watu wachache sana, na wengi wao siyo Watanzania. Leo hii unakwenda kuacha biashara ikafanyike sehemu moja wanufaike watu wachache na wakati sekta hii imeajiri zaidi ya watu milioni sita kwenye nchi nzima. Iruhusuni biashara ya tanzanite ifanyike kwa uhuru ili watu wale matunda ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nichangia kwenye upande wa leseni zetu za *brokers;* kama ambavyo nimesema, nchi hii imewaajiri watu zaidi ya milioni sita kwenye sekta ya madini, lakini leo hii ukienda kwenye upande wa ma-*broker,* tunajua ni wale watu wa kati ambao huwa hawana mitaji – wameweka leseni ni dola 100, watu wale hawawezi, hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye tu mahesabu kama Wahindi. Mhindi anaweka faida ya shilingi 100 anauza bidhaa zake 200 kwa siku, sisi tunalazimisha hapa tunaweka faida ya shilingi 300 unauza bidhaa 10 kwa siku. Ni mahesabu madogo hayahitaji hata *degree*. Punguzeni bei ya leseni watu wakate leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka kwenye jimbo ambalo yanatoka madini. Unakuta wenye leseni kubwa wako 60, halafu ma-*broker* ambao ni wengi zaidi, wako chini ya 50. Maana yake ni kwamba anashindwa ku-*afford* kukata leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi unarudi upande wa *TRA* na wenyewe wanawakadiria kodi zaidi ya 400,000, 500,000 kwa mwaka; watu hawawezi kufanya biashara. Ukiwaangalia hata kula yao ya chakula cha mchana inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, nafikiri kama Mheshimiwa Waziri angekuwa ananisikia, angeweza kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba *TRA* wanaweka viwango ambavyo wananchi wale wanaweza ku-*afford* kufanya vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni zetu kutoka kwenye dola 100, wekeni hata dola 50, hata dola 30, watu wengi watakata leseni na tutapata faida, lengo ni kukusanya mapato. Ukikatisha watu wengi zaidi utapata hela, ukikatisha watu wachache utapata hela kidogo. Kwa hiyo, ni hesabu ambayo haihitaji *degree.* Ni watu tu kujipanga na kuweza kufanya mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninapenda kuchangia kwenye Wizara ya Ardhi. Kwenye mijadala hapa Wabunge wamepiga kelele sana kuhusu migogoro ya ardhi, naamini Serikali imechukua na inakwenda kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto kwenye upande wa uthamini. Ni kweli Mheshimiwa Rais kisheria anayo haki ya kuchukua ardhi ya mtu yeyote sehemu yoyote kwa manufaa ya Umma, kwa ajili ya maendelezo ya Umma. Lakini kuna taratibu ambazo zimewekwa juu ya ulipaji fidia za wale watu ambao wanataka kuhamishwa kwa ajili ya maendeleo ya Umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema kwamba ukiwa umekwenda kufanya fidia, umemaliza kufanya fidia kwa wananchi, inatakiwa kulipwa ndani ya miezi sita. Baada ya miezi sita *valuation* inakuwa ime-*expire*. Sasa ikisha-*expire* maana yake ni kwamba unatakiwa wewe umlipe fidia ya usumbufu yule mwananchi, yule mwananchi anakuwa halipwi fidia, baada ya muda, anakuja tena mtu yuleyule anataka kufanya tena *valuation* upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hajalipa fidia, mbaya zaidi haji na jedwali ambalo liko kwenye bei ya soko ya muda huo, anakuja na jedwali la mwaka 2015, leo mwaka 2023, mdizi uliuwa unauzwa shilingi 2,000, leo anataka kumfanyia *valuation* mwananchi yuleyule kwa bei ya shilingi 2,000, kitu ambacho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Leonard Chamuriho.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa kuniona na kunipatoa nafasi hii kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza ninapenda kuunga mkono hoja bajeti hii kwani ni bajeti ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kumpa pongezi Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea bajeti ya wananchi, kwani ni bajeti murua ambayo ukiangalia amefuta ada kwa kidato cha tano na sita, vilevile kwa vyuo vya ufundi ili tuweze kupata rasilimali watu nzuri kwa nafuu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ametoa mikopo kwa vyuo vya kati na anaendelea kutafuta rasilimali kwa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile *SGR,* Bwawa la Nyerere, na hivi karibuni ametutafutia wawekezaji wazuri katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake; Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande; Katibu Mkuu, Dkt. Natu Mwamba na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na timu nzima, kwa kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais kutuletea bajeti hii ambayo ni nzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ntajikita kwenye vifaa vya ujenzi ili kuona ni jinsi gani tutawezesha miundombinu hii ambayo Mheshimiwa Rais anaitolea pesa itakavyoweza kutusaidia ili tuweze kupata *value for money.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 107 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea vizuri kuhusu *cement* na jinsi ambavyo inalindwa pamoja na wafanyakazi wake. Lakini ninapenda kutoa mchango wangu kwa kuhakikisha kwamba hii

*cement* ili isipande bei ni nini ambacho tunatakiwa tukifanye kwenye uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hapa nina orodha ya viwanda 14 vya *cement* (saruji) kama ambavyo vimewasilishwa, na vilevile nimeangalia hotuba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambayo imeonesha kwamba jumla ya uwezo wa uzalishaji *(installed capacity)* ya viwanda vyetu hivi ni tani milioni 10.48. Lakini uzalishaji wa sasa hivi ni tani milioni 7.6, na matumizi kwa sasa hivi ni tani milioni 7.1. Kwa hiyo, tuna ziada kidogo ambayo inakwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia katika hiyo bajeti inasema kwamba bei ya *cement* imeonesha uhimilivu, kwani ina ongezeko la 0.5 tu. Sasa hii inabidi ilindwe ili tuweze kupata unafuu katika bei ya saruji tuweze kuendeleza miundombinu yetu ambayo tunaijenga kwa pesa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali ijikite katika kuhakikisha kwamba hii bei haipandi. Nini kifanyike; ukiangalia uwezo wa kuzalisha saruji na baadhi ya viwanda vyetu utagundua kwamba viwanda vikubwa vinazalisha chini sana ya uwezo wao. Ukiangalia kwa Mfano Kiwanda cha *Mbeya Cement,* kinazalisha asilimia 43 tu; ukiangalia *Dangote Cement,* anazalisha asilimia 54 tu. Kwa hiyo, hivi viwanda vikiongeza uzalishaji vitahakikisha kwamba *cement* (saruji) inakuwepo na haitapungua bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tumeona ukosefu wa saruji umesababisha bei kupanda, lakini hawa wawekezaji wakubwa kama watapandisha uzalishaji uendane na *installed capacity,* tunaweza kuhakikisha kwamba tunapata saruji ambayo itakuwa ina bei ambayo inaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulishuhudia huko nyuma kwamba viwanda hivi vikipanga matengenezo kwa pamoja vinasababisha uhaba wa saruji, kitu ambacho kinasababisha tena bei hiyo kuweza kupanda. Hivyo, tukiweza kuhakikisha kwamba hivi viwanda tunaviratibu vizuri ili vifanye matengenezo

yao makubwa, siyo kwa wakati mmoja ili uzalishaji usiathirike, basi tutahakikisha kwamba upatikanaji wa saruji unaendana vizuri na uwezo wa viwanda hivyo ili viweze ku-*maintain* hiyo bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kama Wizara husika itaangalia, kuna orodha ya kampuni ambazo tayari zimekwishajiandikisha hapa lakini bado viwanda vyao havifanyi kazi. Kama vitaanza kufanya kazi tutahakikisha kwamba saruji itapatikana na vilevile tutaweza kupata bidhaa hiyo kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye nondo unakuta kuna changamoto hiyohiyo. Ukurasa wa 144 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeongelea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeniwashia taa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kumalizia kwa kusema kwamba viwanda tuvijengee uwezo wa kuzalisha bidhaa hizi ndani ili tuweze kupunguza bei na miundombinu anayotafutia pesa Mheshimiwa Rais iweze kudumu. Ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Dkt. Chamuriho. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Nicodemas Maganga watamalizia kwa upande wa Wabunge.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. Wenzangu wamesema apewe maua yake, nami nasema Mheshimiwa Rais apewe maua yake, anafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu nzima ya wizara, mnafanya kazi nzuri, taarifa nzuri sana, kila unapoisoma unaona raha, kwa kweli *package* ni nzuri kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninayo machache ya kuchangia katika bajeti hii. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako umesema kabisa kwamba wastani wa watu waliochangia kodi ni asilimia 20 tu ndio waliochanga vizuri. Umesema kwamba walipa kodi waliosajiliwa ni 4,455, wenye *TIN* halali ni 4,400,000; wenye *TIN* halali ni milioni moja, hawa milioni moja wamechangia trilioni 16.7 kwa maana ya asilimia 80 ya mapato yetu, ambayo mwenyewe umesema kabisa mapato hayo yamepatikana na idadi ya wachangiaji wadogo sana, asilimia 20. Palepale ukasema kwamba katika maneno muhimu ya kuzingatia ni ukweli kabisa kwamba wastani wa walipa kodi siyo mzuri sana kwa sababu wanaolipa kodi ni wachache kwa hiyo wachache ndio wanachangia kodi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini; nataka kusema kwamba bado kuna kazi kubwa tunatakiwa kufanya ili tuweze kuongeza mapato, ili tuweze kuongeza hawa wachangiaji wa hii kodi yetu. Na hii inaweza kusaidiwa kwa kuendelea kuongeza vyanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia hapa mwaka jana, na leo nasema; bado tu sisi tunaotoka majimbo ya mpakani; Kakonko, Kibondo, bado tuna fursa ambayo haijatumika vizuri, fursa ya mipaka yetu. Bado masoko ya ujirani mwema yanafanyika kiholela, masoko ya ujirani mwema ni shamba la bibi kwa sababu uratibu haupo. Kila mtu pale ni afisa mkusanyaji mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba hapa kujengewa forodha ya pamoja ili tuwe na *TRA* pale, tuwe na polisi na *migration* ili biashara iweze kufanyika vizuri kwenye Soko langu la Mkarazi na Soko langu la Kibuye. Haya yote yameshindikana. Haya ni mapato ambayo yanapotea. Tungeweza kudhibiti haya mapato tusingeendea kukandamiza wananchi kwa kung'ang'ania

vyanzo vichache, lakini walipa kodi wachache ndio wanatuchangia Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nakuomba uje kwenye masoko yetu ya ujirani mwema. Kule Muhange, Mkarazi na Kibuye, tunaomba uje, kuna pesa kule, turatibu zile biashara za kwenye mipaka ili tuongeze walipa kodi na ili tuweze kuratibu hizi biashara za mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, tukiongeza walipa kodi hatutakuwa tunaongeza kodi kwenye vile vyanzo tunaona kwetu ni rahisi. Nimeona hapa tumeongeza tena kwenye mafuta na *cement,* ina maana tunatafuta urahisi wa kupata hii pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo ninavyoongea Jimbo la Muhambwe *cement* inauzwa 23,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 50. Sasa ninajiuliza hii kodi ikiongezeka kwenye *cement* wananchi wa Muhambwe tutajenga kweli? Mtu wa Dar es Salaam ananunua 14,000, tunaambiwa usafiri ndiyo unasababisha *cement* iwe 23,000 Kibondo. Sasa mafuta nayo yameongezeka, wananchi wa Muhambwe hii *cement* hawataweza kuinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ninawaomba, hebu tutoke nje ya boksi na wataalamu watusaidie, akili ichangamke kidogo, basi turatibu hii bei, bei iliyoko Dar es Salaam na bei iliyoko Kibondo iwe ileile ndiyo tuongeze hizi kodi. Lakini kama tunasema usafirishaji unasababisha *cement* iwe ghali basi tunaomba hii kodi ya *cement* itolewe. Maana yake mpaka sasa ni 23,000, kwa hiyo, itakuwa changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mafuta yatakwenda kuleta matatizo mengi; nauli itapanda, mazao yatapanda, kila kitu kitapanda. Kwa hiyo, ninaomba wataalamu wetu nao akili zao zijiongeze tunasema watoto wa mjini watafute vyanzo vingine ili tusiendelee kumkamua ng'ombe wa maziwa mmoja huyohuyo, atakufa maana yake atakamuliwa mno Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, vilevile niombe; ni hakika tunahitaji hizi pesa, hata natamani tuzipate kwa ajili ya kuratibu na kuharakisha miradi, maana yake tunayo miradi kwenye majimbo yetu ambayo kwa kweli kasi yake haifurahishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni tu miliona vibonzo vinapita vikionesha vumbi la Kibondo. Hata sisi watu wa Kibondo hatujisiki vizuri, tunatamani lile vumbi liishe. Tunaomba miradi yetu ya kimkakati ya barabara yetu ya kuunganisha Kasulu, Kibondo, barabara ya kuunganisha Kigoma, Tabora, zipelekewe pesa, wakandarasi walipwe pesa zao ili hizi barabara ziweze kuisha na sisi tusiwe vibonzo kwenye mitandao kwa ajili vumbi linaloendelea katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, miradi hii ya kimkakati inayojengwa katika Mkoa wa Kigoma inayo miradi ya *complementary* ambayo inategemea kujengwa Kasulu, Buhigwe na Kibondo. Barabara zipo asilimia 60, 70, 80, lakini miradi hii haijaanza kabisa. Tunaiomba Serikali miradi hii ianze, kwa sababu kama hizi barabara zitaisha halafu miradi haijafanyiwa chochote matokeo yake hii miradi itakwenda kupotea. Na sisi tulishawaambia wananchi wetu kwamba hii miradi ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niombe Mheshimiwa Waziri, bajeti ya mwaka 2021/2022 majimbo yote ya Mkoa wa Kigoma yalipewa milioni 150 kwa ajili ya kumalizia maboma ya zahanati, kasoro Jimbo la Muhambwe. Nimeshakwenda TAMISEMI zaidi ya mara nne, nimeshakwenda Wizara ya Fedha zaidi ya mara nne, naambiwa vifungu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa mlitupa ninyi na majimbo yote yamepewa. Afisa mipango vifungu anavitoa wapi? Nilishakwenda Kumkuyu nikafanya mkutano; Rukaya nikafanya mkutano, tena kwa kujinasibu jamani naleta milioni 50 ya zahanati, leo hii naambiwa vifungu ambavyo hizo pesa mmeleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri unavyokuja kuhitimisha hapa naomba milioni 150 yangu kama ambavyo majimbo mengine yamepewa ili na mimi niende

kutimiza zile ahadi ambazo niliwaahidi wananchi wa Jimbo la Muhambwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Tunaendelea na Mheshimiwa Nicodemas Maganga, tutamalizia na Neema Lugangira.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili na mimi niweze kuzungumza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbogwe Mkoani Geita ili niweze kuwasilisha mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuwasilisha mawazo ya wana Mbogwe. Kwa vile muda sio rafiki sana naomba niende haraka haraka, lakini ikikupendeza uniongeze kwa sababu ni mara ya pili tu toka Bunge lianze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu kuweza kuwasilisha mawazo ya wananchi. Namshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi anazozifanya kwenye Taifa letu la Tanzania. Najua nguzo kubwa sasa hivi ni mkataba, wananchi wangu wangependa nilielezee suala la mkataba ambalo linagonga kichwa, kila mtu anajiuliza ni nini hatima yake, lakini muda hautoshi. Niwaombe wananchi wangu wa Mbogwe ninakuja mwezi wa saba, tutakuja tufafanuliane na tuelimishane vizuri kuhusiana na hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwatoe wasiwasi, hakuna kitu cha kuharibika mbele ya Mama yetu ambaye ni Amiri Jeshi wetu Mkuu. Kwa hiyo Watanzania muwe na imani kabisa, kwamba nchi

iko salama, na bandari haijauzwa. Hayo maneno mnayoambiwa mitaani yapuuzeni, hakuna kitu kama hicho, wala kufikiria suala kama hilo. Na mimi mwakilishi wenu mliniamini na endeleeni kuniamini hivyo hivyo, na mimi ninasimama kwa ajili yenu kuhakikisha kwamba hakuna jambo la kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwako, Waziri wa Fedha. Kwanza nikupongeze sana kaka yangu, wewe ni Waziri wa Fedha, ni sekta ambayo ni ngumu kuliko Wizara zote, maana wewe ndiwe umeshikilia fedha. Nikuombee tu kwa Mwenyezi Mungu. Mawe unayopigwa endelea kuvumilia. Hata Yesu alipigwa, wengine walisema alikuwa mwizi wa mbao lakini ki ukweli alikuwa anaponya watu. Kwa hiyo na wewe simama kuhakikisha kwamba Taifa letu tunakwenda vizuri na tuweze kukidhi mahitaji ya watu wetu waliotuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri mambo mawili makubwa. Nimeona kwenye mpango huu Mheshimiwa Waziri amedhamiria kwenda kumwongezea mchimbaji asilimia mbili, naomba hiyo hebu aiache, maana itatuletea kero ambayo haitaisha tena; kwa sababu mpaka sasa hivi wanalipa *rate* ya asilimia saba lakini vile vile wachimbaji hawa wanakabiliwa na *service levy*, kwa hiyo ukiweka asilimia mbili tena itakuwa asilimia 9.3. Hii nikumwongezea mzigo mchimbaji na kumuumiza kumtoa barabarani na kusababisha utoroshwaji tena wa madini uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2017, lengo la kuweka asilimia saba lilikuwa kwamba ninyi Serikali mtajuana huko; nne itaenda madini tatu itaenda *TRA*. Kwa hiyo hata sasa hivi niwaombe Serikali, kwa kuwa ni wamoja kaeni kwa ajili ya kutupunguzia adha au balaa wale tunaoishi kwenye maeneo ya madini. Muwe mnagawana tu humo kwenye asilimia saba, mtakuwa mnajua wenyewe hii inaenda *TRA*, hii inaenda madini ili watu waendelee kuzalisha dhahabu na kuchimba na wao waweze kutoka kwenye wimbi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili napenda nikushauri Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la mafuta kuongezea tena

shilingi mia moja, na lenyewe mimi nisingependa iongezeke hiyo shilingi mia moja, itoe. Tunavyo vyanzo vingi vya mapato kwenye Taifa hili ikiwemo Sheria tuliyopitisha ya miamala, najua ni trilioni nyingi tu tutaingiza kama usimamizi ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile bandarini pale mpaka sasa hivi kuna wafanyabiashara tuna ushahidi kabisa hawatoi hata risiti. Weka usimamizi mzuri kwenye maduka hayo makubwa ya Kariakoo ili watu waweze kuchangia Pato la Taifa. Nina imani hauta-*fail* popote pale nakuomba sana kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kwa kuwa hii ni bajeti kuu nizungumzie upande wa maliasili. Ninalo pori pale Mkweni wananchi wangu wanakaa kwa kubanana. Kwenye ahadi zetu kwenye Ilani, tulifanya mikutano mingi tukawaaminisha watu kwamba tutatenga maeneo kwa ajili ya kuchungia ng'ombe. Nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atenge muda na siku aje anitembelee Wilayani Mbogwe aje alione hilo pori la Kigosi ambalo halina faida kabisa, maana hata wanyama walikwisha, sifa za kuwa pori ilikwishaisha, matokeo yake limekuwa pori la kusulubisha watu, kukamata watu wauza mikaa pamoja na watu wengine. Kwa hiyo niombe tutakapolimaliza Bunge hili Mheshimiwa Mchengerwa aje anitembelee kwenye Wilaya yangu ili kusudi tuangalia hayo maeneo tuweze kuwafungulia wananchi tuweze kuchungia maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse Wizara ya ujenzi. Tunazo barabara ambazo walitutengenezea kweli mwaka jana lakini mvua zimenyesha hizo barabara zimeharibika. Nakumbuka mwaka 2021 nilimuomba kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwamba kwenye bajeti zake hizi aniruhusu kwenye halmashauri yangu ninunue *caterpillar*. Nimeandika andiko maalum naomba ani-*support* kaka yangu kwenye Wizara yake ya Fedha, twende tukanunue *grader* ili barabara zinapokatika mvua zinaponyesha tuwe na uwezo wa kutengeneza barabara wenyewe kuliko kusubiria masuala ya bajeti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** … bao kuna matatizo makubwa kusubiria hizi bajeti, mvua zinaponyesha barabara zinakatika wananchi wanashindwa kupita, matokeo yake wanamuona Mbunge hafai, Rais hafai, chama hakifai lakini kumbe dhamira ni nzuri…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, ahsante sana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** …nitengee hii bajeti na andiko langu unipitishie Wizarani ili kusudi niweze kununua *caterpillar*. Baada ya kusema hayo machache na mengi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali, na nianze kwa kutambua na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kuinua uchumi wa Tanzania pamoja na uchumi wa mtu mmoja mmoja. Aidha, kipekee ningependa kumpongeza sana na kumtia moyo mchumi mbobezi kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba na Wizara yake nzima kwa kazi kubwa wanayofanya, na kazi yao tunaiona na kupitia bajeti hii tuna ona dhamira ya dhati kabisa ya kufanya uchumi wa Tanzania upae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia haraka haraka kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza, naishukuru sana Serikali kwa kuyafanyia kazi maoni ambayo sisi Wabunge tunatoa, maana nafahamu Serikali ilitambulisha kodi ya huduma za kidigitali na kampuni za nje kama *Facebook* yaani meta wameshaanza kuwasilisha taarifa zao Serikalini, nawapongeza

sana. Aidha, nawapongeza pia kwa uamuzi wa kuamua kutoza kodi kwa biashara za mitandao *(online businesses)* kwa maana halisi ya *online businesses* ambazo hazina maduka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe tu angalizo kuhusu kutoa kodi kwa hawa watu wanaoitwa *influencers.* Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, tuwe na *definition* sahihi ya *influencer* ni akina nani. Kwa sababu mathalani mimi naweza nikawa ni shabiki wako, nika-*post* kazi inayokuhusu wewe lakini utakuwa hujanilipa, mimi nimefanya tu kwa utashi wangu na kwa namna ambavyo ninakukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapa pia nimeona viongozi wengi pamoja na Wizara nyingi zimelipia kwenye Kampuni ya *Twitter* ili wapate *verification.* ambapo wanalipa gharama kwa dola nane mpaka kumi kwa mwezi. Sasa ningependa kufahamu pia Wizara ina mpango gani wa kupata kodi kupitia fedha inayolipwa *Twitter* kupitia viongozi wetu wa Serikali pamoja na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili; Serikali ilishaweka dhamira ya dhati ya kuona namna gani ambavyo tunainua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja hususan makundi maalum kupitia wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hii imefanyika kupitia sheria ya manunuzi, ya asilimia 30. Ningependa kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri nini ambacho anapanga kufanya ili kuhakikisha kwamba wanawake, vijana na makundi maalum wananufaika na asilimia 30 ya manunuzi ya umma kama ambavyo Sheria ya Manunuzi ya Umma imeelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho, dhamira ya dhati ya Serikali ni kuinua uchumi wa nchi yetu, na ili tufanye hivi ni lazima Serikali iweke jitihada za makusudi kabisa kuangalia mikoa ambayo inatambulika kama ina hali kubwa ya umaskini ilhali ni mikoa ambayo haipaswi kuwa katika nafasi hiyo. Hapa nitaongelea Mkoa wangu wa Kagera. Mkoa wa Kagera umepakana na nchi tatu, umepakana na Rwanda, Burundi na Uganda na unabeba asilimia kubwa ya Ziwa Victoria. Una hali

nzuri ya hewa, una ardhi yenye rutuba, unapata mvua misimu miwili na zaidi kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa ije na mkakati thabiti wa kuona namna gani ambavyo itainua uchumi wa Mkoa wa Kagera, kwa sababu kwa hali ilivyo sasa haikubaliki na hairidhishi. Kwa hiyo kwa haraka haraka ningependa kushauri maeneo yafuatayo kuhusiana na kuinua uchumi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ulikuwepo mradi wa Mto Ngono, na naishukuru Serikali wameshaanza kufanya upembuzi yakinifu. Lakini mimi naona na ninaomba sana Serikali mradi huu uwekwe katika orodha ya miradi ya kielelezo *(flagship project)* na uweze kutafutiwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, kwa kutambua kwamba Mkoa wa Kagera unapakana na nchi tatu na fursa zilizopo katika ukanda huo wa nchi za maziwa makuu, niombe sana Serikali irudishe mpango wa kujenga *airport* ya kimataifa, maana mpango ulikuwepo. Wakati sasa umefika tuurejeshe mpango ule ili Mkoa wa Kagera upate *airport* ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tunayo *Airport* ya Bukoba, wengi tunafahamu mchango wa *Airport* yetu ya Bukoba, niombe sana Serikali katika mwaka huu wa fedha ambao tunakwenda, 2023/2024, *Airport* yetu ya Bukoba iweze kufanyiwa uwekezaji kupata *fog light* pamoja na *control tower* ili safari za kwenda Mkoani Kagera ziwe ni safari zisizo kuwa na misukosuko na ikiwemo pia kufungua uchumi wa Mkoa wetu wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natambua kwamba Wilaya ya Bukoba Mjini ndiyo *reception* ya Mkoa wetu wa Kagera unaounganisha Mkoa wetu na nchi zinazo tuzunguka. Naomba kipekee kabisa Stendi ya Bukoba Mjini ipewe kipaumbele katika Mkoa wetu wa Kagera ikiwemo pia na Soko Kuu. Haikubaliki kwamba Mkoa wetu kwa namna ulivyo na kwa ukubwa wake, na ukizingatia hata kitakwimu za sensa tunazaidi ya watu milioni tatu

lakini mpaka leo Stendi yetu haieleweki ni lini itajengwa na fedha kupangwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoelekea kumalizia, Mkoa wa Kagera una zaidi ya *ranch* tano lakini bado *ranch* hizi hazijaonesha katika umahsusi wake unachangia vipi katika biashara ya nyama ikiwemo pia biashara ya maziwa. nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kushirikiana na Mawaziri wenzako mfanye tathmini, na hili jambo hata Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alishalisema. Tufanye tathmini ya zile *ranch* nini kifanyike ili *ranch* hizi ziwe na tija ziweze kuchangia ukuaji wa uchumi si tu wa Mkoa wa Kagera lakini na uchumi wa Tanzania. Ili *ranch* zile wapewe wawekezaji ambao wataleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami naunga mkono hoja, na ninaendelea kumpongeza sana Mwanauchumi Mbobezi Daraja Moja Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Wizara yako nzima. Halikadharika namshukuru sana na ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira, ahsante sana. Ninaendelea sasa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Mheshimiwa Kasalali hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, hayupo. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti kuu ya nchi yetu.

Nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya ya kujenga na kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri kaka yangu Dkt.

Mwigulu, kazi yake ni njema, yeye na timu yake na niseme tu kwamba hatuna mashaka na uwezo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nichangie bajeti kwenye maeneo mchache. Eneo la kwanza ni kwenye hali ya makusanyo. Nimeona kwenye ukurasa wa 19 Mheshimiwa Waziri ameeleza hali ya makusanyo. Na kwa ninavyomfahamu alivyo bingwa wa namba ameweka fedha tu hakuweka asilimia. Mimi nikajipa kazi ya kwenda kwenye asilimia nikajikuta makusanyo ambayo tumeshakusanya mpaka anawasilisha taarifa ile Aprili, 2023 tuko kwenye asilimia 78. Niwapongeze kwa kazi hii nzuri lakini kwa mahitaji ya nchi yetu bado tuna haja ya kuongeza nguvu zaidi kwenye makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tuungane na Mheshimiwa Waziri. Suala la kusisitiza umuhimu wa ulipaji wa kodi sio suala la Waziri peke yake na wala si suala la Serikali peke yake. Hakuna nchi inayoweza kuwezeshwa bila watu kulipa kodi. Sisi kama viongozi tuungane pamoja kuhamasisgha ulipaji wa kodi kwenye nchi yetu ili tuendelee kutengeneza maendeleo ya kwetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yako maeneo mawili naomba nitoe ushauri, eneo la kwanza nimeona kwenye ukurasa wa 107 Mheshimiwa Waziri ameeleza kuanza kutoza shilingi 20 kwa kilo ya saruji inayotoka nje na inayozalishwa ndani. Ukisema shilingi ishirini maana yake kwa mfuko mmoja unakwenda kuongeza shilingi elfu moja. Leo hii hatujaongeza tozo hii bei ya saruji ni kubwa na malalamiko ya watu wetu ni mengi, maeneo mengi watu wanashindwa kufanya kazi ya ujenzi kwa sababu ya bei hii ya saruji. Tukaliangalie vizuri jambo hili, sioni kama litakwenda kuwasaidia sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia watu watafanya ulinganisho, unakwenda kutoza shilingi 20 kwa kilo moja ya saruji lakini wakati huo huo kwenye ukurasa wa 97 unakwenda kutoa msamaha wa *VAT* kwenye *gaming odds* na kwenye *gaming software*. Jana amesema vizuri sana ndugu yangu Mheshimiwa

Jerry Silaa, jambo hili si zuri. Tunaomba mkaliangalie vizuri kama Serikali na ikiwezekana kwenye *finance bill* marekebisho yafanyike ili tuliondoe jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nataka nichangie ni kwenye upatikanaji wa fedha za kigeni. Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kwenye ukurasa wa 50 na 51 wa hotuba yake, kwamba nchi nyingi ziliingia kwenye changamoto ya kuwa na upungufu wa fedha za kigeni ikiwemo nchi yetu. Lakini umeeleza jitihada na hatua ambazo Serikali inafanya ikiwemo kuongeza uzalishaji ili tupunguze kuagiza bidhaa kutoka nje, ninawapongeza wa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo hili, pamoja na hii ya kuongeza uzalishaji na kupunguza kuagiza bidhaa liko eneo ambalo tunaweza kutengeneza fedha nyingi za kigeni kwenye nchi yetu, na si eneo lingine, ni kwenye eneo la sekta yetu ya utalii. Sekta ya utalii inaweza kutuingizia fedha nyingi za kigeni kwenye nchi yetu. Na bahati nzuri amesema mwenyewe kwenye hotuba yake. Niungane naye kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua kufanya kazi ya kutangaza utalii wa nchi yetu kwa vitendo. Matokeo ya *Royal Tour* yameonekana, amesema mwenyewe kwamba tumeongeza fedha za kigeni kutoka dola 1,310,000 mwaka 2021 hadi dola 2,527,000.7 mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ninayoiona hapa, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa *Royal Tour,* tunampongeza kwa maneno au tunampongeza kwa dhati ya mioyo yetu na kwa kazi ambazo tunazifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto; mwaka 2019 wakati wa kupitisha bajeti ya mwaka 2019/2020 tulifanya marekebisho kwenye *Finance Bill.* Marekebisho tuliyoyafanya tukaleta utaratibu mpya wa taasisi za uhifadhi kukusanya fedha, akina *TANAPA,* Ngorongoro kwamba fedha zao zikusanywe moja kwa moja kwenye mfuko mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida na jambo hilo limefanyika lakini tangu tumeanza jambo hili changamoto zimekuwa ni nyingi. Tukaja na mawazo ndani ya Bunge hili kwamba pamoja na makusanyo haya kwenda moja kwa moja tuhakikishe tunaweka *retention* kwa taasisi hizi ili ziweze kujiendesha, shughuli za uhifadhi ni za gharama, zina dharula nyingi, wazo hilo halikusikilizwa. Wakati wa kupitisha bajeti ya mwaka 2021/2022 kamati ya bajeti ikashauri kama *retention* imeshindikana basi angalau muweze kutoa hali ya miezi miwili au mitatu mbele kama *OC* kwa taasisi hizi, mpaka leo imeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapozungumza leo, hali ya taasisi za uhifadhi ni mbaya. Tunakwenda kwenye *high season* hawana fedha, miradi ya barabara imesimama, *OC* haziendi. Hiyo *high season* tunakwenda nayo namna gani, tunatengenezaje fedha? Tunaomba Mheshimiwa Waziri walete utaratibu mpya, tutoe *retention* kwa taasisi hizi. Wakishindwa *retention* basi *OC* za taasisi hizi wa akina *TANAPA*, Ngorongoro, *TAWA* zitoke mapema, ikiwezekana awe na *advance* ya miezi mitatu. Tembo wanasumbua wananchi taasisi hazina fedha, majangili wanarudi kwa kasi taasisi hazina fedha lazima tuziwezeshe taasisi hizi ziweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mheshimiwa Waziri akija atuambie, wakati wa bajeti ya Wizara ya Maliasili tulisema lakini hatukupata majibu. tumekwama wapi kwenye zoezi la kuhamisha watu kwa hiari kwenye hifadhi ya Ngorongoro? Zaidi ya miezi saba zoezi limesimama. Kama unataka kunusuru hifadhi ile ni lazima tuhakikishe, tunahamisha watu na watu wamekubali, wamejiandikisha, wamesimamisha shughuli zao tumekwama wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atuambie... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava...

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Maimuna Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii, Nimshukuru pia Mwenyezi Mungu, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pamoja na yote namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kile kitendo ambacho amekifanya kutukwamua sisi watu wa Mtwara kutokana na barabara yetu ya kiuchumi ya Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi. Mheshimiwa Rais amepeleka zaidi ya bilioni 234 kwa ajili ya barabara ile ambayo ilikuwa kwenye ilani kwa muda mrefu na haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye bajeti, niipongeze sana Wizara kwa wasilisho zuri, lakini zipo changamoto ndogo ndogo ambazo zinatakiwa kuangaliwa. Kwenye ile bajeti kuna aya inayozungumzia suala la sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo; na tunatambua kabisa watu wetu wengi wanaishi vijijini wanategemea kilimo kwa ajili ya kustawisha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambayo inawakumba wakulima wetu. Kwa mfano, ukienda mikoa ile ambayo inalima zao la korosho kumetokea na utaratibu mwaka huu wa kufanya sensa wa miche ya mikorosho. Wakulima wametekeleza agizo hilo, lakini sasa wakati wa kutoa zile pembejo ambao unafuatana na zile sensa, mambo yamekuwa magumu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo baadhi ya kata ambazo vijiji vyake, kwa mfano, ukienda Kata ya Maputi ambayo ipo Jimbo la Newala Vijijini, kati ya vijiji sita vya kata ile, vijiji vitatu havimo kwenye mpango. Vile vile, ukienda Kata ya Mnyambe, Kata ya Malatu, hizo zote zina–*miss* kuwemo kwenye utaratibu wa kupata pembejeo kwa sababu ya mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Wizara kuangalia utaratibu mzuri ambao wakulima watapata pembejeo kwa wakati kwa sababu msimu wa upuliziaji wa zao la korosho ni sasa.

Inapotokea mkulima hayupo kwenda kurekebisha inachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, tutapishana na wakati. Badala ya wakati wa upuliziaji, upuliziaji utapita, kwa hiyo yale manufaa ambayo tumeyapanga kwamba tunataka kukusanya mazao, tutakosa kupata kile ambacho tulikuwa tunakitarajia. Kwa hiyo, niombe sana hilo lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye upande wa elimu; kuna mambo mengi. Tumeona sasa hivi namna ambavyo Serikali inapeleka fedha nyingi kujenga madarasa. Tunashukuru na kwa sasa madarasa mengi yanakwenda yakiwa na madawati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna changamoto ambayo imejitokeza kwenye yale madarasa ya zamani. Madarasa mengi ya zamani watoto wanakaa chini, hakuna madawati. Ili umwandae vizuri mwanafunzi lazima akae sehemu nzuri ya kujifunza na kujifundishia. Mwanafunzi anapokosa dawati, hawezi kujifunza vile ambavyo tulikuwa tunatarajia. Kwa hiyo niombe, mwaka 2026 kulikuwa na mkakati ambao ulizilazimisha halmashauri kuhakikisha kwamba madawati yanapatikana. Baada ya mkakati ule hapakuwa tena na shinikizo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu halmashauri inakumbana na changamoto nyingi kutokana na mambo ya kifedha, lakini kama hatutaweka msisitizo, wanafunzi wataendelea kupata shida ya namna ya tendo la kujifunza na kujifundishia kwa sababu wengi wanakaa chini, tunawasababishia afya zao kuteteleka kwa sababu anajikunja tangu asubuhi mpaka jioni, zoezi la mwaka mzima, tutawasababishia wanafunzi wetu vibyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, tunayo misitu yetu ambayo inasimamiwa na watu wa Maliasili, tuone namna ambayo tunaweza kupata magogo tukapeleka yakatengenezwa madawati ambayo yatakwenda kusaidia shule zetu.  Nafahamu upo utaratibu, lakini watu wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakae pamoja na watu wa TAMISEMI, waone namna ambavyo changamoto hii inaweza kwenda kutatuliwa ili wanafunzi wetu wapate sehemu ya kukalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasafirisha magogo kwenda kuyauza nje, sawa tunapata fedha lakini je, afya na ustawi wa wananchi wetu na watoto wetu tunauweka wapi? Tunapotengeneza mazingira ambayo yatasababisha magonjwa, tunazalisha kitu kingine ambapo tutakwenda kutafuta fedha kwa ajili ya kuwatibu, kitu ambacho kingekuwa *solved* kama wanafunzi hawa wangekaa katika mazingira mazuri ya kusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, kuna suala la usafi binafsi. Tunafahamu hali za wananchi wetu ni ngumu. Mtoto anakaa chini, asubuhi anaondoka yuko vizuri, msafi, lakini anaporudi jioni ana vumbi amechafuka kwa sababu amekaa chini tangu asubuhi mpaka jioni. Kwa hiyo, kuna vitu vingi vinatengenezwa hapo, lakini *source* inakuwa ni ukosefu wa madawati katika madarasa yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka wajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kuboresha uchumi na maisha bora kwa Watanzania. Kwa hakika naomba nifanye nukuu kutoka kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimekuwa nikilisemea hili kwamba Mama Samia anapiga kote kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo anafanya miradi mikubwa na midogo, wakati huo huo wastaafu wanapata stahiki zao, wafanyakazi wamepandishwa madaraja na wamelipwa mishahara. Hakika Mama anastahili maua kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Vile vile, tunasema Mama yuko kazini na kazi inaendelea. Pia, wale ambao waliofikiri Mama Samia hawezi, hakika wameona anakwenda anafukunyua, anaibua ili kuhakikisha kwamba anafanya kazi yake sawasawa. Kwa hiyo, niwaombe Watanzania waelewe kwamba hakuna wakati wa kumpangia. Kuna wakati watasema ana–*copy* na ku–*paste* kwa sababu wanawake hawawezi, Hapana, wanawake tunaweza, tuna–*initiate,* tunabuni na tunasogeza. Mama yuko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie bajeti hii ya 2023/2024. Niipongeze Serikali kwenye suala zima la kuongeza mapato. Nitachangia vipengele viwili vya ukurasa wa 27 na ukurasa wa nane kwenye Mapato na Uchumi wa Kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, Desemba, 2022 waliweza kufanikiwa kukusanya zaidi kwa kupata trilioni 2.53 ambazo hazijawahi kutokea kukusanywa, zimekusanywa kipindi hiki cha Mama Samia Suluhu Hassan. Vile vile, Serikali imekiri kwamba mafanikio yale yalitokana na kuboresha mifumo. Hata hivyo, bado naamini na Serikali inaamini hivyo kwamba tunaweza kukusanya zaidi mapato yetu ya ndani. Pia, wengi wamezungumza hapa kuhusu suala zima la kuongeza mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nishauri kwenye suala zima la uchumi wa kidigitali. Sasa hivi Serikali imebuni lakini tunategemea *EFD machine* pekee katika kuhakikisha kwamba tunakusanya kodi. Hata hivyo, kwenye *EFD* tunajua kulingana na baadhi ya Watanzania ambavyo walivyo, hawataki kulipa kodi utakuta mtu amenunua kitu cha 100,000 anapewa risiti ya 10,000 au wakati mwingine hapewi risiti kabisa. Sasa, nini kifanyike kuhakikisha kwamba *automatic by default* mfanyabiashara atahakikisha analipa kodi? Nafikiri ni *increase visibility* ya *cash flow* ya mfanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tunaweza kujua kila simu ya Mtanzania inayoingia imepigwa kwa dakika ngapi na shilingi ngapi, nina hakika kabisa kwa kutumia uchumi wa kidigitali, tunaweza kujua *cash flow* ya kila mfanyabiashara nchini. Pia, iwapo *cash flow* yake itakuwa *visible, there is no way* huyu mtu atakwepa kulipa kodi, atalipa kodi *accordingly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kutumia uchumi wa kidigitali, naomba sana tu–*encourage* kulipa malipo kwa Lipa namba, tu–*encourage* kuhakikisha *VISA Card* zinatumika, tuhakikishe kwmba tuna–*discourage* malipo ya *cash* (*cash money* isitumike katika kuhakikisha tunafanya manunuzi). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa tunalipa *cashless* kwa kutumia *card*, tuna *increase visibility* ya *cash flow* ya biashara yoyote ile nchini. Pia, itakuwa ni rahisi ya kuhakikisha kwamba mfanyabiashara analipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu na mikakati ya kuhakikisha kwamba Watanzania hatulipi fedha taslimu (tunalipa kwa kutumia lipa namba na tunalipa kwa kutumia *VISA Card*). *Of course,* mwanzoni tutahitaji elimu, lakini hata mbuyu ulianza kama mchicha. Naamini Tanzania imeweza kubuni mambo mengi na ndio sababu tumeweza kusogea. Hivyo, hili pia linawezekana, tu–*increase visibility* ya *cash flow* ya mfanyabiashara yeyote yule, ni *solution* pekee ya kuhakikisha kwamba kodi inalipwa. Vile vile, *through EFD only* bado kodi inakwepwa. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 43 umezungumzia uwezeshaji, viwanda na biashara. Sasa, wakati Serikali inasema imeendelea kuboresha mazingira ya kibiashara, nimekuwa najiuliza, kwa nini viwanda ambavyo vimekwishaanzishwa vinakufa? Serikali imefanya tathmini gani katika viwanda ambavyo vinakufa ili kuhakikisha havifi na vinasaidia kusimama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kule kwetu Tanga, mimi roho inaniuma sana. Kiwanda cha Kutengeneza Mazulia

ambacho kipo Tanga Mjini kimekufa wakati sisi ndio tunazalisha mkonge. Kwa nini Serikali haikuona haja ya kuweka juhudi kuhakikisha kiwanda kile hakifi? Kwa nini kule Lushoto Kiwanda cha Usambara *Factory* ambacho kinatengeneza *tomato* na nyanya zinazalishwa Lushoto, kwa nini kiwanda kile kimekufa? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali watakapokuja ku–*windup* watupe kwa nini viwanda hivi vimekufa na Serikali wamefanya juhudi gani kuhakikisha viwanda hivi havifi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo wajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia angalau kidogo kwenye Bajeti hii ya Serikali. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kumwakilisha Mama yetu ambaye anaitumikia nchi hii kwa moyo wa upendo na moyo wa kutujali Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze tu moja kwa moja kumwomba Mheshimiwa Waziri kaka yangu, najua mengi yameshaongelewa lakini katika Jimbo langu la Mkalama na Jimbo lake la Iramba Magharibi na Iramba Mashariki *TRA* wanafanya kazi kwa kuijbanza kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pale Jimboni kwake, Jimboni kwangu wamepanga vyumba viwili, hatuna watumishi, hatuna Meneja, sasa hii inatupa shida sana.

Nimwombe Mheshimiwa Waziri, angalau atenge hata kidogo, japo milioni 150 kila wilaya ili angalau tupate Ofisi ili tuweze kulipa kodi vizuri na wananchi wetu wasipate shida wakati yeye ndiye Waziri wa Fedha, *charity begins at home* hiyo haikwepeki. Akija kuondoka hapo hajajenga Ofisi tutakuwa tunamnyooshea vidole, tunamwomba atenge fedha ajenge Ofisi pale Mkalama na pale Iramba Magharibi na Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri, suala la kukwepa kodi kwa kutokuchukua risiti limezidi sana. Pia, hii inasababishwa na jinsi sheria yenyewe ilivyo. Kuna Mbunge mmoja hapa alitoa wazo kuhusu kutoa *commission* kwa watu watakaotudai risiti, hilo ni wazo zuri. Nami nataka niongeze jambo moja, Waziri amefanya vizuri sana kwa kuongeza kiwango kwamba mpaka milioni 200 ndipo mtu ataingia *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hiki kiwango cha kutoka milioni nne mpaka kufikia hiyo milioni 200 hakina madaraja, yaani ikishafika tu milioni nne Kwenda 11, Afisa wa kodi ndio anakaa anaangalia asilimia 3.5 ya mauzo. Ina maana mtu mwenye milioni 200 anapaswa kulipa milioni saba. Hiki kiwango ni kikubwa mno kinasababisha watu wakwepe kodi. Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, hiki kiwango cha kutoka milioni nne mpaka milioni 200 kiwe na madaraja ambayo yatasababisha watu watumie *EFD machine* bila wasiwasi kwa sababu anajua daraja langu ikifika kiasi fulani nitalipa kiasi fulani. Pia, naomba nimshauri Waziri kuhusu madaraja ambayo mimi naona nafaa kupendekeza na wataalamu wako wataona, yako kama saba hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuanzia milioni nne mpaka milioni 11 wafanyabiashara wakilipa 150,000 itatosha. Kuanzia milioni 12 mpaka milioni 20 walipe 450,000. Kuanzia milioni 21 mpaka milioni 50 walipe 650,000. Kuanzia mauzo ya milioni 51 mpaka milioni 75 walipe 850,000. Kuanzia mauzo ya milioni 76 mpaka milioni 100 walipe milioni moja. Kuanzia milioni 101 mpaka milioni 150 walipie 1,500,000. Kuanzia mauzo ya milioni 150 mpaka hiyo milioni 200 waliyoweka walipe milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mfanyabiashara wa daraja la chini, akienda kulipa kila baada ya miezi mitatu analipa 500,000, watu wengi watalipa kodi na hawatakwepa hiyo *EFD*. Atakuwa anatumia *EFD,* anatoa risiti hana wasiwasi, anajua nikifika milioni 200 nitalipa milioni mbili, nikifika 150 nitalipa milioni moja. Itakuwa hakuna suala la kukwepa na watu wengi sana watalipa kodi ambayo itakuwa haina maumivu wala nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la asilimia 3.5 ya mauzo kuanzia milioni 11, Afisa anakaa pale anakukadiria haiangalii ulipata hasara, haiangalii sijui mauzo na mtaji ule ni kiasi gani, mauzo yanaweza kuwa makubwa lakini faida ni kidogo, lakini unapigwa 3.5 na unatakiwa kutoa milioni saba, watu wataendelea kukwepa kulipa kodi kila siku. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri akae na wataalam wake, waweke haya madaraja, mimi nimetoa yangu, lakini mimi sio mtaalam wa kodi, lakini ninyi mnaweza mkayaboresha zaidi. Aidha, wakaongeza au wakapunguza. Haya madaraja yakiwepo watu watakuwa hawana hofu, anajua mimi daraja langu likifika nitalipa kiwango hiki, *EFD* itaonesha kwamba nimefikiwa hicho kiwango na watu watalipa kodi kabisa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala la kujenga Ofisi kwenye majimbo yetu mawili, langu na lake, sisi ni pacha asisahau. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo wajiandae.

Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nyingi anazozifanya za kuwahudumia Watanzania. Vile vile, niwashukuru kaka yangu Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri kwa kazi wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu suala la kodi. Wenzangu wengi wamezungumza kuhusu ukusanyaji wa kodi, lakini yako mambo ya msingi ambayo kama Wizara wanatakiwa wayaone na wayaangalie kwa mapana na marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mfano mmoja, leo kontena linatolewa bandarini na likitolewa bandarini *charge* zote zinafanyika mle ndani. Hata hivyo, yale makontena yakishaingia Kariakoo, wakati yanatelemshwa utakuta kuna askari zaidi ya 30 wanazunguka kwenye yale makontena. Pia wale askari kuondoka kwenye yale makontena ni lazima kuwepo na utamaduni wowote ambao wao wanaufikiria na ambao ndio unaotendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini ambacho nataka kukiongelea? Kama kontena linatoka bandarini likiwa limelipiwa kodi stahiki zote na linakwenda maeneo ya Kariakoo kushushwa, hakuna tena haja ya yule mfanyabiashara kwenda kutoa rushwa wakati anateremsha lile kontena. Kwa hiyo, haya mambo ndiyo wanayoyazungumza Wabunge humu ndani, ukwepaji wa kodi ni mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Mradi wa Maji wa Ruvuma kule kwangu. Hili nalizungumza kwa masikitiko makubwa sana. Huu mradi wa Ruvuma ambao unakwenda kuwasaidia wananchi wa Mtwara na pembezoni mpaka kufika Lindi, tayari mradi huu Benki ya *ADB* ilishaweka *token* kwenye miradi yake kwa zaidi ya dola 160, wako tayari ku–*engineer* huu mradi ufanye kazi, lakini iko kampuni ya China *Railways International Group* na wao waliweka dola milioni180. Sasa, sijui uzito uko wapi au shida iko wapi wakati Mheshimiwa Rais amefika mahali sasa ametanua wigo na amempa mamlaka Mheshimiwa Waziri wetu kwamba amsaidie Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia 2025 wananchi wa Mtwara hawana maji salama, lakini wako watu ambao inawezekana wakasaidia kutuleta maji. Mheshimiwa Waziri, akija hapa aje na majibu kigugumizi kiko wapi? Kwa kweli Mheshimiwa Mwigulu mimi ni mdogo wangu na msikivu sana, si vema nikazungumza hapa kwa ukali sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa hili anisaidie kaka yake. Namwomba sana Mheshimiwa Mwigulu, hajawahi ku–*fail* kwenye jambo lolote ambalo anali–*engineer*. Sasa kama mimi kaka yake ananifanyia hivi mpaka napiga kelele hapa, kwa kweli ni vitu ambavyo sio vizuri sana nianze kupiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kampuni ya *Alliance* inaleta magari aina ya *TATA*. Kampuni hii imekuwa ni kampuni ya kudhulumu Watanzania toka imefika katika nchi hii. Nazungumza humu ndani tukiwa ndani ya Bunge hili, kabla Wabunge hawajaja kuwa Wabunge humu, kuna wahanga zaidi ya 30. Unakwenda kukopa hela benki na wewe unakwenda kukopa gari, unaacha pale milioni 70, unapewa gari ya milioni 130. Unaposhindwa kulipa takribani zimebakia milioni tano au sita, zile gari unanyang'anywa na Mheshimiwa Waziri, Mwigulu Nchemba, anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaleta kampuni tukiwa na lengo kubwa la kuwasaidia Watanzania, lakini kampuni hii haiwasaidii Watanzania. Leo tukipiga parapanda hapa tuwaite Watanzania waliodhulumiwa na ile Kampuni ni hatari sana. Sasa Serikali tunayo na niishauri Serikali waamke sasa. Hawa wenzetu tayari wamefika mahali wamewadhulumu Watanzania zaidi ya asilimia 80. Kwa kweli suala hili halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimezungumza hapa kuhusu madai ya vijana wetu na wazee wetu wa Jimbo la Mtwara Mjini ya fedha za Kampuni ya *PRIDE*. Deni hili ni deni la muda mrefu kaka yangu Mwigulu analifahamu sana, zaidi ya milioni 500. Leo hii wale wananchi ambao wanaidai *PRIDE* wengi wao ukiwaona wameshauziwa nyumba zao hawana pa kwenda, lakini Serikali kila nikiingia humu ndani Bungeni naambiwa kesho, kesho kutwa utapata majibu na majibu ni haya ya malipo kulipa fedha. Sasa mimi nataka Mheshimiwa Mwigulu atakapoingia hapa anieleze

kwamba bwana wale wananchi wangu ambao wanadai fedha za *PRIDE* zaidi ya milioni 500 lini wanakuja kuwalipa wale Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zilikuwa ni tano na mimi nimezitumia dakika tano na nusu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, nilimtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaishukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengi sana ambayo hatuwezi kuyataja yote lakini utekelezaji mzuri wa bajeti ya mwaka 2022/2023 ambayo imetuwezesha sasa kuingia kwenye bajeti hii ya 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi katika Jimbo langu la Mwanga ni mingi ambayo imetekelezwa lakini tunaomba kusisitiza juu ya ukamilishaji wa miradi muhimu ambayo bado inaendelea. Mradi wa kwanza ni Hospitali ya Wilaya ambapo tulitengewa bilioni 3.3 mpaka sasa hivi tumepata bilioni mbili tunaomba hiyo bilioni 1.3 ili tumalizie ile kazi iliyobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi mkubwa wa Maji wa Same, Mwanga - Korogwe, tunaishukuru sana Serikali imekwamua mradi huu ambao ulikuwa umekwama tumeahidiwa kukamilika ndani ya miezi 14 na nikuambie tu kwamba kuna mama mmoja aliniita kwenye eneo lile la mradi, amepigilia vijiti 14 kwenye ukuta wake kila mwezi ukipita anang'oa kimoja ananiambia Mheshimiwa Mbunge vinavyozidi kupungua hivi vijiti ndiyo mimi nategemea maji yanywewe. Kwa hiyo, kuna siku atakapong'oa cha mwisho kama maji hayajanywewa tutapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwanga wana imani kubwa sana kwamba miradi hii itakamilika na sababu kubwa ni mbili, sababu ya kwanza ni kwamba wanamuona Mheshimiwa Rais jinsi ambavyo ameendeleza mahusiano katika diplomasia ya uchumi kiasi ambacho tunaendelea kupata fedha za maendeleo. Pili, kinachowapa imani kubwa ni bajeti hii ambayo kwanza imepanua wigo wa kodi lakini pili imeweka *commitment* ya kutumia utaratibu wa *PPP* na pia kufufua Ofisi ya *Tax Ombudsman* ambayo nayo itatuharakishia fedha kuingia kwenye mzuguko, kodi kulipwa kwa wakati na mambo kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo imani ya watu wa Mwanga ni kwamba kwa sababu hiyo basi, miradi yao itaendelea kutekelezwa vizuri. Wito wangu ni kwamba Serikali iendelee ku-*negotiate* vizuri mikataba ya *PPP,* tui-*negotiate* kibingwa ili tuweze kupata faida tunayostahili sisi kama wananchi wa Tanzania. Ile mikataba inayofanya vizuri tuendelee kuiheshimu kama mkataba wa *SONGAS* kwa mfano, ni moja kati ya *PPP* ambazo kwa ufahamu wangu zimetuletea heshima kubwa sana kama nchi tujifunze kwamba tulifanya nini hawa *SONGAS* wakatufanikisha kiasi hicho tuendelee kuutunza mkataba huu lakini pia tuendelee kuingia mikataba mingine mizuri kama huu wa *SONGAS* ambao unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kilio kikubwa sana ambacho kinasumbua katika nchi hii kwa sasa hivi, nacho ni suala la wakandarasi wazalendo na malimbikizo ya madai yao katika miradi ambayo wanaifanya. Wako wakandarasi wengi sana ambao wanashikilia *certificate* sasa hivi zaidi ya miezi tisa na hawajalipwa na wameanza kukata tamaa, wameanza kufilisiwa na mabenki kwa dhamana zao kuuzwa, lakini kikubwa pia ni kwamba pamoja na kwamba wakati mwingine tunapata hasara ya kulipa *interest* lakini ile *interest* ile riba haisaidii chochote kwao, kwa sababu wamekopa benki kwa riba kubwa za asilimia 20 halafu fedha zikichelewa ile riba inazidi kukusanyika wakati wao huku riba wanayolipwa ni kidogo sana kwa mujibu wa Mkataba. Kwa hiyo, wanaendelea kwenda chini na pia iko hatari ya mabenki kufikia mahali kuona kwamba miradi hii ya Serikali ni

miradi hatarishi jambo ambalo si jema na wala halifai kwa afya ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza mara nyingi kwamba walipwe kwa wakati ili tuweze kukwepa riba hizi ambazo Serikali upande mmoja inapata hasara lakini pia wakandarasi wetu wanazidi kupata hasara kwa sababu riba ile ni ndogo ukilinganisha na riba ambayo wanalipa kwenye mabenki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nishauri tu juu suala la *Tax Ombudsman* ambalo nimelizungumza, nimejaribu kuangalia kanuni zilizotengenezwa mwaka jana kwa bahati mbaya zinaleta mlolongo mrefu kidogo wa jambo kuamuliwa mbele ya ile Ofisi ya *Tax Ombudsman*. Ukiangalia zile *notice* zinavyokwenda ni karibu siku 154 kwa shauri moja kuamuliwa, hiyo inaweza iturudishe kulekule ambako kulikuwa na mlolongo wa kwenda kwa Kamishna halafu uende *TRAB,* uende *TRAT* uende Mahakama ya Rufaa unatumia karibu miaka mitano. Nchi jirani hapo mwaka 2016/2017 Ofisi ya *Tax Ombudsman* ilishugulikia masuala ya malalamiko 92,000 na ikafanikiwa kuamua 77,000 na hiyo ni kwa sababu r*egulation* zao kidogo zinachukua muda mfupi kukamilisha malalamiko ambayo yamepelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo mimi kwa kweli ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia zote, nikitarajia kabisa kwamba kasi ya miradi iliyokuwa ikienda katika Majimbo yetu hasa Jimbo langu la Mwanga itaendelea kama vile ambavyo imekuwa ikiendelea na pengine kwa kasi zaidi kutokana na jinsi ambavyo bajeti hii imeleta matumaini makubwa. Mheshimiwa Waziri tukupongeze na tukushukuru unatuwakilisha vizuri katika sekta yako na kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukuamini kama ambavyo sisi tumeweza pia kukuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anania Tadayo.

Waheshimiwa Wabunge muda wa wachangiaji Wabunge umeisha sasa tutaingia wachangia upande wa Mawaziri, lakini kabla ya kuanza kuwataja Waheshimiwa Mawaziri nina matangazo mawili, tangazo moja ni la wageni ambao wametutembelea jioni hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wetu wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri ana watoto wengi na wazuri ambao amejaliwa na Mwenyezi Mungu kuwalea, leo wapo hapa ambapo wengine anaishi nao kwenye bweni la wavulana na wasichana hapa Dodoma pia na Dar es Salaam wapo anaishi nao.

Kwa hiyo, leo naomba niwatambulishe watoto 50 ambao wameambatana na mkewe *Mrs. Neema Mwigulu Nchemba* pamoja na mtoto Isack Mwigulu, wako pale wale, karibuni sana watoto wetu wazuri kutoka Dar es Salaam na hapa Dodoma. *(Makofi)*

*Mrs. Neema Mwigulu* na Isack Nchemba ni wapi? Anhaa! wale pale, karibuni sana karibuni hongera sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa timu hiyo nzuri sana Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, wale pale karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Muharami Mkenge. *(Makofi)*

Pia tunao wageni ambao wametembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo tuna vijana 60 wa Jukwaa la Viongozi wa *Africa Youth Leadership Forum* kutoka nchi nzima, karibini sana Viongozi wa Jukwaa hili katika Bunge letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunalo tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge, ananiomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - JKT, anawakaribisha kushiriki mbio za *JKT marathon* siku ya

Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 ambazo zitaanza na kuhitimishwa katika Uwanja wa Jamhuri Jijiini Dodoma. Mbio hizo ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 60 JKT. Washiriki wote wanaombwa kuwasili katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma kuanzia 11.30 alfajiri. Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne.

Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria mbio hizi muhimu katika kusheherekea Miaka 60 ya JKT.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza upande wa Waheshimiwa Mawaziri, tutaanza na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, baadae atafuata Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika bajeti hii ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na juhudu za dhati za kuhakikisha tunafikia kujenga uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu ambayo ni adhma ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Daktari Mwigulu Nchemba ambaye kwa kweli anafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha nasi tunajenga uchumi wa viwanda ambao kimsingi unategemea ushirikishwaji kati ya Serikali na sekta binafsi na Serikali tumeendelea kufanyakazi kubwa ili kuweka maboresho mbalimbali ambayo tunaamini yanaendelea kusaidia kupunguza urasimu katika ufanyaji biashara lakini pia katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo nitumie nafasi hii kueleza kidogo kuhusiana na mpango wa kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ambayo Wizara yangu inaendelea kuratibu lakini kwa kushirikiana na sekta zote muhimu katika nchi hii ili kufikia azma ya kuwa na uchumi shindani kama nilivyosema na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2023 jumla ya marekebisho 307 ambayo yameondoa na kupunguza tozo mbalimbali yamefanyika lakini katika kipindi hicho Sheria 48 zimefanyiwa marekebisho ambapo kwa mwaka 2022/2023 pekee zaidi ya Sheria 12 zilifanyiwa marekebisho ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa na maboresho jumla ya 105 yanayohusu ada, tozo na kodi mbalimbali ambazo zilikuwa kero katika kufanyabiashara na uwekezaji nchini lakini kubwa zaidi katika hili ni mfano wa usajili kuanza kutumia fedha za Kitanzania badala ya dola ambazo zimekuwa kero katika kuhakikisha tunatoa huduma kwa Watanzania. Moja ya mfano huo ni usajiri wa chakula cha watoto wachanga na *formula* za ukuzaji kabla ya maboresho ilikuwa inatumia dola za Kimarekeni 900 ambayo ilikuwa ni sawa na shilingi 2,120,400 lakini sasa tunatoza kwa shilingi milioni moja pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea pia kuboresha, kuondoa na kupunguza tozo katika maeneo mbalimbali muhimu, moja ni sekta ya kilimo, afya, mifugo, utalii pamoja na taasisi za udhibiti zilizoko hapa nchini. Pia maboresho mengine ni uimarishaji wa mfumo TEHAMA ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwamba tuendelee kuboresha. Kwa mfano, sasa hivi mifumo 58 ya kutoa vibali na leseni zinatumia njia za kielektroniki katika mamlaka mbalimbali za udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mfumo wa malipo ya Serikali wa kielektroniki ambao umeimarishwa kwa maana ya *GePG* ambao unatoa huduma zaidi ya 900 ambazo zimeunganishwa na kurahisisha walipaji kodi na huduma mbalimbali wanazolipa Watanzania ili kupata huduma kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mfumo unaowezesha mifumo mbalimbali ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa, maana yake kulikuwa na hoja kwamba ndani ya Serikali hakuna mawasiliano lakini tunaendelea kuboresha, hadi sasa zaidi ya mifumo 50 katika taasisi 45 zimeweza kubadilishana taarifa ambazo zinasaidia ufanyajikazi ili kuhakikisha tunaendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tumeendelea pia na kuanzisha sasa vitengo maalum, changamoto kubwa tuliyonayo ni katika ngazi za Halmashauri. Sasa tunaenda kuanzisha kitengo ambacho kitashughulikia masuala ya uwekezaji, viwanda na biashara ili shughuli hizo ambazo wengine wanalazimika kuja Makao Makuu kwa maana Wizarani sasa waweze kuapata huduma kule katika ngazi ya Halmashauri. Hii yote ili tuweze kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo ya haya ambayo tunaendelea nayo kumekuwa na angalau sasa kupunguza malalamiko kama si kumaliza, angalau tumepunguza kwa asilimia 71. Matokeo ya kupungua kwa siku za kuhudumia kwa mfano katika taasisi zetu, mfano OSHA wamepunguza muda wa kupata vibali kutoka siku 14 mpaka siku tatu.  Pia muda wa kutoa leseni na kukabidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kutoka siku 28 mpaka siku tatu, muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 mpaka siku moja. Muda wa usajili wa hospitali binafsi kutoka miezi 12 hadi miezi mitatu. Muda wa usafirishaji wa mizigo umepungua kwa mfano kutoka Dar es Salaam mpaka Tunduma ilikuwa wastani wa siku saba na sasa hivi imeenda kuwa siku tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tumepunguza kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka zaidi ya siku 14 hadi siku tatu mpaka saba. Pia tumepunguza mchakato wa ushughulikiaji wa maombi, mfano taasisi ya *OSHA* hatua ambayo imepunguza kutoka hatua 33 mpaka hatua saba, zaidi tumepunguza foleni ya kuomba huduma katika taasisi zetu ambazo zilikuwa ni foleni kubwa ukifika kwa mfano pale *BRELLA* na maeneo mengine

utakuta msururu wa watu wanasubiri kupata huduma katika Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka niseme haya kwa sababu kwa kweli pamoja na changamoto tulizonazo kwenye uwekezaji na viwanda wamesema hapa kuna viwanda vingine ambavyo vimefungwa lakini tunahakikisha sasa sababu zile au changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia Serikali tunazichukua kwa umakini kabisa ili tuendelee kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara ili nasi sasa tuendelee kuwa nchi shindani katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki lakini pia katika *SADC* lakini katika Eneo Huru la Biashara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni mbalimbali ambazo kwa kweli tunadhani ni muhimu katika kutekeleza shughuli za Serikali. Kwa mfano, Serikali imepitia na kurekebisha Sheria na Kanuni 12 hususani katika sekta za uwekezaji, viwanda na biashara, kilimo, ufugaji, afya na maliasili na hii imeenda kuboresha katika kuhakikisha tunaimarisha mifumo ya taasisi, kama nilivyosema tumeanzisha dawati au kitengo maalum cha viwanda, biashara na uwekezaji katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Mheshimiwa Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri wa Ujenzi atafuatiwa na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuunga hoja ya bajeti hii, bajeti ya wananchi, bajeti ambayo kwa kweli imewasilishwa kwa umakini mkubwa na kwa umaridadi mkubwa sana, hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa ufafanuzi kwa mambo machache ambayo yamejitokeza kutoka kwenye michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na hasa ile ambayo iligusa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na hasa Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kupokea na kuwashukuru Wabunge wote ambao wamesimama na kuchangia, kupongeza jitihada na juhudi kubwa ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jinsi anavyofanya, kuitendea haki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hili linafanyika kutokana na ukweli kwamba Mheshimiwa Rais ametambua kwamba uchumi wa Tanzania unaendelea kukua sana na ili uendelee kukua moja ya kigezo kikubwa sana ni kufanya miundombinu na hasa barabara iwe bora ambayo inaweza ikapitika kwa uharaka na kwa urahisi na hivyo kushusha gharama ya uendeshaji hasa katika ufanyaji wa shughuli za biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomsaidia Mheshimiwa Rais kwa nafasi hizi, napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba miradi yote ambayo tumeiahidi, tumeitangaza na ambayo tunaendelea kuitangaza, tuna uhakika kwa asilimia 100 kwamba itatekelezwa kama ilivyopangwa, kwani hatuna mashaka na yale ambayo ni makusudi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ushauri, maoni na mapendekezo yote ambayo mmeyatoa tumeyachukua na tunaahidi kwamba tutaenda kuyafanyia kazi ili kuendelea kuboresha katika utekelezaji wa majukumu yetu katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie suala moja ambalo kuna Mheshimiwa Mbunge ameliongelea na hasa barabara za Kigoma pamoja na miradi ile *complementary*

*projects*. Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi ndiyo mikoa ambayo kwa kweli ilikuwa haijaunganishwa na lami kati ya mikoa na mikoa. Ambacho Serikali ya Awamu ya Sita inaifanya ni kuhakikisha kwamba Kigoma hii inaunganishwa yote kwa barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba tunapoongea, wakandarasi watano kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kwa maana ya Kasulu - Manyovu wako *site* na kwa kweli kasi ni kubwa na hasa baada ya kipindi cha mvua kwisha. Upande wa kutoka Tabora sasa hivi ukishafika mpaka Malagarasi ni lami na kipande kilichobaki, mkandarasi ameshika kasi kuhakikisha kwamba pia anamaliza tatizo lilokuwepo la kilometa 51. Kwa sasa zimebaki kilometa 51.3 ukitoka hapa Dodoma kwenda Kigoma ambazo ni za vumbi, lakini mkandarasi yuko *site* na upande wa Mpanda pia wakandarasi wako *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ile ya *complementary* ambayo ni *CSR*, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge hasa wa Jimbo la Kasulu kwa maana ya Wilaya ya Kasulu, Buhigwe na Kibondo, miradi hii itaenda kutangazwa muda wowote. Changamoto ambayo ilikuwepo ni ile ya kubadilisha miradi ama maeneo. Miradi hii inafaddhiliwa na *ADB.* Kwa hiyo, ukibadilisha sehemu yoyote, unaingia kwenye mgogoro, lakini tunajua sasa kwamba zile changamoto zimeshaondolewa. Mapema sana kuanzia Julai, hii miradi inaenda kutangazwa ambapo itagharimu fedha isiyopungua Shilingi bilioni 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo Miradi ya *EPC*. Kuna watu wameendelea kuielezea kwa namna tofauti. Katika kipindi ambacho hatujawahi kukishuhudia ni kipindi hiki cha Serikali Awamu ya Sita kusaini mikataba ya barabara yenye Shilingi trilioni 3.7 na ushee kilometa 2,035 kwa wakati mmoja. Labda tu kwa ufupi katika mpango huu wa *EPC* tunasema ni dhana inayohusisha utekelezaji wa mikataba ya ujenzi, yaani *EPC* baina ya mkandarasi na taasisi ya umma, na kunakuwa na mikataba miwili; upande wa Wizara ya Ujenzi ni *EPC* na wenzetu wa fedha wanafanya *F*. Miradi hii ina faida kubwa sana. Moja ni kwamba

zile *risks* zote haziko upande wa Serikali, lakini hakutakuwa na *variation* na hakutakuwa na *extension*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yale makubaliano mliofanya ndiyo yatakayokuwa. Pia mkandarasi huyu ana uwezo wa kugawa maeneo maeneo. Kwa hiyo, katika barabara aliyopewa anaweza kuwa na vipande hata vitano ili aweze kumaliza haraka hizo Barabara. Vile vile kwa sababu ana uhakika wa kulipwa, kinachofanyika kwa Serikali sasa kwa upande wa Wizara, kuna watu wamehoji ubora, sisi tutahakikisha kwamba yaani anasimamiwa, anajenga kwa *specification* zilizowekwa, anajenga kwa ubora tuliouweka, na kwa sababu *design* ni ya kwake, akiharibu, kwa sababu wakati wa kukabidhi ile barabara, kila baada ya hatua ni lazima atahakikiwa. Tunafanya *verification,* pale ambapo ameharibu, gharama ni za kwake. Kwa hiyo, hatakuwa tayari kufanya hivyo kwa sababu anajua gharama itamsumbua. Hatakuwa tayari kupoteza muda, kwa sababu anajua hata akipoteza muda, hatalipwa chochote. Kwa hiyo, tuna hakika mpango huu utakwenda kuhakikisha kwamba barabara nyingi zinajengwa kwa uharaka sana, na kwa ubora mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tu ndio tulikuwa hatuaanza, lakini wale wanaosoma, ni miradi ambayo wenzetu ndio wanavyotekeleza miradi yao. Baada ya hapo ni kwamba hizi barabara zitakuwa ni barabara za kawaida, hakuna uhusiano wa *EPC + F* na *PPP,* tusichanganye. Baada ya hapo, hizo ni barabara za kawaida kama barabara zilizopo. Hizi ni *highway,* kwa hiyo, hakuna kulipia wala kufanya nini. Cha msingi tu ni kwamba hizi barabara zitajengwa kwa haraka na zikiwa zinasimamiwa na Serikali katika kila hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nitolee ufafanuzi kwa sababu kuna watu walikuwa wanapotosha, labda kutakuwa na kulipia, Serikali hakutakuwa na mkono; Hapana. Suala la fedha, nina hakika Mheshimiwa Waziri wa Fedha atalielezea vizuri sana namna fedha itakavyokuwa inapatikana na inavyolipwa. Watalipwa tu pale ambapo Wizara ya Ujenzi inasema alichofanya

ndicho hicho ambacho sisi tulimwagiza, kinyume chake ataambiwa abomoe kwa gharama zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, niseme hakika tuendelee kumpatia mama maua yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe. Tunaendelea na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi na baadaye Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti ya Serikali Kuu. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi Rehema aliyetupatia uhai hata kuchangia kwenye bajeti hizi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri iliyotukuka ya kuwatumikia Watanzania. Nina sababu nyingi sana za kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi hii ambayo anaifanya, maana amefanya, amefanya na ameendelea kufanya na kuzidi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimekuja katika Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi, Sekta ya Uchukuzi. Nitaanza kutoa ufafanuzi baadhi ya hoja nikianza na Taasisi yetu ya Usafiri wa Nchi Kavu *(LATRA)*. Kulikuwa na hoja ambayo inasema mabasi ya abiria kusafiri masaa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la saa 24, tumekaa na wenzetu wa Jeshi la Polisi na baada ya kujiridhisha kwamba usalama upo, tukatoa masaa kwamba yaanze kusafiri saa 11.00 alfajiri badala

ya saa 12.00. Baadaye tukatoa tena, baadhi ya mabasi yapatayo 68 kwamba tuanze kusafiri kuanzia tisa alfajiri na hii inafanyika. Tunakoelekea ni baadhi ya mikoa. Tunategemea mikoa yote tuanze kufanya hivi, lakini hadi hapo tutakapopata taarifa kamili za kiusalama kwamba inaruhusiwa kusafiri masaa 24. Kwa hiyo, tumeanza kama *pilot study* lakini tunaendelea na hadi hapo tutakapoanza kusafiri kwa saa zote 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja nyingine ya *TRC* kuhusu miundombinu ya Reli ya *MGR*. Ni kweli kwamba reli yetu ya kisasa inajengwa, na pia tuna reli ambayo ndiyo inafanya kazi hivi sasa. Tumeendelea kuiboresha na kuikarabati hususan katika maeneo ya kutoka Kaliua – Mpanda ambapo imegharimu takribani zaidi ya shilingi bilioni 357 na mkandarasi yupo *site* na njia ya kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora tunaendelea kuikarabati. Kwa maana hiyo, hadi kutoka Tabora – Kigoma tutaendelea kuikarabati kwa kuwa pia kuna mkandarasi ambaye yuko *site* kwa reli hii ya *MGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa kuna hoja za *SGR* ya kutoka Dar es Salaam – Morogoro yenye kilometa 300. Tayari tumefanya kwa asilimia 98.14 na 2% zilizobaki ni kwa ajili ya kuunganisha pale bandarini. Tuna hakika ifikapo mwezi wa Tisa mwaka huu, kadiri mkataba ambao tumesainiana na mkandarasi, eneo la kutoka Stesheni Kuu - Posta kwenda Bandarini litakuwa imekamilika. Hivyo asilimia 100 ya reli hii kwa kipande hiki cha Dar es Salaam – Morogoro kilometa 300 kitakuwa kimekamilika chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepokea mabehewa ya kisasa ya mfano na ya ghorofa ambapo mabehewa haya yataanza kutumika ifikapo mwezi wa Saba mwishoni, mara tutakapokuwa tumepokea vichwa vya umeme vya kuendeshea mabehewa haya. Kwa hili nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu katika historia ya nchi ya Tanzania, tutaanza kutumia mabehewa ya ghorofa ya kisasa na bora kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Morogoro mpaka Makutupora yenye kilometa zaidi ya 422 tuko asilimia 93.

Tunategemea pia ifikapo mwakani reli hii tutakuwa tumeikamilisha na kutoka Makutupora – Tabora kilometa 368 tupo 7%, kutoka Tabora – Isaka kilometa 165 tuna 3%, Isaka mpaka Mwanza kilometa 341 tuko asilimia 31 na kutoka Tabora mpaka Kigoma tayari mkandarasi yupo *site* na anaendelea na *mobilization* kwa maana ya kujenga *camp*. Hii yote ni kutaka kuunganisha pande zote za nchi yetu kutoka Ziwa Victoria mpaka Dar es Salaam baharini; kutoka Ziwa Tanganyika mpaka Dar es Salaam baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo hata kwa wenzetu wa *Mtwara Corridor* (ushoroba wa Mtwara) mara nyingi imeulizwa maswali hapa kwamba ni lini reli ya *SGR* itaanza? Nataka niwahakikishie mikoa yote ya Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma kwamba reli hii yenye kilometa 1,000 ilishafanyiwa upembuzi yakinifu. Sasa tayari makampuni zaidi ya kutoka nchi tano yameonesha nia ya kuwekeza katika reli hii. Kikwazo kikubwa ilikuwa ni kwa namna gani sheria yetu ile ya ubia tuweze kuiboresha. Tayari ile sheria imeboreshwa na Waheshimiwa Wabunge mliipitisha wiki iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kazi iliyopo, mara baada ya Mheshimiwa Rais kusaini sheria hii, tayari wakandarasi na makampuni kutoka hizo nchi wapo kutoka Uingereza, Marekani, Afrika Kusini, Croatia, Morocco na nchi nyingine. Wote wameonesha nia ya kuja kuwekeza katika *Standard Gauge* katika mikoa hii ya ushoroba wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la meli katika Ziwa Tanganyika. Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi, ninyi ni mashahidi, tumekaa kikao takribani zaidi ya masaa matatu mpaka usiku kujadili ni namna gani wananchi wetu waliopata shida kwa miaka mingi na wengine wengi wamepata changamoto ya usafiri katika Ziwa Tanganyika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Bajeti ya mwaka ujao imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa meli kubwa mbili za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo hayo, walishauri badala ya kuwa na meli moja ya kubeba abiria 600 na tani 400 ya mizigo, ni bora tuwe na meli mbili. Hili ndilo ambalo limetufanya tusisaini mkataba ambao tayari tulishampata mkandarasi, lakini ile meli ya mizigo yenyewe tutaendelea kuitengeneza na pia tutaendelea kusaini mkataba wake. Kwa maana hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika mikoa hiyo kwamba katika Bajeti ijayo, nina hakika kwamba tunakwenda kuboresha usafiri katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na suala la viwanja vya ndege. Waheshimiwa Wabunge wengi wameuliza, kwa nini ndege zetu ikifika saa 12.00 jioni, muda wa giza ukiingia nazo zinatua? Katika Bajeti ijayo tunakwenda kukarabati viwanja visivyopungua 15 na vingine ambavyo vinafanya kazi sasa. Tunaanza na kiwanja cha kwetu hapa Dodoma ambacho hakina taa. Sasa hivi taa zilizopo ni za *solar,* haziwezi kufanya kazi masaa 24. Kwa hiyo, kuna mkandarasi ambaye sasa hivi anaweka taa za kuongozea ndege usiku na mchana. Ifikapo mwezi wa Nane kiwanja hiki kitakuwa na taa, na tuna hakika tutakuwa tunatua usiku na wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa mingine ambayo tunakwenda kuboresha viwanja hivyo ni pamoja na Mkoa wa Lindi na Iringa ambapo yuko mkandarasi. Kwa awamu ya kwanza Serikali imetoa fedha, lakini awamu ya pili Benki ya Dunia ndiyo itakayokamilisha majengo pamoja na kujenga *control tower.* Vile vile kuna Mkoa wa Tanga, Sumbawanga, Kigoma, Musoma, Bukoba ambako tutajenga *control tower,* kuna Mkoa wa Arusha ambapo tunategemea tujenge taa za kuongozea ndege, nako hakuna taa, na pia kubadilisha *runway* kwa sababu iko karibu sana na barabara, ile barabara tutaihamishia upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la Chato, Msalato, Moshi ambako kuna mkandarasi lakini naye tutaendelea kumwezesha ili akamilishe Kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini.

Kuna Shinyanga, Kahama, Mpanda, Songwe, Songea, Mtwara, *JNIA*, Mwanza na Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumepokea ndege ya mizigo yenye kubeba tani 54. Ni furaha iliyoje kwamba sasa ndege yetu itaanza kazi rasmi kuruka katika maeneo mbalimbali kwa maeneo ambayo tumekubaliana kuanzia tarehe 26 mwezi huu wa Sita. Tutaanza kuruka kwenda Kinshasa, Comoros, Lusaka, Harare, India, Dubai, Lubumbashi pamoja na Entebbe. Hii ni fursa kubwa kwetu kwa kuendelea kuwekeza katika mazao, kwa maana ya ndege hii itakapokuwa inabeba mizigo, tunategemea tukauze, lakini pia kuwe na mizigo ya kuja ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona tushiriki kuchangia katika hotuba hii katika haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameuliza. Pia kuna reli ya kisasa kutoka Uvinza – Msongati – Itega yenye urefu wa kilometa 367 ambayo inafadhiliwa, ama itajengwa kwa ufadhili wa *African Development Bank* na tayari tupo katika hatua za manunuzi. Lengo kubwa la reli hii ni kwenda kuchukua malighafi zilizopo nchini Burundi *(Nickel)* na kuunganisha na reli yetu ya kisasa itakayokuwa inajengwa kutoka Tabora kuja Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete. Nilimtaja Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, ajiandae.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Mapendekezo ya Bajeti yaliyowekwa hapa mbele. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja mapendekezo haya, kwa sababu bajeti hii imelenga kumkomboa mwananchi na ndiyo maana Wabunge wengi waliochangia wanasema ni bajeti ya wananchi. Waziri wa Fedha

na timu yako, hongera sana kwa kazi nzuri mliyofanya ya maandalizi ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa nguvu zote mapendekezo haya kwa sababu Sekta ya Mawasiliano ziko hatua kubwa sana zimependekezwa kwenye mapendekezo ya Bajeti hii na sisi watu wa Sekta ya Mawasiliano tunayaunga mkono na kuwashawishi Wabunge wayaunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kuna jambo la msingi linazungumzwa kwenye Mapendekezo ya Bajeti hii, kuhusu kupeleka nchi yetu kwenye *cashless economy,* kwenye uchumi ambao hatutumii *hard cash*. Nimewasikia Wabunge wakiliunga mkono jambo hili. Jambo hili kubwa litaipeleka nchi yetu kuwa moja ya nchi ambazo zinafanya vizuri kwenye eneo hili la uchumi wa kidijitali. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kutupeleka kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna fedha zimetengwa za uwekezaji kwenye Sekta ya Mawasiliano. Tunaendelea kujenga mkongo, kupitia bajeti hii kuna fedha zimetengwa za kuunganisha nchi yetu na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na maeneo mengine ya uwekezaji kwenye Sekta ya Mawasiliano. Mheshimiwa Waziri ahsante kwa usikivu, wewe na timu yako kwa kutenga fedha kuendelea kuwekeza kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni hatua za kikodi ambazo zimependekezwa kwenye bajeti hii ambapo hatua hizi zitaenda kusaidia kushusha gharama za mawasiliano katika nchi yetu. Mheshimiwa Waziri nakushukuru na kukupongeza kwa kuitikia wito na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia. Rais Samia alituelekeza; moja, tuhakikishe Sekta ya Mawasiliano inatulia katika nchi yetu. Tukachukua hatua, na kumekuwa na kelele kwamba kumekuwa na gharama kubwa za mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuzuia gharama zisiendelee kupanda. Nilisikia juzi baadhi ya Wabunge walikuwa wakilijadili jambo hili, lakini toka mwezi wa Kumi mwaka 2022, miezi tisa mpaka sasa gharama za mawasiliano kwenye

nchi yetu hazijaongezeka, na hazijapungua *bundle*. Toka Mwezi wa Kumi mwaka jana. Kuna hatua zilichukuliwa na ndiyo maana hali ikatulia. Kwa hiyo, mtu leo akisema kuna gharama zimepanda, kwa kweli ni kupotosha. Kwa miezi tisa haijaongezeka kitu, hakijapanda chochote kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita ilichukua hatua ya kutuliza gharama zisiendelee kupanda. Hiyo ilikuwa hatua ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ilikuwa ni kuzishusha gharama hizo sasa. Kwenye mapendekezo hapa, liko pendekezo kubwa la msingi sana. Gharama za mawasiliano nchini zinachangiwa na gharama ya uwekezaji. Uwekezaji kwenye miundombinu. Hapa watu wa mawasiliano tulikuwa tunalipa Dola 1,000 kwa kilometa kwa mwaka tukipitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye *road reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyoletwa kwenye bajeti hii na ndiyo maana sisi watu wa mawasiliano tunayaunga mkono. Yako mapendekezo ya kuitoa dola 1,000 kwa mwaka kupeleka dola 100 kwa mwaka ambalo ni punguzo kubwa sana litapunguza gharama ya uwekezaji na ndiyo maana nasema hatua ya kwanza ilikuwa ni kutuliza gharama zisiendelee kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ni kuchukua hatua za kuzipunguza gharama na haya mapendekezo bila shaka ya kikodi hili la kushusha kutoka dola 1,000 kwenda dola 100, kutoka dola 1,000 kwenda dola 200 kama *initial investment* ni uamuzi wa busara utatuondoa kwenye gharama hii kubwa ambayo tumekuwa tukiitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za uwekezaji, gharama za mawasiliano moja ni hizo gharama za uwekezaji zilikuwa zinatupeleka kwenye tatizo kubwa la kuwa na gharama kubwa ya mawasiliano. Lakini ya pili kuna gharama za uendeshaji, Gharama za uendeshaji leo ukiendesha mnara mmoja wa mawasiliano kwa kutumia *diesel* unauendesha kwa shilingi 1,800,000 kwa mwezi lakini ukiunganisha huu mnara na umeme unauendesha kwa shilingi 400,000 pekeyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Bajeti hii imeelekeza upelekaji wa umeme kwenye vitongoji na Rais alielekeza kwamba umeme huu ukipelekwa uende ukaweke kipaumbele kwenye maeneo ya mawasiliano na sisi tunaamini gharama hizi sasa umeme huu ukifika tutaondoka kwenye kuendesha mnara mmoja kwa shilingi 1,800,000 mpaka kwenda kuuendesha kwa shilingi 400,000 na hizi ndiyo hatua ambazo zitashusha gharama za mawasiliano katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninaunga mkono mapendekezo haya ambayo yameletwa hapa na ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa kuelekeza uwekezaji huu mkubwa kwenye eneo hili kubwa la mawasiliano ili tumuunganishe kila Mtanzania na hasa wale walioko vijijini ambao hizi huduma zitaenda kubadilisha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mapendekezo haya na kwa hatua hizi na ni matumaini yangu kwa sababu bado kodi kwenye huduma za mawasiliano bado ziko juu. Katika kila shilingi 100 tunayolipa, shilingi 41 inakwenda kwenye kodi. Uamuzi huu wa kuondoa hii ni uamuzi wa awali. Ni matumaini yangu kwamba Waziri tutaendelea kuzungumza tuendelee kufanya mapitio kama ambavyo Rais Dkt. Samia ameelekeza, kadiri tutakavyokuwa tukiwekeza, kadiri tutakavyokuwa tukiongeza miundombinu na hizi gharama tuendelee kushuka ili Watanzania waendelee kufaidi huduma hizi za mawasiliano katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii wakati namalizia kumpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kujenga nchi yenye kupenda haki. Ameunda timu imezunguka nchi nzima kukusanya maoni na kutuletea kuona namna ya kuboresha Hakijinai katika nchi yetu. Hatuna njia nyingine, haki ndiyo itakayoinua Taifa letu. Tukitenda haki watu wetu watapata haki, Taifa letu litastawi, Taifa letu litanawiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja iliyopo mezani na ninaomba Wabunge wenzangu tupitishe Bajeti hii kwa

sababu imelenga kugusa na kuboresha maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape Moses Nnauye. Nilimtaja Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki baadaye Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nianze kwa kuunga mkono mapendekezo haya ya Bajeti Kuu ya Serikali lakini kipekee nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais lakini vilevile kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara ya Fedha kwa kuona umuhimu wa kuja na mapendekezo haya, mapendekezo ya kimapinduzi, mapendekezo ya kimaendeleo lakini vilevile mapendekezo ya Bajeti ambayo yameangalia makundi mbalimbali pamoja na sekta zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Bajeti hii ni Bajeti ambayo inataka tuelekee zaidi katika kujitegemea. Ukiangalia zaidi ya takribani shilingi trilioni 31.38 zitatokana na mapato ya ndani. Kwa kweli ni hatua kubwa sana na nitoe pongezi sana kwa Wizara nzima ya Fedha chini ya Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mapinduzi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nishukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii na ambao wameweza kugusa katika maeneo ambayo Ofisi ya Rais TAMISEMI tunayasimamia katika utekelezaji. Kulikuwa kuna hoja ambayo ilijitokeza huu mchango kuhusiana na utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo ya 10% katika halmashauri zetu kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuhakikisha kwamba mfumo huo mpya unaopendekezwa basi uwe ni mfumo rafiki kwa walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tayari kikosi cha wataalamu kinaendelea kufanya uchambuzi na mapendekezo na kimeweza kukutana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kweza kupata maoni zaidi na pindi utaratibu mpya utakapokamilika basi tutaweza kuutangaza na utoaji na urejeshwaji wa mikopo hiyo utaweza kuendelea. Niwahakikishie kwamba azma yetu ni kuhakikisha kwa kiasi kikubwa inakuwa ni mfumo ambao utakuwa na ufanisi lakini mfumo ambao utakuwa rafiki ambao utaweza kuwasaidia vijana wetu, wanawake na watu wenye ulemavu kuweza kuendeleza shughuli zao mbalimbali za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mchango kuhusiana na *TARURA* kuweza kuongezewa fedha. Kwanza nipende kumshukuru sana Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa mapendekezo ya nyongeza ya takribani shilingi bilioni 350. Mtakumbuka mwezi wa nne Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipowasilisha Bajeti yake hapa tuliweza kuwasilisha Bajeti ya takribani shilingi bilioni 855.37 kwa ajili ya *TARURA* na ukiangalia tangu miaka miwili Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alipoingia madarakani tulianza na Bajeti ya shilingi bilioni 275.03. Mwaka huu tumeweza kuwasilisha hapa Bajeti ya shilingi bilioni 855.37. Utaona ndani ya miaka miwili tu peke yake takribani mara tatu mpaka mara nne Bajeti imeongezeka lakini hiyo haikutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais bado akaweza kumuelekeza Waziri wa Fedha na wataalamu wake wakafanya uchambuzi na wametuletea mapendekezo ya nyongeza ya shilingi bilioni zingine 350 ambayo endapo Waheshimiwa Wabunge mtapitisha Bajeti hii basi *TARURA* kwa Mwaka huu wa Fedha wa 2023/2024 itakuwa ina Bajeti ya shilingi trilioni 1.235. Sasa hebu angalia kwa miaka miwili nyuma ilikuwa na Bajeti ya shilingi bilioni 275, nani kama Mheshimiwa Rais Samia? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa

Waziri kwa usikivu wake lakini zaidi kwa ushirikiano na kuweza kutambua umuhimu wa barabara katika maeneo yetu lakini namna ambavyo tutaweza kufungua maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa na vikwazo. Tutajenga madaraja ya kutosha, tutaweka vivuko lakini vilevile tutahakikisha kwamba tunakuwa na barabara ambazo zinapitika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika nyongeza hiyo tutajitahidi kwa kiasi kikubwa kuweza kuweka nyongeza katika fedha ile ya Jimbo ambayo kila Mbunge alikuwa akipata. Tutaongeza shilingi milioni 500 nyingine ya ziada ili kuhakikisha kwamba maeneo yenu mengi zaidi yanaweza kupitika na kuweza kufunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikia pia mapendekezo kwa kiasi kikubwa Waheshimiwa Wabunge wakihoji ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa. Tumeweka pia walau fedha za kutosha katika eneo hilo kupitia nyongeza hii ya Bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri Fedha amependekeza ya shilingi bilioni 350. Kwa hiyo, niendelee kuweka msisitizo tunaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuiunga Bajeti hii mkono na yote haya yametokana kwa kweli na mapendekezo yao kwa namna mbalimbali na vipaumbele vyao kwa kweli niwahakikishie tumekuwa tukivipokea na tutaweza kuvifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kweli nikushukuru sana sana sana na timu yako. Umeturahisishia kazi yetu kubwa na ninaamini haitaishia hapa na ninaamini na mwaka kesho pia mtaendelea kutuangalia katika nyongeza ya Bajeti ili walau sasa *TARURA* tuendelee kufikika zaidi kwa wananchi, TAMISEMI ya wananchi lakini zaidi wananchi wetu kule na sisi tutakuhakikishia Mheshimiwa Waziri tutakuonyesha kwa vitendo. Barabara hizi tutazielekeza katika maeneo ya uwekezaji, katika maeneo ya kiuchumi, katika maeneo ya uzalishaji ili kuhakikisha kwamba na ule mfuko pale ulipo punguza basi tuweze kukuongezea fedha nyingi zaidi na tuweze kuonyesha matokeo chanya kupitia Bajeti hii na nyongeza mliyotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kuongeza idadi ya shule za kidato cha tano na cha sita. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tumeendelea kupokea mapendekezo mbalimbali na kwenye hili pia tena niweze kuwashukuru sana Wizara ya Fedha kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo tumeona fedha nyingi zimeendelea kutolewa. Tutakuwa na takribani zaidi ya shilingi bilioni 248.5 ambazo tutazielekeza katika kuongeza miundombinu mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na shule nyingi za kutosha za kidato cha tano na cha sita. Kwenye hili pia nimshukuru Waziri wa Elimu kupitia Kamishna wa Elimu ambao walipopata mapendekezo mbalimbali ya kupandisha hadhi shule ambazo unakuta zilikuwa hazijafikia vigezo baada ya kuweka miundombinu basi wamekuwa tayari kuweza kupandisha hadhi shule hizo tunashukuru pia nao sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Asenga. Alitaka kuweza kuona Serikali inatoa tamko na haswa katika usafirishaji wa mazao yaliyo chini ya uzito wa tani moja. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kupitia jedwali la kwanza la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura ya 290 imeweka zuio la kutokutoza ushuru wa mazao kwa mzigo wenye chini ya tani moja unaosafirishwa kutoka halmashauri moja kwenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kusisitiza tu katika halmashauri zote ziweze kufuata masharti ya jedwali hili la kwanza la Sheria hii ya Fedha ya Serikali za Mitaa na tusije tukaleta usumbufu kwa wananchi wetu mbalimbali ambao wanasafirisha idadi hiyo ndogo ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kuhitimisha niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote tumesikia hoja mbalimbali kuhusu hitaji la watumishi. Tuendelee kuwahakikishia kwamba tutaendelea kupeleka watumishi kwa kadiri Bajeti ya Serikali itakavyokuwa ikiendelea kuruhusu na niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tayari tumeshapeleka takribani watumishi wa afya 5,319 na tunakamilisha mchakato wa ajira zingine 2,751 na pindi watumishi hawa watakapopatikana

pia tutaweza kuwasambaza katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za afya katika halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vifaa vya afya na vifaatiba. Nimewasikia Waheshimiwa Wabunge tumetenga katika mwaka ujao wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 116.92 ambazo tutaweza kuzisambaza katika hospitali zaidi ya 31, katika vituo vya afya 278 pamoja na zahanati mbalimbali 367 nchini na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mikoa yote mtaweza kuguswa na usambazaji huo wa vifaa na vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja kwa upande wa magari ya wagonjwa na kwenye hili pia niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tumeendelea kuyapokea tunaamini muda siyo mrefu tutaweza kukabidhi magari mawili mawili katika kila halmashauri lakini vilevile gari moja kwa ajili ya usimamizi wa huduma mbalimbali za afya na uratibu katika maeneo yenu katika halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja ya mfumo wetu wa *TAUSI*. Niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tumeendelea kuuimarisha na sasa tunatoa leseni zote za kibiashara na leseni nyingine mbalimbali katika mfumo wa kidijitali. Tuendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kusaidia kuwahamasisha wananchi wetu watoe ushirikiano na kuweza kutumia mfumo huu wa *TAUSI* kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato lakini vilevile katika kupata huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na nipende kusema ninaunga mkono hoja hii kwa 100%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na nilimtaja Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na baadaye Mheshimiwa Angeline Mabula ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii na mimi ya kuchangia

Hotuba hii ya Bajeti Kuu ya Serikali. Naomba nitangulie kusema naiunga mkono 100% na ni matumaini yangu kwamba Wabunge wote kabisa tutaunga mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwanza kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa mapendekezo mazuri sana yaliyoko kwenye Bajeti Kuu pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Katibu Mkuu Dkt. Natu, Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Bajeti na wengine wote kwa sababu wameleta mapendekezo mazuri na nitazungumzia kidogo kwenye Sekta ya Elimu na baadaye nitajibu hoja moja tu iliyotolewa ambayo ni kubwa kwenye suala la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hawa katika maandalizi yao kwa kweli wamejitahidi sana kulenga yale maono ya Mheshimiwa Rais aliyoyaelekeza na kama tunavyoona katika Bajeti na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hapa kuna vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Rais aliviweka. Elimu ni kati ya kipaumbele kikubwa sana cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa hilo kwa kweli nadhani tumpongeze sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni rahisi sana kutafuta vitu ambavyo matokeo yake unayaona sasa hivi lakini katika mageuzi ya elimu kama nitakavyosema hapo baadaye matokeo yake huwezi kuyaona mapema. Wanasema kwamba *a politician focuses on the next election; a state man focuses on the next generation.* Rais wetu anaangalia na vizazi vijavyo kwa jinsi ambavyo ameamua kuwekeza katika elimu. Baadhi ya matokeo ya mageuzi haya yatakuja wakati 2030 ameshamaliza urais wake amepumzika na matunda yake yataonekana mbele ya safari. Kwa kweli Rais wetu lazima tumpongeze sana kwa maono yake haya na hii Bajeti kwa kweli inazingatia maelekezo ya Rais wetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba nakushukuru na kukupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja baadhi ya maeneo ambayo wote tunajua. Tunafahamu na wote tumesikia elimu bila ada. Kuna baadhi ya watu wanadhani ile ada ni ndogo sana na wengine wanadhani kwamba pengine kuondoa ada kuna madhara katika elimu lakini tukumbuke tulivyoanza tu Serikali ilivyoanza kuondoa ada kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne, tulishangaa wanafunzi waliosajiliwa mashuleni idadi iliongezeka kwa ghafla sana kuonyesha kwamba kumbe tulikuwa tunaacha baadhi ya wanafunzi wanashindwa kwenda shuleni kwa sababu ya ada hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alivyoingia madarakani mara moja aliamua kuongeza elimu bila ada kwenda *form five* na *form six* na vilevile kuondoa ile ada ya mitihani ambayo kwa kweli inanufaisha familia nyingi ambazo vinginevyo baadhi ya wazazi walikuwa wanajaribu kushawishi watoto kwamba jitahidi usifaulu sana kwa sababu sina hela za kukupeleka shuleni. Tunamshukuru sana Rais wetu na tunashukuru sana Waziri wa Fedha kwa kutekeleza maagizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine tunajua kwa mfano, ongezeko la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Tunajua kwamba wakati Mheshimiwa Rais alivyoingia alikuta ni shilingi bilioni 464. Hakuacha nyongeza iende *progressively, jump* kubwa imeshafanyika sasa hivi mikopo ya elimu ya juu imefikia shilingi bilioni 731. Hilo ni ongezeko kubwa sana lakini zaidi ya hapo katika bajeti hii inabeba ongezeko la fedha ambazo wanafunzi wanazipata kwa siku kutoka shilingi 8,500 mpaka shilingi 10,000 na haya yalikuwa maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Rasi baada ya kukutana na uongozi wa wanafunzi wa elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine ambacho kinaonekana ni fedha kidogo sana, *Samia Scholarship*. Mnakumbuka wakati tulivyokuja hapa mwaka jana kuomba fedha hapa tuliomba tutenge fedha kwa ajili ya kutoa *scholarship* kwa wanafunzi wanaofanya mtihani wa *form six* kupitia Baraza la Mitihani wafaulu vizuri sana kwenye masomo ya sayansi na wakubali kwenda kusoma sayansi *(engineering* au *medicine)*.

Mliipitisha Waheshimiwa Wabunge hapa tumeiweka ile sisi baadaye Wizarani tukasema tuiite *Samia Scholarship. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shilingi bilioni tatu tulipitisha mara ya kwanza na sasa hivi tumetengewa tena fedha nyingine. Kwa hakika imetushangaza jinsi ambavyo wanafunzi sasa hivi wanaonyesha mwamko mkubwa wa kusoma masomo ya sayansi na Taifa haliwezi kuendelea bila kuwekeza katika sayansi, teknolojia na ubunifu. Kwa hiyo, hata hilo nashukuru sana Waziri wa Fedha kwa sababu maelekezo ya kutoa fedha hizi kwa ajili ya *scholarship* yalikuwa maelekezo ya Rais wetu. Kuiita *Samia scholarship* tuliamua sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hii ni Bajeti ambayo inaenda kutekeleza kazi ya ujenzi wa zile kampasi mpya za vyuo vikuu katika maeneo chungu mzima ambayo yalikuwaga hayana kampasi ya vyuo vikuu. Mikoa kama Tabora, mahali kama Singida, sehemu kama Tanga. Mikoa yote hiyo sasa hivi itaenda kuwa na kampasi za vyuo vikuu, tunaenda kutekeleza ujenzi wa vyuo vikuu 14, mchakato unaenda vizuri sana. Kuna mchakato mrefu kidogo katika taratibu hizi na *World Bank* lakini tunaenda vizuri na utekelezaji wake umebebwa na Bajeti hii ndiyo maana naomba sote tuiunge mkono na tuiunge mkono kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bajeti hii inayotusaidia kwenda kuendeleza ujenzi wa vyuo vya *VETA* ambavyo tunavijenga katika nchi nzima katika takribani wilaya 64 pamoja na Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe. Najua Wabunge wengi wote ni wanufaika wanafahamu ujenzi unaoendelea kule sasa hivi na Waziri wetu wa Fedha kwanza mwaka jana alipewa maelekezo na Rais wetu tena baada ya Bajeti ya Wizara ya Elimu kwamba hebu kaongeze ujenzi wa vyuo vya *VETA* na sasa hivi ametenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo. Tunampongeza sana Waziri wetu huyu kwa kutekeleza maelekezo ya Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika Bajeti hii, kilio kikubwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tuanze kuwaangalia wanafunzi wanaoenda vyuo vya kati ambavyo

tunasema vinatoa elimu ya amali (mafunzo ya kazi moja kwa moja) ili wanafunzi wengi waweze kumudu kwenda kusoma kule. Waziri wa Fedha ametenga fedha kwa kuondoa ada katika baadhi ya *course* wanafunzi wanaotoka kidato cha nne kwenda kusoma *DIT,* kusoma *Arusha Technical,* na *MUST. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wanaweza wakaenda kusoma kule bila ada tunapongeza sana Wizara ya fedha na mnaelekezwa na Rais wetu ni mwendelezo wa kukuza elimu ya amali ambao wako katika moyo wa mageuzi ya elimu na kadhalika. Kuanzisha programu ya kutoa mikopo sasa kwa vyuo kadhaa vya kati ambavyo ni ubunifu mwingine umeletwa na Wizara yetu ya Fedha kutekeleza maelekezo ya Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kusema, kwa upande wa mageuzi ya elimu bajeti hii vilevile imebeba bajeti ya kuanza safari ya mageuzi ambayo tumekuwa tukiyajadili hapa. Mageuzi haya kama mnavyofahamu yalikuwa ni maelekezo mahususi ya Rais wetu. Alivyoapishwa tu, nadhani wakati alifanya mabadiliko kidogo katika Baraza la Mawaziri, alianza kuelezea anachotaka kuona katika elimu. Siku ile alikuwa anapitia wizara moja hadi nyingine, wakati huo Mheshimiwa Profesa Ndalichako alikuwa Waziri wa Elimu alisema hapa Wizara ya Elimu nataka nione mageuzi ya elimu, mitaala na bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndalichako ananiona pale kazi hiyo inatekelezwa. Kwa hiyo watu wakisikia tunamsifu Rais wetu wajue tunamsifu hata wenyewe wanaweza waka-*verify*. Maelekezo mengine hamuyasikii wote lakini haya yalisemwa hadharani na alikuja akaahidi hapa Bungeni kwamba Serikali anayoiongoza itafanya mageuzi makubwa. Bajeti hii itatuanzishia safari hiyo, kwa hiyo naombeni sana tuiunge mkono kwa asilimia 100 utekelezaji wa mageuzi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niseme kitu kimoja na hili suala lililetwa na Mheshimiwa Janejelly James kuhusu wanafunzi wanaorudi kutoka nchi ambazo zina matatizo ya vita. Wanafunzi waliotoka Ukraine kwa sababu ya vita kati ya Ukraine na Urusi na wanafunzi wanaotoka Sudani kwa sababu ya

machafuko ya hali ya hewa. Nitangulie kusema nchi yetu imebaki ya amani hili tulikumbuke siku zote, tunapoona changamoto hizo, wanafunzi wanarudi hapa wanatafuta mahali pa kusoma, tukumbuke vilevile nchi yetu ina amani na amani hii inatokana na jinsi tunavyoendesha siasa zetu, kwa ustarabu, kwa kuheshimiana, kwa kuunga mkono viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa alichouliza Mheshimiwa Janejelly James ilikuwa ni kwamba sasa tumeona wanafunzi chungu mzima wameenda Muhimbili kutoka Sudan. Wale wa Ukraine vipi? Kwa nini wale hawajapata fursa ya kujiunga na vyuo vikuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitolee maelezo kidogo jambo hili na Watanzania wengine wote wasikie. Wanafunzi waliokuwa wanasoma Ukraine, baadhi yao, si wote, waliomba kujiunga na vyuo vyetu na utaratibu unaoitwa *credit counselor* ukafanyika. Baadhi yao wameweza kujiunga na vyuo vyetu, si wote. Kwa sababu utaratibu wa kuhamisha masomo unayosoma Chuo Kikuu kimoja kuja chuo kikuu cha ndani unasimamiwa na *TCU.* Kuna vigezo vingi sana vinaangaliwa baadhi yao ya wale walioomba walienda kusoma Ukraine wamejiunga na vyuo vyetu na sio wote walioomba kuja huku. Kwa wale waliotoka Sudan mpaka sasa hivi hakuna hata mmoja ameweza kujiunga na chuo chetu. Mchakato unaendelea najua kesho kuna vikao vinaanza kwa wale ambao wanataka kujiunga na vyuo vyetu ili tuangalie utaratibu wa *credit transfer* waweze kuhamisha masomo yao kutoka Sudan kuja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale walioonekana kwenye picha walipokelewa na Profesa Janabi Hospitali ya Muhimbili sio *MUHAS. MUHAS Vise Chancellor* anaitwa Profesa Pembe. Wale wanafunzi waliotoka *University of Medical Science and Technology Sudan;* wameshasoma miaka mitano wamekuja kwa ajili ya *clinical trial* kwa ajili ya *clinical training* na huu ni utaratibu. Tumepokea wote wanafunzi kutoka Zimbabwe ambao wamemaliza masomo yao ya *medicine* wanakuja hapa kuomba kufanya kazi kwenye hospitali zetu wapate *certification* halafu wanaenda ku-*graduate* kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanafunzi tuliowaona wameenda Muhimbili tunawatakia kila la heri tunafurahi wamekuja nchini kwetu, watafanya *clinical training* hapa Tanzania, na watakapomaliza watarudi kwenda kuhitimu kwenye vyuo vyao. Hao wengine walioomba tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu. Tungependa wote tuweze kuwa- *integrate of course* kuna changamoto. Kuna wengine kuna *criteria* zilizotumika kuwa-*admit* katika vyuo vyao kule sio *criteria* ambazo sisi tunatumia kuwa-*admit* wanafunzi huku. Kwa hiyo ni changamoto ambayo *TCU* inafanya. Najua kutakuwa na vikao kushirikiana na Wizara ya Elimu ya Zanzibar na kwetu na *TCU* kuona kwa wale wanaotaka kujiunga na vyuo vyetu tutatumia utaratibu gani. Kwa hiyo mpaka sasa hivi kwa kweli hatujaweza kuwachukua wale wanafunzi lakini navyojua nina taarifa kwamba kuanzia kesho kuna vikao vitaanza kuona namna ya kuwa- *integrate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize hapo narudia tena naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha na naomba wote tuiunge mkono asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia nilimtaja Mheshimiwa Angelina Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na baadaye atafatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia 100 bajeti ambayo imeletwa na Waziri wa Fedha; na nimpongeze sana pamoja na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kiasi kwamba wamerahisisha mambo mengi kwa sababu imegusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono niendelee kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameweka mkono wake kwa kiasi kikubwa sana katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanachangia Waheshimiwa Wabunge kwenye bajeti wengi walikuwa wakilalamikia tozo mbalimbali ambazo zilikuwa pengine ni changamoto kwa wananchi na namna ambavyo wengi walikuwa wanakwepa kodi. Nakumbuka kuna baadhi ya Wabunge, Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Kamonga waliongelea habari ya *capital gain*. *Capital gain* mara nyingi watu wamekuwa wakinunua ardhi au wananunua nyumba kufanya *transfer* walikuwa wanakwepa kwa sababu ya kiwango kilikuwa kikubwa cha asilimia 10. Kwa kilio kile Mheshimiwa Rais amepunguza kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 3 ni punguzo kubwa sana ambalo halijawahi kutokea. Mara nyingi tukipunguza tunakwenda kwenye *50 percent*, lakini Mheshimiwa Rais amekwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe watanzania wale wote ambao walikuwa wanasita sasa kubadilisha hati zao kuwa kwenye majina yao wabadilishe kwa sababu tayari wameshapata fursa nzuri ya kuweza kumiliki ardhi zao kwa majina yao na wakatumia pia kwa shughuli za kimaendeleo. Punguzo hili limeleta nafuu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja, walizungumza Mbunge alikuwa ananiuliza hapa kwamba na kwa wale warithi inakuwaje maana hawana uwezo. Naomba niseme kwenye suala la *transfer* kwa mrithi halipi ile *capital gain tax* kwa sababu ni *transmission* tu kutoka kwa mzazi kwenda kwa mrithi ambaye yupo kutoka kwa marehemu. Anacholipa yeye ni mambo ya *stamp duty* pamoja na ile gharama ya *registration*. Kwa hiyo nao pia watambue ya kwamba wana haki ya kuweza kumilikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimpongeze pia sana Mheshimiwa Rais na hasa katika suala zima la umiliki wa nyumba. Mara nyingi watu wengi wamekuwa wakiogopa, kwamba tunasema nyumba za gharama nafuu lakini bado walikuwa wanaona si gharama nafuu; na kubwa lililokuwa linaleta changamoto ilikuwa ni suala la *VAT*. Sasa Wizara ya Fedha wamekuja na pendekezo ambalo ni zuri kwa kushirikiana na

wizara husika ambayo tunatarajia wale wote ambao walikuwa na mpango wa kumiliki nyumba hasa zile zinazouzwa na taasisi zetu *National Housing, TBA,* Watumishi *Housing*, *NSSF,* ambazo zinaitwa za gharama nafuu sasa watazinunua bila *VAT*. Kwa hiyo nasema tu kwamba tutumie fursa hiyo kwa sababu ni namna ambavyo unaweza kumwezesha mwananchi, akiweza kuipata ile pia ataitumia katika shughuli zingine za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii haikuishia hapo tu, wengi walikuwa wakilalamika gharama za umilikishaji zilikuwa ni kubwa kiasi kwamba wanashindwa kupima na kurasimisha maeneo yao; lakini sasa gharama za kumilikisha zimepunguzwa kwa asilimia 50. Maana yake ni kwamba yeyote yule ambaye alikuwa pengine ana hofu ya kuweza kuomba hati sasa hivi imepunguzwa. Tuna viwanja 1,500,000 ambavyo tayari umiliki wake, kwa maana ya kwamba vina watu lakini hawamiliki kisheria, na wote hawa walikuwa wanaogopa kwenye suala zima la tozo zile ambazo zinatakiwa kulipwa lakini sasa hivi malipo yote yamepunguzwa. Ukienda kwenye *premium* imepungua kutoka asilimia 0.5 imekwenda 0.25 iko kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo lingine la hati kutoka asilimia 20 kwenda asilimia 10, ile *deed plan* ambayo ilikuwa inachajiwa 20,000, tunaita kiziduo kwa lugha yetu ya Kiswahili, sasa hivi unaipata bure. Sasa hivi kila kitu kimeshuka na ile kiziduo tena hakichajiwi. Niwaombe sana Watanzania bajeti hii imeleta nafuu sana katika suala zima la umiliki wa ardhi pamoja na umiliki wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliona changamoto kubwa ya watanzania katika suala zima la ulipaji wa kodi alitoa nafuu. Haijawahi kutokea Mheshimiwa Rais yeyote yule katika historia ya Tanzania, aweze kutoa msamaha kwa miezi kumi haijawahi. Sana sana tutapata mwezi mmoja, miezi miwili *maximum* miezi mitatu. Lakini Mheshimiwa Rais alitoa msamaha huo kuanzia Julai, 2022 mpaka 31 Aprili na katika kipindi hicho watanzania waliochangamkia fursa wamejitokeza kwa wingi na tumeweza kukusanya bilioni 38 lakini tozo ambayo walisamehewa ni bilioni 27 na zile zilizosamehewa Watanzania hawa wanaweza

kuzifanyia shughuli zingine. Kwa hiyo nachotaka kusema tu ni kwamba bajeti hii imegusa maisha ya mtanzania katika kila Nyanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo suala zima la uwekezaji, wawekezaji wetu nchini wamekuwa pia wakitafuta ardhi ya kuwekeza lakini imechangiwa pia na Mheshimiwa Rais kufungua nchi. Katika kipindi kifupi hichi ambacho tumekuwa nacho tumetoa ardhi kwa wawekezaji yenye hekta 29,820 ambayo imeimngiza fedha za Kitanzania trilioni 7.8 na haya yote ni ule mtaji ambao wamewekeza. Kwa hiyo, kwa maana nyingine wanaporahisisha pia masharti mbalimbali katika suala zima la umiliki wa ardhi inaleta nafuu. Na hii imekwenda mbali zaidi sasa hivi, ukiangalia ile Sheria ya Uhamiaji namba 54 nayo pia kwenye habari ya *resident permit* imepunguzwa pia imewekwa kiasi cha dola 150. Mwenye mtaji wa dola 150,000 anaweza kujenga nyumba yake na anaweza akauza kama watanzania wengine na hii inafungua fursa pia kwa *Diasporas* ambao watatambuliwa kwa hati maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunasema bajeti hii inakwenda kugusa kila mmoja lakini inakwenda kukuza pia mtaji katika sekta ya nyumba ambako pia wawekezaji wamepewa fursa. Mara nyingi tulikuwa tunalalamika kwamba wawekezaji hawapewi fursa. Maana yake ni kwamba akijenga nyumba haondoki nayo, akikiuka masharti ya nchi manake ataondoka atatuachia nyumba yetu, hapo tayari atakuwa ameshaendeleza mji. Kwa hiyo hili nalo limeleta nafuu kubwa katika suala zima ambalo lilikuwa likipigiwa kelele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote katika suala zima la bajeti ya mwaka huu, ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana; mwaka jana kwenye fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo zilikuwa ni bilioni 27 lakini mwaka huu fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ni bilioni 82.13 sawa na ongezeko la asilimia 203 haijawahi kutokea. Ndiyo maana nasema Mheshimiwa Rais kwa kweli amefanya jambo la msingi sana na tukiangalia ardhi ndiyo sekta wezeshi katika maeneo mengine yote. Unapokuwa umewezeshwa katika suala zima la kuwa na *program* hii ya

maendeleo ya sekta ya ardhi kwa kiasi kikubwa hiki tunachokipata ni utekelezaji wa kuzingatia sheria namna ambavyo Watanzania tunatakiwa tuzizingatie. Hii kwetu imekuwa ni rahisi kwa sababu tunakwenda kuwekeza pia katika miundombinu ya upimaji ambayo ilikuwa ina shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati mnachangia Wizara ya Ardhi mlipiga kelele sana kuhusiana na suala la kwenda kwenye vijiji, kwamba vijiji vilikuwa vichache. Kilio hicho kimesikika na kwenye bajeti kimeoneshwa ya kwamba sasa vijiji vitakavyokwenda kupimwa ni vijiji 2000 ambavyo vimeongezeka kutoka vile vijiji 250 vilivyokuwepo. Katika upimaji wa hivi vijiji pia vinatoka katika vijiji 1,059 ambavyo tayari vina mpango wa matumizi. Na katika suala hili kwa sababu tunahitaji pia kuona kwamba uwekezaji mkubwa unaenda kwenye sekta ya kilimo. Tumekuja kukubaliana na wenzetu wa kilimo kwamba, ardhi yote ya kilimo ambayo inafaa kwa kilimo itatambulika na itatangazwa katika gazeti la Serikali ili iweze kutunzwa kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambao watapata fursa ya kupewa maeneo yale kwa ajili ya kilimo, niwaombe sana watimize masharti ambayo tunahitaji pengine kila mwekezaji anapopewa aweze kutumia eneo lake kwa faida na kama jinsi alivyoomba. Kuna wengi wanapewa ardhi lakini wanaiacha na watu wanavamia tunakuwa na migogoro. Naomba sana katika wale ambao watapata fursa ya kumilikishwa ardhi kipindi hiki niwaombe sana kwamba watekeleze masharti yote yanayotakikana ili tuweze kuondokana na kero ambayo tulikuwa nayo katika kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yamefanyika katika sekta hii ya ardhi ambayo mara nyingi imekuwa na migogoro mingi lakini kwa hiki ambacho kimefanyika katika bajeti ya mwaka huu tuna imani tunakwenda kuboresha na hasa mifumo ambayo tayari tumekwishaanza. Sasa hivi ukiangalia hata usafishaji wa takwimu zetu, kwa maana ya *data cleaning* inaendelea kufanyika na nyingi zimefanyiwa tathmini na kuweza kurekebishwa, na tunakwenda kupata taarifa zetu kupitia

kiganjani. Tulikuwa tunazungumzia habari ya maji unaweza kupata bili ukalipa sasa hivi pia kwenye sekta ya ardhi imekwishaanza na watu wameshaanza kupata taarifa zao kiganjani kama una deni unaletewa pale na unaweza kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo haya yote ni kwa sababu tu tumewezeshwa kama wizara kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda sawa. Ninakushukuru nimekuibia dakika zako mbili lakini Mungu ni mwema nimemaliza niliotaka kusema, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Angelina Mabula. Nilimtaja Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo baadaye Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Maliasili na Utalii ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi. Pili nimshukuru sana Waziri wa Fedha na Wizara ya Fedha kwa ujumla. Katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, katika mpango wa mwaka ujao wa fedha amesema wazi kabisa, katika miradi ya kielelezo na miradi ya kipaumbele, miradi ya umwagiliaji itakuwa ni eneo la kwanza ambalo Serikali itaweka fedha. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *guidance* anayotupa na maelekezo anayowapa wenzetu wa Wizara ya Fedha kuangalia uwezekano wa kuweza kuweka kipaumbele katika eneo hili la kilimo namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wametoa ushauri na wamesema mambo mengi. Kwanza nitumie Bunge lako Tukufu kuwaambia kwamba kwa mara ya kwanza tangu tumepata uhuru uzalishaji wa zao la kahawa tumefika *metric tons 82,000* ambazo tumeziuza mwaka huu. Vilevile zao la tumbaku uzalishaji wetu sasa hivi unakwenda tani 120,000. Hizi zote ni *effort* ambazo Mheshimiwa Rais amefanya na tunaendelea na masoko

na masoko yanaendelea vizuri tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hali inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea eneo la mafuta ya kula na eneo la ngano. Nataka nitumie nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge tumewasikia na tumekaa na Wizara ya Fedha tumekubaliana tutakuwa na *tax measures* na tutakuwa na *administrative measures* ambazo zitaonekana kwenye *finance bill* ambazo zitafanya uzalishaji wa mafuta tuweze kuwa na *tax* ambazo zinaweza kumlinda mkulima. Serikali inaweka fedha tumegawa mbegu nyingi sana za ruzuku na safari hii mashamba yetu yote ya kuzalisha mbegu yatakuwa yanatumia *pivot technology*. Mwenyezi Mungu akitujalia mpaka kufika mwishoni mwa mwaka huu baadhi ya mashamba ambayo yamefungwa mifumo ya umwagiliaji ya kutumia *technology* ya *center pivot* yataanza kufunguliwa ili tuweze kuzalisha mbegu mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana suala la tija. Ni ukweli kwamba mchango wa sekta ya kilimo na ukuaji wa sekta ya kilimo hauakisi tamaa tulionayo kama Taifa. Ili tuweze kufikia huko ni lazima tuwekeze kwenye tija. Serikali inafanya jitihada kubwa sasa hivi ya uwekezaji kwenye maeneo ya kuongeza tija. Mmepitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo na Bajeti Kuu ya Serikali; na mwaka kesho mtaona tunaanza kutekeleza miradi katika majimbo yenu ya kuchimba visima kwa ajili ya wakulima wadogowadogo na kuwawekea *irrigation kit* ya hekari 2.5 kila mkulima ili wakulima waweze kuzalisha kwa wingi na waweze kuwa na uhakika wa kuzalisha kuwa na *resilience* kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uwekezaji, tumeshatangaza *tender* sasa hivi za kufanya *feasibility study* na *detail design* kwenye mabonde yote 33. Na ninawashukuru Wizara ya Fedha kwa kutupa kibali. Tumeshatangaza tender na mikataba imeshasainiwa wakandarasi wanaanza kufanya *feasibility study* kwenye mabonde ya Ziwa Victoria, *Lake Tanganyika Lower Basing* ya Ruvuma na mabonde ya Rifiji. Yote haya tunayafanyia

*detail design* ili tuweze kuanza mipango ya kujenga miradi ya umwagiliaji ili Mwenyezi Mungu akitujaalia tukikamilisha hizi zaidi ya hekta laki tatu na kitu zitatuongezea eneo kubwa la uzalishaji wa mwaka mzima katika maeneo tunayofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine Wabunge waliongelea pamba, wakatoa *concern* yao kuhusu bei. Nataka niwakumbushe mwaka 2020/2021 tulianza msimu kwa bei ya shilingi 800 tulimaliza msimu kwa bei ya 1200. Mwaka 2021/2022 tulianza na msimu kwa bei ya shilingi 1500 tukamaliza msimu na bei ya shilingi 2200. Mwaka huu tumeanza na bei ya 1060 ninaamini kwamba bei ya pamba itaimarika namna ambavyo *competition* inavyoongezeka na soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ambayo tunaongea na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha, ni kutengeneza mfumo ambao utatufanya sisi wakati wakulima wanalima, wanavuna, wanapata *assured good price* na tunahifadhi, tunaenda katika mfumo wa *TMX* na kuangalia namna gani tutawasaidia waongezaji wa thamani, waweze kuongeza thamani ya pamba yetu na kutengeneza *financing scheme*. Tuko kwenye majadiliano na Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara, naamini ndani ya miaka miwili, mitatu tutafika katika eneo hilo. Hii ni safari haiwezi kutokea haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamaa yetu ya kuwa na *stabilization fund,* kama mtakumbuka mwaka jana wakati tunapitisha *Finance Bill* tulianzisha *Agricultural Development Fund* hapa ndani ya Bunge. Sasa hivi tuko hatua za kukamilisha kanuni ambapo tutakuwa na Mfuko wa Fedha ambao unatumika kwa ajili ya kuwalinda wakulima wetu na changamoto za masoko ili pale ambapo wanapata hasara tuweze kuwa–*cover. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo na mlimsikia akiwa Mwanza, alitoa maelekezo ya kuiongezea fedha *National Food Reserve Agency,* tumepata *approval* ya bilioni 320 na tumeshaanza kuzitumia hizi fedha. Nawashukuru sana Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaweka fedha kwenye *National Food Reserve Agency?* Pia sasa hivi tumetangaza *feasibility study* kwa ajili ya kuongeza uwezo wetu wa kuhifadhi. Mpango wa Serikali katika kipindi cha miaka mitano mpaka minane ijayo tuwe na uwezo wa kuwa na maghala ya kuweza kuhifadhi mazao yasiyopungua tani milioni saba ndani ya nchi yetu. Kwa kutumia njia hiyo ndiyo tutaweza kuwalinda wakulima wetu na kuweza kujiwekea usalama wa chakula katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetupatia fedha kwa ajili ya Kampuni ya Serikali na niwapeni *good news,* tulifanya majaribio *TFC* na Profesa Mkenda ametoka nataka nimshukuru mbele ya Bunge hili, akiwa Waziri wangu ali–*champion* hili jambo. Leo *TFC* tumeipatia fedha, baada ya kuipatia fedha imefanya biashara ndogo na imepata faida. Matokeo yake Wizara ya Fedha wametuelewa, wametupatia bilioni 40 kwa ajili ya kuipa *TFC* na tumepata dola milioni 25 kwa ajili ya kuipa *TFC* na sasa hivi *TFC* imeshaagiza mbolea kutoka nje ili tuwe na mbolea ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoto ya nchi kuwa na *blending facility* ambayo Serikali ina *share, TFC* sasa hivi tuko kwenye maongezi ya mwisho na *OCP,* lakini niwahakikishie Wabunge tusipoelewana na *OCP* tutawekeza wenyewe *facility* ya ku–*blend* mbolea ndani ya nchi na tutafuta wawekezaji wa Kitanzania kuwakabidhi waweze ku–*run* hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie wakulima wa korosho, nimesikia kilio cha kwamba mfumo tuliouweka na *equation* tuliyoiweka ya miche 100 kwa mfuko mmoja tumeshawaagiza Bodi ya Korosho wafanye *review* na mgao wa pili utakapotoka watatoa kutokana na idadi ya mikorosho na ukubwa wa mikorosho. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa korosho, wakulima sasa hivi wanapokea pembejeo kwa kutumia teknolojia ya *biometric*, tuendelee kuwahamasisha wajisajili. Akijisajili akiwa na namba yake hata wakati wa kuuza korosho atauza korosho kwa kutumia namba yake aliyosajiliwa nayo ili

tuwaondoe hawa wote ambao wanachukua mazao ya wakulima katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Wabunge wamekuwa wakisema sana. Wabunge wa Nyanda za Juu Kusini, naomba niwahakikishie, Wilaya ya Makete msimu ujao ngano tunawapa ruzuku ya tani 1,000 kwa ajili ya kwenda kufanya *pilot*. Wamefanya majaribio na niishukuru Halmashauri ya Makete kutoa *ten percent* kuwapa wale wakulima katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge matarajio tuliyonayo, Rais ana nia na Wizara ya Fedha imekuwa *flexible* kwa ajili ya kutoa fedha. Ndani ya miaka miwili, mitatu tutayaona matokeo makubwa katika sekta hii kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa Waziri wa Maliasili na Utalii na baadaye Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango atajiandaa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru, kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini nimshukuru sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Lazima tukiri kwamba wakati fulani Taifa letu linahitaji kufanya maamuzi magumu sana ili tuweze kupiga hatua za maendeleo na sisi kizazi cha leo tunatambua waasisi wetu waliotangulia wa Taifa hili kuanzia kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuja kwa Rais wetu wa Awamu ya Sita yamefanyika maamuzi mengi magumu ambayo yamelifanya Taifa hili kuwa Taifa imara, yamelifanya Taifa hili kuwa Taifa lenye amani na utulivu na mambo mengi kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuchukua hatua muhimu kabisa za uchumi katika Taifa letu. Tunampongeza sana Rais wetu kwa kuendelea

kuchukua maamuzi magumu ya kiuchumi na Baba wa Taifa aliwahi kusisitiza miaka ya 1961 wakati wa *Arusha Manifesto*. Sisi katika Sekta ya Utalii Baba wa Taifa aliyaondoa na kuyapandisha hadhi baadhi ya maeneo ili tuweze kuhifadhi na alisema kwamba tutafanya kila tuwezalo ili tuweze kuhifadhi, kwa sababu uhifadhi si tu kwa ajili ya kustaajabishwa na wale wanyama lakini bali tunahifadhi ili iwe mustakabali wa kizazi cha leo na kizazi cha kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema Hotuba ya Waziri wa Fedha, kwanza nimpongeze sana na sisi tunampongeza na kumtia moyo aendelee kufanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika eneo hili la fedha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Dkt. Samia kwa mara ya kwanza kabisa alifanya maamuzi magumu ya kutoka ofisini na kwenda kuitangaza Tanzania kupitia Filamu ya *Royal Tour* na watu wengi walibeza. Watanzania wengi walizungumza maneno mengi sana kuhusu ni kwa nini Mheshimiwa Rais leo hii ametoka ofisini na kwenda kuitangaza Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha amezungumza kwa kina mapato yaliyopatikana kutokana na utalii ambayo yametokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi tunasema tutaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na wakati mwingine Taifa letu kama ambavyo nimesema tunahitaji kufanya maamuzi magumu na maamuzi haya aliyoyafanya, anayoendelea kuyafanya katika uchumi, katika sekta yetu ya utalii ni maamuzi ambayo yatalifanya Taifa hili kupiga hatua sana kwenye sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge wengi katika hoja walizozizungumza hapa kwa mara ya kwanza kabisa tumewaona Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana kuhusiana na utalii. Katika miaka mingi sana tumekuwa tukizungumza kuhusu hifadhi. Msingi wa uhifadhi ulianzia nyakati za Baba Taifa, utalii haukuzungumzwa kwa muda mrefu sana kwenye Bunge hili katika miaka mingi sana, lakini

tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana kuhusu utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba maeneo mengi ambayo wametushauri, tutakwenda kuyafanyia kazi. Hoja nyingi ambazo zilikuwa zinakwama kwa sababu ya urasimu kwenye Sekta ya Utalii tutakwenda kuzikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukiri na kumshukuru Mheshimiwa Rais. Tulipoteuliwa kwenye nafasi hii mimi na Mtendaji Mkuu katika Wizara hii, tumeingia katika nyakati ambazo tumekuta kuna changamoto nyingi sana katika sekta ya uhifadhi. Tumekuta kuna changamoto nyingi za wanyama wakali, kuna changamoto nyingi za wanyama waharibifu na lazima nisimame hapa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, toka tulipoanza kujadili Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, tukaja kujadili Bajeti hii Kuu kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa, alisema moja kwa moja. Katika misingi ya Ibara ya 21, wananchi wengi wanawakilishwa leo hii Bungeni na Wabunge waliochaguliwa na wananchi. Sauti za wananchi zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao yote tukianzia kule kusini mpaka magharibi na maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitambue mchango wa Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Kitandula ambaye pia amezungumza kwa uchungu sana kuhusiana na matatizo ya uhifadhi, matatizo ya ndovu katika eneo la kule Jimboni kwake. Sisi kama Serikali ni lazima tujitafakari sana kwenye eneo hili, kwa sababu michango mingi iliyozungumzwa nikiri kabisa kwamba kama Serikali tusipochukua hatua za haraka tatizo hili linaweza kuwa kubwa zaidi hata ile dhamira ya uhifadhi tunaweza tusiione. Dhamira ya Baba wa Taifa kuhusu uhifadhi tunaweza tusiione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Serikali lazima tukajipange na nimewaambia wenzangu kila mmoja kwenye

eneo lake tujipange hasa. Tunatambua kwamba eneo hili linahitaji fedha nyingi na Baba wa Taifa alisema kwamba pamoja na kwamba uhifadhi ni faida kwa Taifa letu lakini peke yetu hatutaweza ni lazima tupate msaada kutoka maeneo mbalimbali. Mashirika ya Kimataifa, lakini nilipotoka hapa asubuhi nilikuwa nateta na Waziri wa Fedha kumwomba zipo fedha ambazo zimetengwa kwa mujibu wa sheria na hizi kwa muda mrefu zimekuwa hazitufikii Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi ni gharama kubwa. Wahifadhi wetu wanafanyakazi kubwa na kazi nzuri sana, kazi ngumu sana pamoja na changamoto nyingi ambazo tunaendelea nazo lakini lazima tukiri kwamba changamoto la wanyama wakali ni janga ambalo tunahitaji kama Serikali kujipanga hasa ili tuweze kulimaliza. Inawezekana changamoto hizi zikawa zimesababishwa na pande nyingi; upande wa wananchi wanaweza wakawa na mchango wao, lakini sisi pia kama Serikali lazima tujipange hasa kwa sababu ipo mipango mingine ambayo inapangwa bila kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii wakati mwingine, ndiyo inapelekea leo hii tunajikuta kwamba tuna matatizo mengi ambayo tunahitaji kwenda kuyatatua na matatizo haya yanahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nateta pale na Waziri wa Fedha kuona ni namna gani wataweza kuendelea kutusaidia kwa sababu mchango wa sekta hii hauwezi kudharauliwa. Sekta hii inatoa mchango kwa asilimia karibu 25 fedha za kigeni na kwa fedha za ndani *GDP* mchango zaidi ya asilimia 22, lakini mchango huu ni mdogo. Tunaamini kabisa tukijipanga vizuri tukaweka mikakati mizuri ya uhifadhi na utalii tukaweza kudhibiti wanyama wakali, tukaweza kutengeneza sera nzuri, tukadhibiti ubadhirifu wa fedha, tukadhibiti rushwa katika uhifadhi, tukadhibiti rushwa katika uwekezaji wa uhifadhi. Naamini kiasi hiki ambacho leo hii tunakiona asilimia 25, asilimia 21 kwenye pato la Taifa, basi tunaamini kabisa tunaweza kuvuka lengo na kufika mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha amenithibitishia, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mwenyekiti wa

Kamati, alipokuwa anazungumzia suala la *retention* na fedha nyingine za kisheria ambazo zinapaswa kuja kwenye Wizara. Waziri wa Fedha amenithibitishia na yeye ni msikivu sana, naamini tutakaa pamoja kuweza kuona ni namna gani tunawenda kumaliza changamoto hizi kwa kupata fedha ambazo ameniahidi kwamba Wizara itapata ili tuweze kuzimaliza hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na michango mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika Bunge lako hili tukufu pamoja na mambo mazuri ambayo Waziri wa Fedha ameyazungumza. Sisi kama Wizara tutaendelea kujipanga vizuri. Naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, tunatambua Wizara yetu ina–*cover* karibu asilimia 50 ya nchi yetu, asilimia 50 ya nchi yetu ipo ndani ya hifadhi. Tuna kazi kubwa kila mmoja wetu na sisi tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge, wawakilishi wa wananchi, kama ambavyo wameweza kuzungumza kwa kina hapa kuhusu changamoto za wananchi kwenye maeneo yao, tutafika huko, tutakwenda tuweze kuona namna gani tunatatua changamoto ambazo zinawakabili katika maeneo ambayo Wabunge wanawawakilisha wananchi kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuwathibitishie Watanzania, changamoto hizi zimepata mwenyewe na mwenyewe si mwingine ni huyu Mndengereko. Tutakwenda kuhakikisha kwamba changamoto hizi tumezimaliza, tutafika kusini, tutafika magharibi, mashariki na kaskazini kuhakikisha kwamba mzigo huu tuliokabidhiwa tunautendea haki na Watanzania wawe na furaha na nchi yao katika nyakati zote za masika na kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mdogo nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa. Sasa namwita Mheshimiwa Hammad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aweze kuchangia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami kuwa sehemu ya wachangiaji katika hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uzima wa afya ambayo ametujalia, tumekaa hapa, hatimaye tunaenda kufikia ukingoni kwa hoja hii iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba sana nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza sana. Mheshimiwa Rais, mbeba maono wa Taifa hili, mwenye macho haambiwi tazama. Mbeba maono maana yake siyo tu kwamba anahamisha sera kutoka kwenye makaratasi na kuzipeleka kwenye vitendo, bali hata salamu mama anaipeleka kwenye vitendo ana uwezo mkubwa sana wa kutafsiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliposema Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee, hiyo ni salamu. Tumeona leo dhahiri kabisa salamu hii imetafsiriwa kwa vitendo, hakuna Wilaya, hakuna Halmashauri ambayo hakuna maendeleo au mradi wa maendeleo ambao unafanyika kule. Miradi yote mikubwa tuliyonayo inatekelezwa kama *SGR,* umeme mpaka vijijini, Bwawa la Mwalimu Nyerere, mama ameenda kulitekeleza kwa vitendo. Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi na hii haikuja burebure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais yeye ni neema na ni baraka kutoka kwa Mungu. Kwani ukiniruhusu naweza toa tafsiri kwa ufupi tu. Jina la Mama anaitwa Samia Suluhu Hassan, utanisamehe naenda kwenye kiarabu kidogo, watu wa nahau wanasema "*inna samian suluhuun hassanaah*" kwa hakika Mama huyu ni msikivu wa kusikiliza changamoto za wananchi wake na kuzipatia ufumbuzi mzuri hiyo ndiyo tafsiri yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya zote leo lipo vumbi linapeperuka kwa sababu ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, lakini ujenzi wa madarasa, kila kitu. Hii kwa sababu ya tafsiri la jina lake haikuwa bure bure, hii ni neema. Kwa hakika Mama ni msikivu ambaye anasikiliza changamoto za wananchi wake na kuzipatia ufumbuzi ulio mwema. Siku ukiwa na

muda mzuri tunaweza kutia irabu kwamba *inna* ni nini, *samian* ni nini? na *suluhu* ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ni mbeba maono kweli kweli. Nimpongeze sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Viongozi wetu hawa wanasimama imara kutuelekeza na kusimama imara katika kujenga maendeleo ya Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Wahenga hunena: *"kijua ni hiki tusipouanika tutaula mbichi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nikisema hivyo mnanifahamu? Huu ndiyo wakati, huu wakati wa leo, sasa ndiyo wa kujenga maendeleo yetu, ndiyo wa kuchagiza maendeleo ya nchi hii. Ni wakati huu na siyo wakati mwingine, ndiyo maana unasema kijua ni hiki usipouanika utaula mbichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wangu, Dkt. Mwigulu Nchemba, *mentor* wangu, bosi wangu, kwa kiasi anavyonikuza kisiasa lakini na kikazi. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mungu akubariki sana. Wewe ni mtu mwema sana, ni mtu wa kipekee, nakushukuru sana na nakuhaidi kwamba nitaendelea kushirikiana na wewe katika utendaji wa kazi pamoja na wataalam wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza sana Wabunge, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa namna wanavyotushauri, kutuelekeza lakini hata kutoa mapendekezo yao, hongera sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa nini nawapongeza Waheshimiwa Wabunge? Waheshimiwa Wabunge wanaishi katika maneno ya hekima yaliyosemwa kwamba aliyekufanyia wema, basi mlipe mithili ya wema aliyokutendea, kama huwezi kufanya vile basi mwombee dua, mwombee kwa Mungu. Waheshimiwa Wabunge wanaishi katika hekima hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno yalisemwa kwa Kiarabu; *"Tatamanswana maarufa alaykum au manswanaa alaykum maarufa fakatiuhu,"* maana yake aliyekufanyieni wema mlipeni *"fainlam tajiduu"* mtakapokuwa hamuwezi basi *"swallu alaiy,* mwombeeni dua. Waheshimiwa Wabunge nyinyi mnaishi katika hekima hii, kila Mbunge aliyenyanyuka alimshukuru na kumpongeza na kumwombea dua Mama yetu, kila Mheshimiwa Mbunge. Wabunge wote mnaishi katika hili, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, nasikia, huko mitandaoni, nasikia, toba sikio. Wako wanaosema kwamba wanabeza Bunge, wanabeza Bunge hili, wako wanaobeza Bunge hili, lakini niwaambie Wabunge taingia katika historia maalum, ya wakati maalum, ya siku maalum na kwa tukio maalum. Majina yenu yataandikwa kwa wino mahususi, wino wa dhahabu, kwa sababu wamechapa kazi sana, nani ambaye haoni leo Waheshimiwa Wabunge wanavyopambana? Ni Wabunge wangapi leo siku zote maana yake ukiamka tu asubuhi simu wanadai maendeleo ya Majimbo yao. Waheshimiwa Wabunge hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze wataalam wetu wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Natu Mwamba na Manaibu Katibu wakuu na Wataalam wote nawapongeze sana, kwani usiku na mchana hawa wanafanya kazi. Wanafanya kazi mpaka usiku wa manane na asubuhi mapema kabisa wameshafika ofisini, nisiwe mchoyo wa fadhila, niwashukuru sana wataalam wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo, naomba tu niseme kwamba ushauri wote ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo na maoni tumeyapokea na tunawahakikishia tunaenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni wa dondoo ndogondogo ndiyo hoja ambazo zimetajwa na Waheshimiwa Wabunge niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge. Walipokuwa wanachangia wengi wametoa hoja kwa njia ya

ushauri, wametumia hekima kubwa sana, hongera sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja moja ambayo ilizungumzwa Serikali ihakikishe kwamba inafuatilia au inatafuta mikopo ya gharama nafuu. Serikali imekuwa ikifanya juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba mikopo yote ambayo inaingia Serikali ni ile yenye masharti nafuu na tunawahakikishia kabisa mikopo hii inaenda kutumiwa katika zile sehemu ambazo ni vipaumbele vya Taifa hili ya mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. Vipaumbele vya Taifa hili ambavyo tumeviweka ndiyo mkopo huu unaenda kutumika, hautotumika tofauti na vipaumbele ambavyo tungeweka ili kusudi kupunguza gharama ambazo siyo za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja imesemwa kwamba Serikali iboreshe mikakati na ikusanye mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani. Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuongeza wigo wa mapato kwa kusajili biashara na walipa kodi wapya. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaandaa mikakati maalum, tutaendelea kuitumia mikakati ambayo imeandaliwa na Serikali kuhakikisha kwamba tunapata ongezeko kubwa sana la mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu ambayo tumeweka, ni kupata mapato ya ndani kwa asilimia 70.7 ikilinganishwa na bajeti iliyopita au ambayo tuko nayo leo ya kupata asilimia 67.5. Niwahakikishie kwamba tutapambana, tutajitahidi kutumia maarifa yetu yote, tuone kwamba ongezeko la mapato limepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu sisi wote tuwe mabalozi wa kuwa na utamaduni mwema. Tuwe na utamaduni wa kudai risiti na kutoa risiti kwa wale wafanyabiashara. Tufanye kama utamaduni wetu, kama vile ukiamka asubuhi unaenda kukosha uso, kupiga mswaki na kukoga, basi tufanye hivyo, kila unapokwenda dukani kutafuta bidhaa yoyote, basi dai risiti na wale wanaofanya biashara watoe risiti jambo hili litatusaidia sana. Hakuna mtu anayetoka mbali kuja

kujenga maendeleo yetu kama siyo sisi wenyewe. Kilio kina mwenyewe, wewe mwenyewe ndiyo unajua uchungu wa nchi yako. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuwe mabalozi wa kujitahidi kudai risiti na pia nakutoa risiti kwa wale wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja ya wakandarasi kwamba kuna madeni mengi sana ya wakandarasi. Tulikuwa tunateta hapa na Mheshimiwa Waziri. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba wakandarasi hao ambao *certificate* zao tayari zimeshawiva, mapema mwaka ujao wataenda kulipwa bila wasiwasi wowote. Serikali yetu iko tayari kuwalipa wakandarasi hao hasa hasa wale wakandarasi wadogo ambao tukiwaachia muda mrefu hawajalipwa wanaweza kufilisiwa kama walivyosema Wabunge. Hilo halitotokea katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge baadhi yao wapo wamezungumzia hoja ya kujengewa ofisi za *TRA* au Forodha mipakani. Niwahakikishie, kwa mfano kama Loliondo, Iramba kwa bosi wangu, Mkalama, Itilima na kwingine ofisi hizi zitaenda kujengwa hivi karibuni, mwaka wa fedha unaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme naunga mkono hoja. Wale waliosema mama apewe maua yake mimi naongezea siyo tu maua, mama apewe maua yake na matunda yake yale yaliyo mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wetu wa Fedha na Mipango kwa kutukamilishia mchango huu wa Waheshimiwa Mawaziri kwa siku ya leo.

Nitumie fursa hii kuwapongeza Wabunge wote, kwa kweli tokea tumeanza kazi hii ya kuishauri Serikali na hasa sasa tunaelekea kwenye ukingo wa kazi yetu ambapo leo

tumekamilisha wachangiaji Mawaziri ambao wamejibu hoja mbalimbali na maswali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yaliibuka katika kipindi chote hiki, lakini jumatatu tukijaliwa uzima na afya na naamini Mwenyezi Mungu atatujalia, tutaweza kumsikiliza Mheshimiwa wetu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba akihitimisha hoja yake na pengine kukamilisha yale ambayo Wabunge wengi wamekuwa wanatamani kuyasikia.

Kabla sijaaihirisha shughuli za leo, kuna tangazo moja nafikiri ni muhimu linatoka kwenye Kamati ya Maandalizi ya Bunge Bonanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa kuwa kesho siku ya Jumamosi tarehe 24 Juni, 2023 itakuwa ni siku ya kazi ambapo kutafanyika Tamasha la Pili la Michezo na Burudani ijulikanalo kama "*Grand* Bunge Bonanza" lenye kauli mbiu "Tupende Michezo, Tujenge Taifa Letu".

Aidha, Bonanza hilo liatahusisha michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa meza, kutembea kwa haraka, kurusha vishale, kuvuta kamba, kurusha tufe, riadha, kukimbia na gunia, mchezo wa bao, mchezo wa karata na kufukuza kuku. (*Makofi)*

Lengo la Bonanza hili ni kuhamasisha Wabunge na Watumishi wa Bunge kufanya mazoezi kwa ajili ya kujenga mwili, kuimarisha afya, kutoa burudani, kuimarisha na kuendeleza ushirikiano kama Taasisi, hivyo kuongeza tija katika kazi. Bonanza hili ambalo linadhaminiwa na Benki ya *CRDB* litaanzia katika Kituo cha Mipango saa kumi na moja na nusu asubuhi kuelekea shule ya Sekondari ya John Merlin Miyuji, Jijini Dodoma ambapo michezo hiyo itafanyika.

Baada ya Bonanza kukamilika baadaye kutakuwa na tafrija kuanzia saa kumi na mbili na nusu jioni katika Viwanja vya Bunge ambapo kutakuwa na burudani kama vile kucheza *dance*, uimbaji, ngoma za jadi na utamaduni, ushairi na utenzi, kuimba taarabu, muziki wa kufoka *(Rap Music),* maonyesho ya mavazi na

ucheshi na Mgeni Rasmi katika matukio yote atakuwa ni Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

Waheshimiwa Wabunge, kwa tangazo hili kikao kilichotangazwa kufanyika baada ya kuahirisha Bunge leo jioni hakitokuepo tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, basi nawatakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu akijalia naahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe 26 Juni, 2023 siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.50 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 26 Juni, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*